

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA SITA**

**Kikao cha Saba – Tarehe 11 Septemba, 2019**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Maelezo ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya pamoja ya ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur kuhusu Uwajibikaji Kisheria na Fidia kwa Madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya Bioteknolojia ya Kisasa katika kutekeleza Itifaki ya Cartagena (*Nagoya – Kuala Lumpur Supplementary Protocol on Liability and Redress on Cartagena Protocol on Biosafety*).

**MHE. OMAR A. BADWEL - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya pamoja ya ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur kuhusu Uwajibikaji Kisheria na Fidia kwa Madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya Bioteknolojia ya Kisasa katika kutekeleza Itifaki ya Cartagena (*Nagoya – Kuala Lumpur Supplementary Protocol on Liability and Redress on Cartagena Protocol on Biosafety*).

Azimio la Bunge la Mkataba wa Marakesh ya mwaka 2013 unaolenga kuwezesha upatikanaji wa kazi zilizochapishwa kwa watu wasioona wenye uoni hafifu au ulemavu unaomfanya mtu kushindwa kusoma.

**MHE. JOYCE J. MUKYA - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya pamoja ya ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur kuhusu Uwajibikaji Kisheria na Fidia kwa Madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya Bioteknolojia ya Kisasa katika kutekeleza Itifaki ya Cartagena (*Nagoya – Kuala Lumpur Supplementary Protocol on Liability and Redress on Cartagena Protocol on Biosafety*).

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):**

Maelezo ya Waziri wa Kilimo kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (*The Protocol for Protection of New Varieties of Plant [Plant Breeder's Rights] in the Southern African Development Community – SADC*).

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (*The Protocol for Protection of New Varieties of Plant [Plant Breeder's Rights] in the Southern African Development Community – SADC*).

**MHE. PASCAL Y. HAONGA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KILIMO:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (*The Protocol for Protection of New Varieties of Plant [Plant Breeder's Rights] in the Southern African Development Community – SADC*).

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Maelezo ya Waziri wa Viwanda na Biashara kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Marrakesh inayowezesha Upatikanaji wa Kazi zilizochapishwa kwa watu wasioona, Wenye Uoni Hafifu au Ulemavu Unaofanya Mtu Kushindwa Kusoma wa Mwaka 2013 (*The Marrakesh Treaty to Facilitate Access to Published Works for Persons who are Blind, Visually Impaired or otherwise Print Disabled (MVT) 2013*).

**MHE. OMARY A. BADWEL - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na mazingira kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Marrakesh inayowezesha Upatikanaji wa kazi zilizochapishwa kwa Watu Wasioona, Wenye Uoni Hafifu au Ulemavu unaofanya mtu Kushindwa Kusoma wa mwaka 2013 (*The*

*Marrakesh Treaty to Facilitate Access to Published works for Persons who are Blind, visually Impaired or Otherwise Print Disabled (MVT) 2013).*

**MHE. CECIL D. MWAMBE - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI WA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Kuridhia tifikasi ya Marakesh inayowezesha Upatikanaji wa Kazi zilichapishwa kwa Watu wasioona, Wenye Uoni hafifu au Ulemavu unaofanya Mtu kushindwa Kusoma wa mwaka 2013 *(The Marrakesh Treaty to Facilitate Access to Published Works for Persons who are Blind, visually Impaired or Otherwise Print Disabled (MVT) 2013).*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwamba umependeza na miwani baada ya kulipwa hela za korosho, umenunua miwani. *(Kicheko/Makofi)*

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:** Maswali.

### **MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaanza Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba.

Na. 84

**Kukaribisha Wawekezaji Mkoa wa Tabora**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** Aliuliza:-

Serikali ya Awamu ya Tano imekaribisha wawekezaji wa nje na ndani kuwekeza sehemu mbalimbali hapa nchini:-

Je, Serikali ipo tayari sasa kuelekeza wawekezaji hao kuwekeza katika Mkoa wa Tabora?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI)**

Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kukuza uwekezaji katika sekta mbalimbali na kujenga uchumi wa kati wenye kuongozwa na Sekta ya Viwanda ni suala linalotekelezwa katika mikoa yote ukiwemo Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuupongeza Mkoa wa Tabora na uongozi wake na Mikoa mingine kwa kuwa mfano mzuri katika kutekeleza mikakati ya kuvutia uwekezaji ikiwemo uandaaji wa makongamano ya uwekezaji kama lile lililofanyika mwaka 2013 Dar es Salaam na lililofanyika mwezi Novemba, 2018 katika mjini Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia makongamano hayo, tumeendelea kuhamasisha kila Halmashauri kuandaa mradi wa kimkakati ambao utakuwa dira kwa wawekezaji wengine. Aidha, katika kutekeleza agizo la Serikali la kutenga maeneo ya uwekezaji, Mkoa wa Tabora umetenga ekari 42,053.71 katika Halmashauri zake zote nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kama sehemu ya matokeo ya jitihada za Serikali, takwimu zilizopo katika Kituo chetu cha (TIC) zinaonesha kwamba tangu mwaka 1997, jumla ya miradi ya uwekezaji 55 imesajiliwa Mkoani Tabora katika Sekta za Kilimo, Viwanda, Ujenzi, Utalii Mawasiliano na Usafirishaji. Wilaya ya Tabora Mjini inaongoza kwa kusajili miradi 19, Urambo 13, Nzega miradi tisa, Igunga 11, Sikonge miradi miwili na Uyui mradi mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kati ya miradi hiyo, miradi 30 ni ya Watanzania, miradi tisa ni ya wageni na miradi

16 ni ya ubia. Hivyo, napenda kipekee kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inautambua Mkoa wa Tabora kama mojawapo ya maeneo ya kimkakati yenye fursa za uwekezaji katika sekta mbalimbali na tutaendelea kuwaelekeza wawekezaji kuja kuwekeza Tabora na katika Mikoa mingine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuwahamasisha Waheshimiwa Wabunge wote kushirikiana kwa karibu na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kituo chetu cha Uwekezaji (*TIC*), Mamlaka ya *EPZA* na Taasisi nyingine katika kuibua miradi inayokidhi vigezo (*bankable projects*) na pia kuboresha mazingira ya uwekezaji kwenye maeneo yao. Lengo la hili ni kufanikisha malengo ya Serikali ya kuvutia uwekezaji wenye tija nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Mikoa inashauriwa sasa kuanza kutenga katika bajeti zake fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya msingi kama vile maji, barabara, umeme na kadhalika. Lengo ni kuelekea kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji. Hatua hizi zitasaidia katika kuharakisha uendelezwaji wa maeneo maalum ya uwekezaji kwa kukamilisha hatua muhimu za awali na hivyo kuvutia wawekezaji na hata ushiriki wa sekta binafsi katika kuendeleza maeneo husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuzihamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya kazi kwa karibu na Taasisi za Serikali zinazotoa huduma za ushauri wa kuwezesha uwekezaji nchini ili kuweka mikakati ya pamoja ya kutambua vivutio na fursa za wawekezaji wa ndani na nje pamoja na kuwasilisha miradi ya kutafutiwa wawekezaji na kushirikiana na *TIC* katika kuandaa makongamano ya uwekezaji katika Mikoa husika.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Nchemba.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali mafupi ya nyongeza. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri na

Serikali ya Awamu ya Tano kwa kazi nzuri ambayo inafanywa kwa ajili ya mambo ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba kwa kuwa alipokuwepo Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, alikuwa ameandaa na alishawatayarisha wawekezaji kutoka nchini China ambao walikuwa tayari kuwekeza katika Kiwanda cha Tumbaku, kwa bahati mbaya walishia Dar es Salaam na kulikuwa na matatizo ya Uhamiaji: Je, Waziri yuko tayari sasa kuwafuatilia hawa wawekezaji wa Kichina ambao walikuwa tayari kabisa na maeneo yalitengwa ili waweze kuja kuwekeza kwenye zao la tumbaku?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili: kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa, amefanya jitihada kubwa na Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi kwa kuboresha maeneo katika mkoa mzima na Wilaya zote: Sasa je, Waziri yupo tayari sasa kuwaleta wataalamu rasmi ili kuweza kuainisha hayo maeneo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niseme tunashukuru kwa pongezi na nikuhakikishie tutaendelea kufanya kazi nawe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine pamoja na mikoa yetu katika kuhakikisha kwamba tunachochea na kuvutia uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kweli nimefahamishwa kwamba alikuwepo mwekezaji kutoka China ambaye alikuwa na nia ya kuwekeza Kiwanda cha Tumbaku Tabora. Mpaka sasa tumeendelea kumfuatilia, lakini bado hajaonyesha nia.

Napenda kusema kwamba tutaendelea kumhamasisha yeye zaidi na kutafuta wawekezaji wengine zaidi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Viwanda pamoja na Wizara ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili katika swali lake la pili kuhusiana kuleta wataalam, kwanza napenda kuwapongeza Mkoa wa Tabora kwa kutenga ardhi hiyo ya zaidi ya ekari 42, lakini kipekee napenda kusema tu kwamba ni takribani asilimia tano ndiyo tayari inakidhi vigezo. Imewekwa ardhi kubwa, mfano ukiangalia Kaliuwa, wana zaidi ya ekari 37,201, lakini ni asilimia tano tu ya Mkoa mzima wa Tabora katika maeneo ya uwekezaji yaliyotengwa, ndiyo ambayo tayari yalimewekewa miundombinu wezeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha, Wizara ya Ujenzi pamoja na Mkoa husika wa Tabora kwanza kuhakikisha kwamba maeneo hayo yanawekewa miundombinu wezeshi lakini pia kuhakikisha Halmashauri nazo zinaendelea kutenga fedha ili miundombinu iweze kutengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza sana kipekee Halmashauri ya Nzega ambao tayari kwenye bajeti yao wameweka zaidi ya shilingi milioni 40 kwa ajili ya suala zima ya upimaji. Kwa hiyo, natoa rai kwa Halmashauri nyingine saba zilizobakia na nyingine nchini, basi wajitahidi kutenga fedha katika bajeti yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala zima la kuleta wataalam, nimhakikishie kwamba tuko tayari kuleta wataalamu, lakini zaidi niwapongeze Halmashauri zile nane, kila moja imekuja na mradi wake wa kimkakati; wako ambao wana mradi wa machinjio, wako ambao wana mradi wa mashamba ya mifugo, kuweka kiwanda cha usindikaji na utengenezaji wa vyakula vya mifugo pamoja na sehemu nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza mikoa yote na Halmashauri zote ambazo tayari wameweza kubuni miradi ya mikakati. Nawaomba waendeleo kufuatilia, washirikiane na Wizara ya Kilimo pamoja na Benki yatu ya Kilimo na benki nyingine za kimaendeleo ili kuweza kupata mitaji ya kuweza kuwekeza. Nakushukuru.



**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu mazuri. Mheshimiwa Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Napenda tu kuuliza Serikali, tuna mradi mkubwa wa uchimbaji wa madini ya *niobium* katika milima ya *Panda Hill Songwe*; na kwa bahati nzuri ile miradi ita-*attract direct investment* ya karibu dola milioni 200 na wawekezaji wapo tayari; na katika ziara ya Mheshimiwa Rais alipofanya ziara kule Mbeya...

**MWENYEKITI:** Swali, swali!

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu: Je, ni lini Serikali itakamilisha mchakato wa kuwaruhusu hao wawekezaji waanze kuchimba haya madini ya *niobium* ili vile vile wajenge na kiwanda cha kuchakata hayo madini ambacho ni cha kwanza Afrika na cha nne duniani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kusema kwamba tunatambua kuhusiana na mradi huu wa *Niobium* ambao utafanyika katika milima ya *Panda Hill* na bahati nzuri nami nilipata bahati ya kukaa katika Wizara ya Madini, niliweza kuwaona wawekezaji hawa; na ni madini ambayo kwa kweli ni ya muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tulishaanza kuwashughulikia, pia tumekuwa na mashauriano na Wizara ya Madini pamoja na Wizara ya Viwanda kupitia *EPZ*. Tutakutana pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Madini pamoja na Wizara ya Viwanda ili kuweza kuona ni kwa namna gani tunakwamua mradi huu muhimu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Richard Philip Mbogo, Mbunge wa Nsimbo.

Na. 85

### **Kuangalia Upya Suala la Utoaji Ruzuku za Maendeleo**

**MHE. RICHARD P. MBOGO** Aliuliza:-

Mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290 yameleta nafuu sana kwa wakulima, lakini wakati huo huo Halmashauri za Wilaya zenye wakulima zenye wakulima wadogo zimeathirika kimapato na kusababisha kushindwa kutatua kero za wananchi kwa wakati:-

(a) Je, Serikali inaweza kuangalia upya suala la utoaji Ruzuku za maendeleo?

(b) Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo imeathirika kiwango kikubwa: Je, Serikali ipo tayari kuipatia ruzuku ili kutoa huduma za Elimu na Afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITAIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa ruhusa yako kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mbogo, naomba uniruhusu niwatakie heri vijana wetu, watoto wetu wa Darasa la Saba ambao leo na kesho wanafanya mitihani yao ya kumaliza Darasa la Saba na wanafunzi hao wapo takribani 947,221 wa kawaida na wale wenye mahitaji maalumu.

Nawaomba watu wote ambao wanahusika na zoezi hili la mitihani, wazingatie taratibu na kanuni na miongozo na kamwe wasijihusishe na udanganyifu kwa namna yoyote ile ili matokeo yawe yawe mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba sasa kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI nijibu swali la Mheshimiwa Richard Mbogo, Mbunge wa Nsimbo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali ilifanya mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290 kwa kuondoa kodi ambazo zilikuwa ni kero hasa kwa wakulima wadogo. Takwimu za jumla zinaonesha makusanyo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yamekuwa yakiongezeka kila mwaka. Mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri zilipanga kukusanya shilingi bilioni 665.4 na zikakusanya shilingi bilioni 544.8; mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri zilipanga kukusanya shilingi milioni 687.3 na zikakusanya kiasi cha shilingi bilioni 553.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani hizi zisomeke bilioni, siyo milioni. Mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri zilipanga kukusanya shilingi bilioni 723.7 na zimekusanya shilingi bilioni 661.36. Hivyo, kwa tathmini ya jumla, inaonesha kuwa uamuzi wa kuondoa kodi kero haujaathiri ukusanyaji wa mapato kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya afya katika kipindi cha Mwaka 2017/2018 na 2018/2019, Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya vya Kamoge na Katumba na shilingi milioni 220 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba. Vilevile katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 500 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Nsimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya elimu, mwaka wa Fedha 2018/2019, Serikali imeipelekea Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kiasi cha shilingi milioni 250 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya madarasa 20 ya shule za sekondari. Vilevile katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kupitia Programu ya *EP4R* Serikali imeipatia Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kiasi cha shilingi milioni 205.7 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa manne, ukamilishaji ma maboma ya

madarasa saba na ujenzi wa matundu ya vyoo 12 katika shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kupitia *EP4R*, Serikali imeipatia Halmashauri ya Nsimbo kiasi cha shilingi milioni 100.6 kwa ajili ya ujenzi wa maabara na matundu sita ya vyoo shule za sekondari. Aidha, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Serikali imeitengea Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kiasi cha shilingi milioni 421 kwa ajili ya elimu msingi bila malipo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi ili niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru Serikali kwa kuangalia na kutoa ruzuku kwenye Halmashauri zetu, hususan ambazo zina vipato vya chini. Swali la kwanza; kwa kiwango hiki ambacho Serikali imetoa, bado kulingana na uhitaji kwenye Halmshauri ya Wilaya ya Nsimbo ni kidogo. Je, wako tayari kutuongezea ili tuweze kukidhi ukamilishaji wa maboma na uhitajikwenye upande wa elimu pamoja na afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; katika upande wa mahitaji haya je, Naibu Waziri yupo tayari kurejea ziara yake atembelee Halmashauri ya Nsimbo kujionea na aweze kuona namna bora ya kuiwezesha Halmashauri ya Nsimbo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi. Jiandae Mheshimiwa Mwambe.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza naomba nipokee pongezi hizi za Mheshimiwa Mbunge, na hii pia imezingatia sana kwamba amekuwa akilisemea sana eneo lake hili ili kuweza kuondoa kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anauliza kama Serikali ipo tayari kuongeza fedha. Naomba nimhakikishie yeye na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Serikali nia yake kubwa ni kuhakikisha kwamba inaondoa changamoto ya miundombinu ya elimu na afya na kazi hiyo itakuwa inaendelea kufanyika kadri ya upatikanaji wa fedha kwa Serikali na wadau mbalimbali wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ananiuliza kama nitarejea ziara katika eneo hili. Ni kweli nimeshapanga ziara karibu mara mbili ikikaribia kwenda kule eneo la Katavi na Rukwa, ziara hii imekuwa ikiahirishwa. Naomba nimhakikishie ratiba nimeshaipanga, tukiahirisha Bunge hili Mheshimiwa Mbunge nitakuja Katavi na Rukwa na ntatembelea majimbo yote ya ukanda ule. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza:

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua hivi karibuni TAMISEMI wamekuwa wakitoa *rating* kwenye Halmashauri zetu kwa maana ya kuwapa namba kutokana na makusanyo na utekelezaji wa makusanyo wanayoyafanya. Kwa bahati mbaya sana Halmashauri nyingi ambazo walipanga mipango yao ikitegemea makusanyo ya mazao ya kilimo hawakuweza kufanikiwa kupata hizo pesa kwa wakati kwa sababu Serikali iliamua kuingilia mchakato fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kuuliza kwa Mheshimiwa Waziri, kwamba miradi mingi imesimama kwenye Halmashauri zetu, pesa za posho kwa ajili ya Madiwani hazilipwi kwa wakati na hasa miradi ya afya kwa sababu hivi karibuni – na niipongeze Serikali kwamba wametupatia pesa za 4PR kwa mfano Jimbo la Ndanda tumepata zaidi ya madarasa 13. Sasa ninataka kufahamu; ni lini Serikali mtapeleka pesa kwa ajili ya kukamilisha maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi kwenye Kata za

Ndanda, Lukuledi, Mihima na Mpanyani kwa ajili ya vituo vya afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, ni lini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Mheshimiwa Mwenyekiti, ameeleza maelezo mengi lakini kwa ufupi ni kwamba kama kuna mahitaji mahsusi unaandika TAMISEMI ili waweze kuyafanyia kazi. Lakini mpango wa Serikali ni kwamba hata Mwaka wa Fedha tunapoanza 2019/2020, fedha zimetengwa kwenda kumaliza maboma ambayo yapo ya msingi na sekondari katika Halmashauri zenu. Kwa hiyo tuvute subira lakini kama una jambo mahsusi tuandikie ili tuweze kuchukua hatua za haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme hii haisemwi amesema *4PR*, hii *EP4R* ndiyo lugha sahihi, maana yake ni kwamba *Education Payment For Results*. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu mazuri. Waheshimiwa tunaendelea, Wizara hiyohiyo swali la Mheshimiwa Dkt. Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi.

Na. 86

### Gharama za Elimu na Mafunzo

**MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA** aliuliza:-

Jimbo la Masasi lina Shule moja tu ya Sekondari ya Kidato cha Tano na Kidato cha Sita ambayo ni ya Kitaifa ingawa mahitaji ya Wanafunzi wanaofaulu kwenda Kidato cha Tano na Kidato cha Sita yameongezeka sana, Shule pekee ya Kidato cha Tano na Kidato cha Sita iliyopo Masasi ni Shule ya Sekondari ya Wasichana Masasi:-

(a) Je, ni lini Serikali itazipandisha hadhi Shule za Sekondari za Mwenge Mtapika na Anna Abdallah ili ziweze kupokea Wanafunzi wa Kidato cha 5 na 6;

(b) Jimbo la Masasi linahitaji vyumba 27 vya maabara ambapo hadi sasa vyumba Saba tu ndiyo vina vifaa vya maabara katika shule Nne; Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa vya maabara katika Shule zote za Sekondari?

(c) Ikama ya Walimu wa Sayansi katika shule za Sekondari Tisa zilizopo Jimbo la Masasi ni Walimu 84 japokuwa waliopo ni 24 tu; Je, Serikali inaweza kulifanya jambo hili kama dharura inayohitaji utatuzi wa haraka kwa kutuletea Walimu 60 wa Sayansi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Masasi Mjini, lenye sehemu (a), (b), na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Masasi Mji inafanya jitihada kuziwezesha shule tatu za Sekondari ambazo ni Sululu, Mtapika na Anna Abdallah ili ziweze kupandishwa hadhi na kuanza kutoa elimu ya Kidato cha Tano na cha Sita. Tayari shule hizo zilishakaguliwa na wadhhibiti ubora wa shule na kukutwa na mapungufu kadhaa, hasa ya miundombinu ya maji, umeme na mabweni na hivyo kukosa sifa. Halmashauri kwa kushirikiana na wadau inafanyia kazi mapungufu hayo ili shule hizo ziweze kupandishwa hadhi na kutoa elimu tarajiwa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018, jumla ya shule za sekondari 1,800 zilizokamilisha ujenzi wa maabara zilipelekewa vifaa vya maabara, na kati ya hizo shule sita ni za Halmashauri ya Mji wa Masasi. Vilevile

katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, jumla ya shule 1,258 zilizokamilisha ujenzi wa maabara zitapelekewa vifaa vya maabara na taratibu za manunuzi zinaendelea ambapo shule tatu kati ya shule zitakazopatiwa vifaa hivyo zipo katika Halmashauri ya Mji wa Masasi.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 hadi 2018/2019, Serikali imeajiri jumla ya watumishi 7,515 katika shule za sekondari nchini. Kati yao Walimu ni 7,218 na Fundi Sanifu Maabara ni 297. Kati ya walimu walioajiriwa walimu wenye mahitaji maalum ni 29, walimu wenye elimu maalum ni 50, walimu wa masomo ya sayansi na hisabati ni 7,089 na walimu wa lugha (*Literature in English*) ni 100. Ambapo walimu 15 wa sayansi walipangwa katika Halmashauri ya Mji wa Masasi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape, swali namba 86.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana Naibu Waziri wa Elimu alitembelea Jimboni Mtama na katika ziara yake alikwenda kwenye Shule ya Sekondari Mahiwa na akaahidi kutupatia fedha ya kuikarabati shule ile kwa sababu ilifanya vizuri katika mtihani wa Kidato cha Sita, pamoja na Shule ya Sekondari Nyangao ambayo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Chuachua nimekuona, samahani. Endelea tu Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** ...ambayo mwaka...

**MWENYEKITI:** Subiri Mheshimiwa Nape, samahani. Mheshimiwa Dkt. Chuachua.

**MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza:



Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa kuwa sasa kuna upungufu mkubwa wa walimu wa masomo ya sayansi katika Halmashauri ya Masasi na walimu 46 wanahitajika ili kukidhi Ikama ya walimu wa masomo ya sayansi;

Je, ni lini Serikali italeta Walimu hao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kwamba kwa kuwa suala la kukosekana kwa walimu wa sayansi ni suala la Kitaifa, na kwa kuwa wanafunzi wengi wanaomaliza kidato cha nne na kidato cha sita hawachagui kwenda kujiunga na masomo ya ualimu wa masomo ya sayansi, hivi Serikali haioni kunatakiwa kuwe na jitihada za maksudi za kuchochea watoto hawa ili waweze kujiunga na masomo ya ualimu wa sayansi hususan kwa kuondoa ama kupunguza ada kwa masomo ya *Diplomaya* Ualimu wa Sayansi na *Degree* ya Ualimu wa Sayansi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufuatilia suala la elimu hasa katika masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anataka kujua ni lini walimu wa sayansi watapelekwa katika maeneo haya. Ni kweli kwamba kuna upungufu wa walimu wa sayansi na hisabati katika shule zetu za sekondari lakini tumepata kibali mwaka wa fedha uliopita tukaajiri walimu 4,500 na sasa tunasubiria kibali kingine takribani walimu 15,000. Tukipatakibali hicho tutaajiri, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge maeneo yote ambayo yana upungufu tutaanza nayo, pale palipo na upungufu mkubwa tunaanza na kuendelea katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ni kuwa na walimu wa kutosha katika masomo ya sayansi ili kuweza

kuboresha elimu hii ya sayansi hasa kwenye dhana nzimainayohusiana na Serikali ya Awamu ya Tano ya sera ya maendeleo ya viwanda na uchumi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anazungumzia kama kuna uwezekano wa kupunguza ada katika masomo na hasa katika *Diplomai*li wanafunzi wengi na vijana wengi wajiunge katika masomo ya sayansi na hasa Ualimu ili waweze kupunguza changamoto hii. Kwanza gharama inayotumika sasa siyo kubwa ni gharama ya kawaida kabisa na Serikali imejitahidi sana kupunguza michango mingi ambayo ilikuwa inafanyika. Sasa hivi tumeshapeleka vijana wengi katika Vyuo hivi, wataendelea kusoma na ada ni ya kawaida. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nape.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mtama lina shule za sekondari mbili ambazo zinapokea vijana wa Kidato cha Tano na Kidato cha Sita. Shule ya Sekondari Nyangao na Shule ya Sekondari Mahiwa. Mwaka jana Naibu Waziri wa Elimu alipotembelea Jimboni Mtama alipoenda kuiona Shule ya Sekondari Mahiwa alikuta majengo yake yamechoka na yamekuwa ya muda mrefu na akaahidi kwamba Serikali itatoa fedha kusaidia ukarabati wa majengo hayo.

Je, Serikali iko tayari kutekeleza ahadi yake kwa wananchi wa Jimbo la Mtama?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mhusika, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba nilitembelea Jimbo la Mheshimiwa Nape na ni kweli kwamba alinisihi nimsaidie shule yake iweze kupata miundombinu ili iweze kuwa bora na hatimaye kuwa shule ya Kidato cha Tano na Kidato cha Sita. Naomba niendeleo kumuahidi Mheshimiwa Mbunge

kwamba Serikali imepanga kupeleka fedha katika Awamu ya Nane ya Mpango wa EP4R, kwa hiyo, ahadi yetu iko palepale na itatekelezwa. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe.

Na. 87

### Hitaji la Walimu wa Sayansi – Katavi

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Walimu wa Sayansi katika Mkoa wa Katavi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2016/2017 hadi 2018/2019, Serikali imeajiri jumla ya watumishi 7,515 katika shule za sekondari nchini. Kati yao, Walimu 7,218 na Fundi Sanifu Maabara 297. Kati ya walimu walioajiriwa walimu wenye mahitaji maalum walikuwa 29, walimu wenye elimu maalum ni 50 na walimu wa masomo ya sayansi na hisabati ni 7,089 na walimu wa lugha (*Literature in English*) walikuwa 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2016/2017 hadi 2018/2019 Serikali ilipanga jumla ya Watumishi 121 katika shule za sekondari Mkoani Katavi. Kati yao Walimu wa masomo ya Sayansi na Hisabati walikuwa 115 na Fundi Sanifu Maabara walikuwa Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuajiri watumishi wa kada mbalimbali ikiwemo walimu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mahitaji ya walimu wa sayansi ni makubwa sana na ukizingatia wananchi ambao tunaishi pembezoni unakuta shule moja kama Rungwa Sekondari pale Mpanda ina watoto 1,150, walimu wa sayansi kuanzia *Form One* mpaka *Form Six* walimu wako wanne tu. Na ukiangalia sehemu nyingine kama Usevia shule *Form One* mpaka *Form Six* walimu wawili.

Je, Serikali itatuletea lini Mkoa wa Katavi walimu kwa sababu tunahitaji sana walimu kutokana na uhitaji wa wanafunzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa kuwa Serikali ilifanya kazi kubwa ya kuhamasisha kujenga maabara katika shule zote za Kata nchini, na wananchi walihamasika sana wakajenga maabara na maabara zile zimekamilika lakini walimu wa sayansi hakuna kabisa.

Je, lini Serikali itaweka mikakati maalum kama ilivyofanya kuhamasisha kujenga maabara ili tuweze kupata sasa walimu wa sayansi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza ninampongezasana Mheshimiwa Mbunge Anna Lupembe kwa kuendelea kuwasemea watu wake wa Mkoa wa Katavi ili waweze kupata elimu bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tuna changamoto ya upungufu wa walimu wa sayansi na hasa

katika masomo ya sayansi na hisabati. Vilevile Serikali imefanya kazi kubwa sana ya kuongeza juhudi ya kutafuta fedha ili tuweze kuajiri walimu hawa wakasaidie kuondoa changamoto ya walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwataarifa tu mwezi Mei mwaka huu Serikali ilipeleka fedha za *EP4R* motisha ili moja, zikamalizie maboma ya shule za msingi na sekondari, pili ilikuwa ni ku-*balance* ikama katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaelekeze Waheshimiwa Wakurugenzi katika Halmashauri zetu na Maafisa Elimu wa Mikoa na Wilaya, zile fedha za Serikali ilikuwa ni kuangalia kama kuna shule moja ina upungufu, shule nyingine ina walimu wa ziada, ilikuwa ni kuwahamisha kutoka eneo moja kwenda lingine ili kuweza ku-*balance* ikama na kupunguza changamoto ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kama nilivyosema katika maswali yaliyopita leo asubuhi, tumeshaomba kibali cha kuajiri walimu hawa, zaidi ya 15,000. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na maeneo mengine ya pembezoni, tutakapopata kibali cha kuajiri walimu wa sayansi na hisabati, maeneo ya pembezoni yatakuwa kipaumbele, tutaanza na maeneo ambayo yana upungufu mkubwa wa walimu kwenda pale ambapo pana upungufu ambao siyo mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anaulizia maboma ya maabara zetu. Ni kweli, tumekubaliana tunagawana kazi, Waheshimiwa Wabunge, Serikali na wadau mbalimbali wa elimu na maendeleo. Kazi ya kumalizia maboma haya ya maabara ni ya kwetu sote kama nilivyotaja. Serikali tumejipanga, hapa tulipo tupo kwenye manunuzi, wakati wowote kuanzia sasa taratibu za manunuzi zitakamilika tutapeleka vifaa katika maabara zetu. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine tuendelee kuchangia kwa namna mbalimbali tumalizie maboma yetu, vifaa tutapeleka, wataalam tutapeleka na

hii changamoto hatimaye itaisha ili watoto wetu waweze kusoma katika mazingira ambayo ni rafiki. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tuna maazimio mengi leo. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa David Ernest Silinde.

Na. 88

### **Ujenzi wa Barabara ya Mlowo – Kibaoni**

**MHE. PASCAL Y. HAONGA (K.n.y. MHE. DAVID E. SILINDE)** Aliuliza:-

Je, ni lini barabara ya Mlowo – Kamsamba – Kiliyamatundu – Kibaoni itajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mlowo – Kamsamba – Kiliyamatundu – Kibaoni yenye urefu wa kilometa 369 ni barabara ya Mkoa na inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) Mikoa ya Songwe, Rukwa na Katavi. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (*TANROADS*) imekamilisha ujenzi wa Daraja la Momba lenye urefu wa mita 84 na barabara unganishi zenye urefu wa kilometa 1.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea kwa barabara kuanzia Kamsamba hadi Mlowo, kilometa 130.14 na barabara ya mchepuo kwa kuingia Makao Makuu ya Wilaya ya Momba, kilometa 15, kwa gharama ya shilingi milioni 765.46. Kazi hii imefikia asilimia 75.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 180 kwa ajili ya kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara na kuijenga kwa kiwango cha lami sehemu ya barabara hii kuanzia Kiliyamatundu hadi Kasansa (sehemu ya Kiliyamatundu – Muze (km 142) na Ntendo – Muze (km 37.04), taratibu za kumpata Mshauri Elekezi wa kufanya kazi hiyo zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu sehemu ya barabara kutoka Kasansa hadi Kibaoni (km 60), sehemu ya kuanzia Kibaoni hadi Majimoto (km 34) ipo kwenye hatua za manunuzi ya kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 162). Aidha, sehemu iliyobaki kuanzia Muze – Mamba – Majimoto (km 55) Serikali inatafuta fedha ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii kwa ajili ya usafiri wa wananchi na usafirishaji wa mazao ya chakula na biashara yanayozalishwa na wananchi wa maeneo ya Kata za Igamba, Hulungu, Itaka, Nambinzo hadi Kamsamba pamoja na maeneo ya Kiliyamatundu, Muze, Kasansa, Majimoto hadi Kibaoni, Serikali inaendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kuifanyia matengenezo mbalimbali ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka na mara tu usanifu wa kina utakapokamilika, ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara hii utafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, wakati wa kampeni Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli aliahidi kwamba kabla ya kufika mwaka 2020, barabara hiyo ya kutoka Mlowo kwenda Kamsamba hadi Kibaoni itakuwa imekamilika. Ukiangalia kuanzia sasa hadi mwaka 2020 bado miezi michache tu. Je,

ni lini sasa ahadi hii ya Serikali itatekezwa kwa vitendo badala ya maneno?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa katika majibu ya Serikali kwamba kukamilisha usanifu wa kina hawajataja kwamba ni lini usanifu wa kina utakamilishwa. Je, Serikali kutotaja muda wa kukamilisha usanifu wa kina haioni huku ni kutowatendea haki wananchi wa Mikoa ya Songwe, Katavi, pamoja na Rukwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Haonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, umetaja ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni, lakini ujenzi wa barabara ni mchakato, lazima ufanye upembuzi yakinifu, usanifu wa kina, baadaye uingie mikataba uanze kujenga. Hauwezi ukafanya kabla ya kukamilisha hizo hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vipande vya barabara ambavyo unavizungumzia tayari kuna kimoja mwezi huu wa tisa cha kutoka Mlowo kwenda mpaka pale tulipokamilisha daraja, mwezi wa tisa usanifu wa kina utakamilika baada ya hapo mambo mengine yanaanza. Upembuzi yakinifu umeanzia kule Muze unakuja kuunga Kamsamba, na tuna matarajio ya kuendelea huko na pia tumeshaanzia Inyonga kuja mpaka Maji ya Moto. Kwa hiyo, utaratibu unaendelea ahadi ya Mheshimiwa Rais inatekelezwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge usiwe na wasiwasi na wananchi jirani zangu wa kule wawe na uhakika kwamba barabara ile itajengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

**MWENYIKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba kuuliza swali langu la nyongeza,



barabara ya kutoka Senga Ibisabageni mpaka Sima ni barabara inayotuunganisha Mkoa wa Geita na Mkoa wa Mwanza na Serikali ilitupa fedha upande wa Geita na upande wa Mwanza. Upande wa Geita tulishalima eneo letu tukamaliza lakini upande wa Mwanza umebakiza kama kilomita tatu na leo ni mara ya tatu namuuliza Mheshimiwa Waziri.

Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari kufuatana na mimi kwenda kuona zile kilomita tatu tu ambazo upande wa Mwanza wameshindwa kumaliza ili watu waanze kupitisha magari yao pale? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari kufuatana naye. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mabula jiandae Mheshimiwa Komu.

**MHE. STANLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba niulize swali la nyongeza, kwa kuwa barabara ya Kenyatta itokaya Mwanza Mjini kwenda Usagala kuelekea Shinyanga ni barabara ambayo inahudumia watu wengi na kwa sasa inaendelea kuwa finyu sana. Ni lini Serikali kupitia mipango yake ya uboreshaji miundombinu itaitolea fedha barabara hii walau iwe ya njia tatu mpaka nne ili kuweza kukidhi mahitaji makubwa ya watu wa Mwanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanua barabara, kuongeza reli, hatuendi hivi hivi lakini mpaka *traffic* iweze kufikia kwamba sasa yanapita magari 20,000 au 40,000 kwa siku ndiyo tunaipanua ili kuiongezea uwezo. Kwa hiyo, itakapofikia itafanyika.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Komu.

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kama ilivyo katika Wilaya ya Momba, kule Moshi Vijijini katika Kata ya Uru Shimbwe Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli wakati anagombea alikuja pale akahutubia na akaahidi kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Mamboleo mpaka Shimbwe. Kwa kweli ile barabara sasa hivi iko katika hali mbaya sana, sasa naomba kujua toka kwa Serikali ni lini ahadi hii ya Mheshimiwa Rais itatimizwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Komu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni kuunganisha mikoa kwa barabara za lami, lakini na mipaka ya majirani zetu kuunganisha kwa lami halafu baadaye ndiyo tunaendelea na barabara nyingine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Barabara ya kutoka Iringa Mjini kuelekea Ruaha *National Park* ambayo ni Jimbo la Kalenga imekuwa ni changamoto na ni ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na Rais wa Awamu ya Tano. Ni lini sasa barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile itajengwa pamoja na Uwanja wa Ndege wa Nduli na itajengwa kupitia fedha za Benki ya Dunia, taratibu za kupata hizo fedha zinaendelea itakapokamilika mradi utaanza.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Aida Joseph Khenani.

Na. 89

### **Matamko Juu ya Wanafunzi Wanaopata Ujauzito**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Kumekuwa na matamko na makatazo mbalimbali juu ya wanafunzi wanaopata ujauzito wakiwa shuleni:-

Je, matamko na makatazo hayo yamesaidia kwa kiasi gani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijajibu swali naomba kutumia nafasi hii kuwatakiya vijana wetu 947,221 wanaofanya mitihani yao ya darasa la saba, naomba niwatakie kila la kheri na Mungu awaongoze katika mitihani yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, matamko na makatazo kuhusu wanafunzi wanaopata ujauzito yanatokana na Kanuni za Elimu za Mwaka 2002, Kanuni Na. 4 ya Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978, Sura Na. 353 inayobainisha makosa ya wanafunzi shuleni. Aidha, yanazingatia marekebisho ya Sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 yaliyofanyika mwaka 2016. Katika marekebisho hayo, mtu yeyote atakayepatikana na hatia ya kumpa mimba mwanafunzi wa shule ya msingi au sekondari atahukumiwa kifungo cha miaka 30 jela. Sheria hii

pia inatoa adhabu kwa mtu yeyote anayesaidia mhalifu aliyempa mwanafunzi mimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria na makatazo hayo yamesaidia jamii kufahamu umuhimu wa kulinda hadhi na usalama wa mtoto wa kike. Pia, imesaidia kujua adhabu kwa mtu yeyote anayempa mwanafunzi mimba ambapo kesi zimefunguliwa na baadhi ya wahusika wamehukumiwa kifungo kwa kosa hilo. Aidha, elimu, matamko na sheria vimesaidia kupunguza mimba za wanafunzi kwenye maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeweka mikakati ya kupunguza changamoto kwa watoto wa kike ikiwa ni pamoja na kujenga mabweni na hosteli katika maeneo ambayo wanafunzi wanalazimika kutembea umbali mrefu. Aidha, Serikali pia imeweka mpango wa kusaidia wasichana wanaoacha shule kwa sababu mbalimbali ili waweze kuendelea na masomo. Mpango huo ni kutoa elimu kupitia Vyuo vya Elimu Nje ya Mfumo Rasmi vinavyoratibiwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Waziri pamoja na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC).

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito kwa wazazi na jamii kwa ujumla kuendelea kutoa ushirikiano wa kuwalinda watoto wa kike na kuhakikisha kuwa taarifa zinatolewa kwa mamlaka husika ili kuhakikisha kuwa mtu yeyote anayemsababishia mtoto wa kike kukosa elimu anakumbana na mkono wa sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khenan.

**MHE. AIDA J.KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kutokana na majibu ya Serikali, Serikali yenyewe inakiri kwamba kuna changamoto mbalimbali zinazopelekea mtoto wa kike kupata ujauzito. Lakini inasema ina mpango wa mtoto huyu wa kike aliyepata ujauzito kusoma elimu ya watu wazima ambayo ni nje ya mfumo rasmi. Kuna wanawake ambao wana familia zao wanasoma *degree*,

wanapata *Master's* na *Ph.d* ambao ni mfumo rasmi. Serikali haioni kwa kufanya hivyo ambao tunawaita ni watoto wakasome elimu ya watu wazima ni kuwaongezea adhabu nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Serikali pia imekiri kwamba umbali mrefu nao unachangia watoto wa kike kupata ujauzito. Kwa kuwa Mkoa wa Rukwa nao umekuwa kinara kwa watoto wa kike kupata ujauzito, Mkuu wetu wa Mkoa amekuja na oparesheni ambayo ina kauli mbiu ambayo inasema, Niacha Nisome. Je, Serikali iko tayari kumsaidia fedha kwa ajili ya kujenga hosteli?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hilo la pili, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari Serikali inasaidiana na wananchi kwenye halmashauri zao kujenga hosteli na mabweni kwa ajili ya kuondoa changamoto ya watoto wa kike ambao wanatembea umbali kwenda shuleni. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba tuko pamoja na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kuhakikisha kwamba azma yake hiyo inafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na lile swali lake la kwanza, kwamba kwa maoni yake siyo haki kuwanyima watoto ambao wamepata ujauzito kuendelea na masomo katika shule za kawaida. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba lengo la Serikali ni zuri kwa sababu tunajaribu kumlinda hata mtoto yule anayezaliwa kwa sababu watoto wale ambao wanapata mimba wanakuwa baadaye wanawabeba wenzao. Ukiwapeleka katika shule za kawaida hawatapa mazingira mazuri ya kuweza kuwalea. Kwa hiyo, tunamjali mtoto yule aliyezaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumeweza kujifunza vilevile kwamba hata watoto hao ambao wamepata ujauzito, mara nyingi wakienda kwenye shule za kawaida zile

ambazo wametoka wanakuwa wananyanyapaliwa, kwa hiyo tunawawekea mazingira mazuri ambayo yatawasaidia kusoma kwa uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, wanapoenda kusoma kwenye Vituo vya Elimu ya Watu Wazima, inawasaidia kusoma katika utaratibu ambao...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwahakikishie kwamba tutaendelea kuwasaidia na kwa kweli vituo hivyo ambavyo viko 500 nchi nzima vya watu wazima vimewasaidia watoto wengi wa kike kuendelea na masomo katika ngazi zinazofuata.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani Mbunge wa Uzini.

Na. 90

**Udhibiti wa Fangi Kwenye Mazao ya Korosho**

**MHE. SALUM MWINYI REHANI** Aliuliza:-

Dawa ya Sulphur ndiyo dawa ya udhibiti wa fungue (fangi) kwenye mazao ya korosho na mazao mengine, na Serikali imeunda mfumo wa kuagiza dawa hii ya kupuliza kwa njia bubu *procurement*; na mwaka jana baadhi ya wakulima waliathirika kwa kuchelewa na kupata dawa feki.

(a) Je, ni lini Serikali itakuwa tayari kuleta dawa mbadala ambazo ni rahisi zaidi?

(b) Je, ni lini Serikali itakaa na Vyama vya Msingi ili kupanga ratiba ya kuagiza na kuleta dawa na kupiga na pia kuzuia dawa za msimu uliopita?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)**

Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, Mbunge wa Uzini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haijaanzisha mfumo bubu wa ununuzi wa Salfa. Zao la korosho huathiriwa na magonjwa aina mbalimbali yakiwemo yale yanayosabishwa na *fungue*. Miongoni mwa magonjwa tishio kwa zao hili ni Ubwiriunga, Blaiti, Chule na Mnyauko fusari. Hata hivyo, magonjwa hayo yamekwisha kupatiwa tiba isipokuwa mnyauko fusari. Serikali inaendelea na tafiti kupitia taasisi zake ili kupata kinga na tiba stahiki za magonjwa na wadudu wanaoshambulia zao la korosho hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, salfa ni miongoni mwa viuatilifu vinavyotumika kwa kinga na tiba ya ugonjwa wa Ubwiriunga. Serikali inakusudia kuandaa mfumo wa pamoja wa ununuzi wa viuatilifu kwa ajili ya matumizi ya msimu wa 2020/2021 ambapo viuatilifu vingine kwa ugonjwa huo ambavyo ni *triadimenol*, *hexaconazole*, *tebuconazole* na vinginevyo. Hata hivyo, Serikali itaendelea kuhimiza matumizi ya salfa kwa kuwa kiuatilifu hiki hakiitaji ujuzi mwingi wakati wa kukitumia shambani kwa kuwa kimezoeleka na vilevile hakiingii ndani ya mmea na hivyo kufanya korosho inayozalishwa kuwa na sifa ya kilimo hai (*Organic Cashew Nut*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Bodi ya Korosho itendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na Vyama vya Msingi vya Ushirika katika kutathmini mahitaji ya viuatilifu na ratiba ya uagizaji wa viuatilifu hivyo. Aidha, Serikali kupitia *TPRI* itaongeza uhibititi katika ukaguzi wa viuatilifu nchini ili kuviondoa sokoni viuatilifu visivyo na sifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Rehani.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nauliza maswali mawili ya nyongeza; Je, Serikali ina mkakati gani wa ndani ambao utahakikisha kwamba viuatilifu vyote vinaagizwa kwa mfumo wa *bulk procurement* ambao sasa hivi haujaanza. Mfumo huu ndiyo ule ambao unasaidia kulifanya zao la korosho ku-*stand* kwenye uzalishaji mkubwa zaidi kama ulivyofanyika mwaka juzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa udhibiti wa wafanyabiashara wasio waaminifu pamoja na kutumia watafiti ambao wengine wanashirikiana katika kutengeneza baadhi ya viuatilifu ambavyo wanavichanganya na dawa kama za salfa, dawa kama za *pecoxystrobin* na *proquinazid* ambazo zinachangia sana kuweza kusaidia kuongeza uwezo wa kemikali na kuua wadudu lakini vinaharibu mazingira katika maeneo yetu. Je, mkakati gani upo ambao utaweza kuwadhibiti kupitia *TPRA* hawa wafanya biashara ambao si waaminifu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anataka kujua mkakati wa Serikali kwa ajili ya kuanzisha mfumo wa uagizaji wa viuatilifu kwa pamoja (*bulk procurement*) ukoje. Nataka nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge, Serikali sasa hivi tuko kwenye hatua za mwisho wa mchakato wa kumalizia ili kwa ajili ya uagizaji wa viuatilifu kwa pamoja. Nataka nimhakikishie msimu ujao wa kilimo cha korosho wa mwaka 2020/2021 kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, tutaagiza viuatilifu kwa pamoja kwa kutumia Mfumo wa *Bulk Procurement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anataka kujua mkakati wa Serikali tuliokuwa nao katika kudhibiti uingizaji nchini wa viuatilifu feki. Tulishawaelekeza Taasisi yetu ya *TPRA* na wako *field* wanafanya ukaguzi wa mara kwa mara na ukaguzi wa kushtukiza katika maduka yote ili kubaini viuatilifu ambavyo havina sifa na kuvitoa sokoni na kuchukulia hatua kwa wale walioviingiza. Pia, vyombo vyetu vya ulinzi na usalama pamoja na *TRA* wanadhhibiti mipaka yetu kwa



ajili ya kuingiza viuatilifu hivi feki ili kuwalinda wakulima hawa wapate viuatilifu vinavyostahili.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea muda wetu mchache, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya wizara hiyo hiyo.

Na. 91

### **Tiba kwa Magonjwa Sugu ya Mazao**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** Aliuliza:-

Kutokana na kuwepo kwa magonjwa sugu yanayoathiri mazao ya ndizi, mihogo, minazi na matunda kama michungwa, miembe na kadhalika kumesababisha wakulima kutozalisha kwa kiwango kinachostahili lakini pia mazao haya kukosa masoko ya uhakika nje ya nchi.

Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha magonjwa haya yanapatiwa suluhisho la haraka ili kilimo kiwe na tija na kupata masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE)**

Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sayaka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli magonjwa sugu ya mazao yanaathiri uzalishaji, tija na ubora wa mazao hivyo kusababisha hasara kwa mkulima. Katika kushughulikia changamoto hiyo, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kukabiliana na usugu wa visumbufu hivyo. Mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha tafiti, kuzalisha na kusambaza kwa wakulima mbegu zenye ukinzani dhidi ya magonjwa mbalimbali. Kwa mfano, mbegu za muhogo aina ya Kiroba,

Kizimbani, Kipusa, Chereko, Mkuranga 1 na Mkombozi zinahimili ugonjwa wa Batobato na mchirizi kahawia, miche bora ya migomba aina ya FHIA 17, FHI 23, Nshakara na Nyoya zinahimili ugonjwa wa unyanjano wa zao la migomba. Aidha, mikakati mingine ni kuimarisha huduma za ukaguzi wa mimea na bidhaa za mazao yanayoingizwa nchini ili kuzuia uingizwaji wa visumbufu vamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utafiti wa ndani, kikanda na kimataifa ili kupata mbegu kinzani na viuatilifu katika mazao mbalimbali ikiwemo migomba (*Resistant and Tolerant Cultivars*). Utafiti wa ugonjwa mnyauko bakteria katika zao la migomba unaendelea katika taasisi za utafiti wa kilimo za Maruku, Uyole, Tengeru pamoja na nchi ya Uganda. Aidha, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (*TARI*) kwa kushirikiana na Shirika la *Belgium Technical Cooperation (BTC)* zimetafiti kuzalisha na kusambaza miche bora ya migomba 6,000,000 katika wilaya za Mkoa wa Kagera na Wilaya za Kasulu na Kankonko Mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima na maafisa ugani wanaendelea kupatiwa mafunzo ya mbinu za udhibiti wa vusumbufu vya mimea kwenye mazao hayo ili kuongeza uzalishaji na tija. Serikali inawahimiza wakulima kutumia mbegu zenye ukinzani dhidi ya magonjwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na kuwepo kwa wataalam watafiti wenye uwezo na weledi, taasisi nyingi za utafiti zinakabiliwa na changamoto kubwa za miundombinu mibovu lakini pia ukosefu wa rasilimali fedha pamoja na madawa kwa ajili ya kufanya utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni kwamba kushindwa kutenga asilimia moja ya bajeti kwenda kwenye utafiti inasababisha Serikali kushindwa kuhudumia taasisi hizi

na hivyo kusababisha magonjwa kuendelea kutesa mimea na wananchi kuendelea kuathirika kwa kulima?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Serikali ina mkakati wa kuweza kusambaza mbegu bora na miche bora ambazo zinahimili magonjwa wakati huo huo zinapandwa maeneo ambapo pambeni yake kuna mazao yaliyoathirika, kuna mimea iliyoathirika. Kwanini Serikali isije na mkakati sasa na *program* maalum ya kuondoa mimea iliyoathirika yote na kuwezesha wakulima kupata mbegu nzuri na miche bora ili kuhakikisha kwamba miche mipya inayopandwa haiathiriki na hivyo kusaidia wakulima kuinua uchumi wa familia na uchumi wa Taifa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. HUSSEIN M. BASHE):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sakaya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ni maamuzi ya Kikanda na Kimataifa kwamba tutenge asilimia moja ya pato letu kwa ajili ya *research* na *development* lakini vilevile ni ukweli usiopingika kwamba bado mapato ya nchi na vipaumbele na matatizo yanayotukabili kama nchi ni mengi. Kwa hiyo, uwekezaji katika *research* pamoja na kuwa ni muhimu lakini hatujafikia lengo ambalo tumejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tulichoamua kama Wizara ya Kilimo ni kwamba *all resource* zinazokuja kutoka kwa *development partners* na tarehe 19, Wizara ya Kilimo tutakuwa na kikao na *development partners* wanaowezeza katika sekta ya kilimo, fedha zote tutaelekeza katika *research* na *seed multiplication program* ili uwekezaji katika vyo na taasisi za utafiti uweze kupata *resource* inayotosheleza. Tuondoe uwekezaji unaofanywa katika *capacity building* ambao unatolewa na taasisi za Kimataifa zinazowezeza katika sekta ya kilimo. Kwa hiyo, *focus* yetu katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka huu ni uwekezaji mkubwa wa fedha zote za *donors* na *development partners* zinazokuja

katika sekta ya kilimo pamoja na uwekezaji wetu wa ndani kuwekezwa katika maeneo ya *research* na uzalishaji wa mbegu bora ambazo zitakabiliana na matatizo yanayotukabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kuna changamoto pale ambapo ardhi imekumbwa na tatizo halafu tunapeleka mbegu mpya. Kama Wizara tumeamua kufanya *mapping* na tumeanza programu katika Mkoa wa Dodoma, Wilaya ya Kondoa ambao wameathiriwa na sumukuvu. Maeneo yote haya sasa hivi tunaanza utaratibu wa kwenda kwa wananchi katika kata zilizoathirika kuondoa mbegu walizohifadhi kwa ajili ya msimu ujao na kuanza utaratibu wa kuwapatia mbegu mpya na ku-*treat* ile ardhi ili tatizo hilo lisiweze kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaratibu wa kufanya *mapping* na kuelewa wapi kumeathirika na nini unaendelea ndani ya Wizara. Tunaamini kwa mpango mpya wa miaka mitatu wa Wizara ya Kilimo wa kuwekeza katika *research* na *development* katika taasisi hizi, tutaondoka katika matatizo haya yanayotukabili sasa hivi kama nchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Martin Mtonga Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini.

Na. 92

### **Hitaji la Mazao ya Biashara-Mbinga**

**MHE. MARTIN M. MSUHA** aliuliza:-

Tangu uhuru Wilaya ya Mbinga imekuwa ikitegemea zao moja la biashara ambalo ni kahawa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka zao lingine la biashara Wilayani humo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)**

alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martin Mtonda Msuha, Mbunge wa Mbinga Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya utafiti wa afya na tabaka la udongo katika kanda saba za kilimo zenye kuwezesha uzalishaji wa mazao mbalimbali kulingana na ikolojia ya kanda husika. Kanda hizo za kikolojia ni pamoja na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inayohusisha Wilaya ya Mbinga na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na utafiti huo, Serikali imeandaa mwongozo wa uzalishaji wa mazao kwa kuzingatia ikolojia ambapo Mkoa wa Ruvuma una fursa kubwa ya kuzalisha mazao mengine ya biashara tofauti na kahawa ikiwemo mazao ya korosho, muhogo, alizeti, ufuta na matunda yanayostawi katika ukanda wa baridi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima katika Halmashauri ya Mbinga wamehamasishwa na wameanza uzalishaji wa kibiashara wa mazao ya korosho, alizeti, ufuta, soya, parachichi, miwa, tumbaku pamoja na mazao mapya kama macadamia. Aidha, Serikali inaendelea kusimamia uendelezaji wa mazao kwa kuhamasisha matumizi ya teknolojia bora katika mnyororo wa thamani, kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika kilimo pamoja na kuimarisha ushirika na mifumo ya masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu wa mwaka 2016/2017, Serikali kupitia Bodi ya Korosho ilitoa mafunzo ya uzalishaji wa miche bora ya korosho kwa vikundi sita vya wakulima vya Jembe Halimtupi Mtu *group*, Chapakazi *Group*, *Twiga Group*, *Juhudi Group*, *Kiboko Group* na *Koroshomali Group* ambapo kwa pamoja vilizalisha jumla ya miche bora 111,336 na kuisambaza kwa wakulima kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa zao hilo. Aidha, msimu wa mwaka 2018/2019, jumla ya hekta 29,374.6 zilipandwa mazao ya biashara katika

Wilaya ya Mbinga ambapo kati ya hizo, hekta 265 zilitumika kuzalisha zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika msimu wa 2018/2019, eneo la hekta 806 zilitumika kuzalisha zao la soya, hekta 317 zao la alizeti, hekta 240 ufuta, hekta 32 miwa na hekta 89.5 ni parachichi. Uzalishaji wa zao la soya umeongezeka kutoka tani 42.6 msimu wa mwaka 2017/2018 hadi kufikia tani 403 msimu wa mwaka 2018/2019. Aidha, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga inayo ikolojia inayoruhusu uzalishaji wa mazao mengi ya biashara, Serikali itaendelea kuimarisha huduma za ugani ili mazao hayo yazalishwe kwa wingi na tija.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msuha.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Niipongeze Serikali kwa majibu mazuri katika swali hilo. Pia kwa dhati kabisa nichukue fursa hii kuishukuru Serikali kwa kupeleka Mnada wa Kahawa Wilayani Mbinga kuanzia msimu huu wa mwaka 2019. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na maswali madogo mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ni kweli Serikali imepeleka zao la korosho katika Kata za Rwanda na Litumbandyosi. Changamoto ya wakulima hao ni upatikanaji wa miche bora na kwa bei nafuu. Je, Serikali iko tayari kuendelea kutoa miche ya mikorosho bora kwa bei nafuu au bure kwa wananchi wa Kata ya Rwanda na Litumbandyosi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika jibu la msingi, Serikali imekiri kuwa ilitoa mafunzo ya uzalishaji wa miche bora ya mikorosho katika vikundi sita vya Jembe Halimtupi Mtu, Chapakazi, Twiga, Juhudi, Kiboko na Korosho ni Mali lakini vikundi hivi bado vinaidai Bodi ya Korosho. Je, ni lini madeni ya vikundi hivyo yatalipwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Martin Msuha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anataka kujua kwamba kama Serikali tuna...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, usirudie swali lake mjibu tu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tupo tayari kupeleka miche ya mikoroshu kwa bei nafuu kwa wakulima wa Wilaya ya Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kama tunavyofahamu deni likivuka mwaka madeni yote haya ya Serikali yanahamia Hazina. Sasa hivi Serikali tuko kwenye hatua za mwisho za kumalizia uhakiki na vikundi vyote ambavyo uhakiki umemalizika vimeshaanza kulipwa na hivi alivyovitaja vitaanza kulipwa baada ya uhakiki kukamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Serikali imeamua zao la mchikichi lilimwe Kigoma na liweze kuwa zao la biashara na Waziri Mkuu kwa kuweka msisitizo ameenda Kigoma mara tatu kufuatilia zao hili la mchikichi; na kwa kuwa wananchi wameamua kuitikia mwito huo wa kulima zao hilo...

**MWENYEKITI:** Swali.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali iko tayari sasa kuhakikisha wananchi wanapata mbegu na kuanza kulima zao hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Genzabuke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tuko tayari kwa ajili ya uzalishaji wa miche ya michikichi na kuigawa kwa wakulima. Sasa hivi tumeshatenga zaidi ya shilingi bilioni 5 kwa ajili ya kuanza uzalishaji mwaka huu na mwaka huu mwezi Septemba, miche zaidi ya milioni moja itakwenda sokoni. Tumeshaingia mkataba na sekta binafsi kuzalisha miche milioni tano kwa msimu huu unaokuja na ndani ya miaka mitatu tunategemea kuzalisha miche zaidi ya milioni 20 na kuigawa Tanzania nzima.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini sasa uliza swali lako.

Na. 93

### **Mradi wa REA II - Jimbo la Mbulu Mjini**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** Aliuliza:-

Katika mradi wa REA I na II vijiji vingi vya Jimbo la Mbulu Mjini havikufikiwa na umeme na katika vijiji vilivyofikiwa ni kaya kati ya 20 mpaka 30 pekee ndizo zilizopata umeme:-

(a) Je, ni lini REA III itapeleka umeme katika Vijiji 26 vya Jimbo la Mbulu Mjini?



(b) Awamu ya I na II ziliruka shule nyingi, vituo vya afya na Makanisa. Je, ni lini sasa taasisi hizo zitapelekewa umeme?

(c) Je, ni lini Serikali itarudia usambazaji wa umeme katika vijiji vyote vilivyosambaziwa sehemu ndogo sana katika Jimbo la Mbulu Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Mradi wa *REA III*, Mzunguko wa Kwanza katika Jimbo la Mbulu Mjini, jumla ya Vijiji vitatu vya Gwaami, Tsaayo na Banee vitapatiwa umeme na Mkandarasi Kampuni ya *Angelique International Limited*.

Aidha, vijiji vitatu vya Murray, Silaroda na Gunyoda vinaendelea kupelekewa umeme na Shirika la Umeme Nchini (*TANESCO*) kwa Mpango wa Umeme Vijijini. Vijiji 20 vilivyobaki vya Jimbo la Mbulu Mjini vya Hereabi, Maheri, Kuta, Qwam, Nahasey, Hayasali, Hasama, Hayloto, Kwermusi, Amowa, Gwandumehhi, Aicho, Gedamar, Qalieda, Laghanda mur, Gidamba, Qatesh, Landa, Tsawa na Jaranja vitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA III*, Mzunguko wa Pili unatarajiwa kuanza Januari, 2020.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, shule, vituo vya afya na taasisi nyingine ambazo hazijaunganishwa umeme katika vijiji au maeneo ya karibu yaliyounganishwa umeme na miradi ya awali ikiwemo *REA I* na *II* yatapelekewa umeme katika kipindi hiki. Tumetoa wito kwa Halmashauri au taasisi husika zilipie gharama za kuunganisha umeme ili taasisi hizo ziunganishiwe umeme.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maeneo ya Mbulu Mjini yaliyosambaziwa umeme, tunawaomba wananchi wa maeneo ya karibu na maeneo yenye umeme kuendelea kulipia Sh.27,000 ili maeneo hayo nayo yatumie umeme huo uliopo katika maeneo hayo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nimpungeze Mheshimiwa Rais wetu na Serikali nzima, Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa kazi kubwa wanayofanya katika nchi yetu hususani Jimbo la Mbulu Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu madogo ya nyongeza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa mahitaji ya umeme katika Jimbo la Mbulu Mji ni makubwa; na kwa kuwa Jimbo la Mbulu Mji sehemu nyingi zilikosa umeme wakati wa *REA I* na *II*. Je, sasa Serikali inachukua hatua gani kwa wale wananchi ambao hadi sasa wameendelea kuachwa na umeme umeshapita kwenye maeneo yao na maombi yao hayajibiwi na Ofisi yangu ina orodha kubwa sana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa mahitaji ni makubwa sana ya chombo kinachoitwa UMETA (Umeme Tayari) na kwa kuwa majengo mengi katika Jimbo la Mbulu Mjini yako mbalimbali kwa maana ya nyumba za wananchi. Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta chombo hiki cha UMETA kwa kiasi kikubwa ili kuwapatia wananchi umeme ambao wana uhitaji mkubwa sana?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zacharia, Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini. Nampongeza

kwa kazi nzuri anayoifanya katika Jimbo lake hususani katika kufuatilia sekta ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ameuliza Serikali ina mpango gani kwa kuwa mahitaji ya umeme ni makubwa na kwa maeneo mbalimbali ambayo hayajafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba kupitia Serikali yetu kuna Mradi wa Ujazilizi Awamu ya Pili B ambapo Mkoa wa Manyara ni miongoni mwa mikoa 16 ambayo itahudumiwa. Kwa sasa Mshauri Elekezi *Multiconsult* na *Norplan* wanaendelea kuhakiki vitongoji katika maeneo mbalimbali. Mradi huu utafadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa kwa Euro milioni 100 na unatarajiwa kuanza mapema mwakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sambamba na miradi ya *REA III* ambayo itaendelea kupitia *TANESCO*, nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwa jitihada hizi na huu Mradi wa Ujazilizi kwenye maeneo ambayo umepita vitongoji vimeachwa, Jimbo lake la Mbulu Mjini nalo litazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili ameulizia masuala ya kifaa kinachoitwa UMETA. Kwanza Serikali kupitia utekelezaji wa Mradi wa *REA III*, Mzunguko wa Kwanza vimetoa UMETA 250 kwa kila mkandarasi ambapo vinagaiwa bure kwa makundi maalum. Sambamba na hilo, kwa kuwa tumeona uhitaji ni mkubwa Shirika la *TANESCO* na *REA* wanaendelea na mchakato wa kuhakikisha UMETA inapatikana kwa bei nafuu ambayo ni Sh.36,000 ambapo kila mwananchi ana uwezo wa kumudu.

Kwa hiyo, niendeleo kutoa maelekezo kwa niaba ya Waziri wa Nishati, *TANESCO* na *REA* kuendelea kusambaza UMETA hasa kwenye taasisi za umma ambazo hazina mahitaji makubwa na wananchi wa kawaida. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad.

Na. 94

## Hitaji la Umeme katika baadhi ya Vijiji Shinyanga

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA (K.n.y. MHE. AZZA H. HAMAD)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawapa huduma ya umeme wananchi wa Vijiji vya Buyubi, Itwangi, Imenya, Nyambui na Mwankanga ambao muda mrefu wamekuwa watazamaji wa nguzo za umeme unaokwenda maeneo mengine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) inatekeleza mradi wa kufikisha umeme katika vijiji vyote nchini vikiwemo vijiji 126 vya Wilaya ya Shinyanga Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji 22 kati ya vijiji 126 katika Wilaya ya Shinyanga Vijijini vina umeme. Vijiji 50 vitapatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA III*, Mzunguko wa Kwanza unaotekezwa na Mkandarasi *Angelique International Limited* ambapo hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Agosti, 2019 jumla ya vijiji 19 vimeshawashiwa umeme na ujenzi wa miundombinu unaendelea katika vijiji vilivyobaki na wateja zaidi ya 211 wameunganishiwa umeme. Kazi ya kupeleka umeme katika vijiji hivi itakamilika ifikapo mwezi Juni, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kupeleka umeme katika vijiji 50 vya Wilaya ya Shinyanga Vijijini inahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilometa 170.9; ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilometa 156; ufungaji wa

transfoma 78 za KVA 50 na KVA 100 na kuunganisha umeme wateja wa awali 2,241. Gharama za mradi ni shilingi bilioni 10.7 na mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji 54 vilivyobaki vikiwemo vijiji vya Buyubi, Itwangi, Imenya, Nyambui na Mwankanga vitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA III*, Mzunguko wa Pili unaotarajia kuanza mwezi Januari, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Jecha.

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa Serikali ilielekeza *TANESCO* kwamba vijiji vyote ambavyo umeme umepita juu vipatiwe umeme. Miongoni mwa vijiji 74 ambapo kuna Vijiji vya Buyungi, Imenya, Itwangi na Nyambui, je, Serikali itavipatia umeme lini katika huu msimu wa 2019/2020? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Naibu Waziri aliahidi wananchi wa Nyambui atawapatia umeme. Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya swali la msingi lakini nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuuliza swali kwa wananchi wa Shinyanga kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitoe taarifa Kijiji cha Itwangi kimewashwa umeme tangu juzi ingawaje swali wakati linajibiwa kilikuwa hakijawashwa umeme, kwa hiyo, kimeshawashwa umeme. Kwa hiyo, wananchi wa Itwangi

sasa wanapata umeme kupitia Shirika la Umeme Nchini (TANESCO).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Buyubi pamoja na Minyami kitawashwa tarehe 17 mwezi huu wa Septemba. Kwa hiyo, wananchi wa maeneo hayo wategemee kuunganishiwa umeme katika maeneo hayo kwa wiki inayokuja. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Fedha na swali la Mheshimiwa Boniphace Getere.

Na. 95

### **Kudhibiti Kasi ya Ongezeko la Idadi ya Watu Nchini**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** Aliuliza:-

Idadi ya watu nchini inaongezeka kwa kasi sana na watu wanahitaji maendeleo; aidha ukuaji huu una matokeo hasi na chanya:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kutumia au kudhibiti kasi ya idadi ya watu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa idadi ya watu duniani unaonyesha kwamba idadi kubwa ya watu ni fursa kwa nchi iwapo baadhi ya mambo matano yatafanyika:-

(i) Kuboresha maisha ya watoto na kuboresha elimu na uwezeshaji kwa wanawake;

(ii) Kuimarisha uwekezaji katika afya ili kuwa na nguvukazi bora na yenye tija;

(iii) Kuimarisha uwekezaji katika elimu ya juu ili kuwa na nguvukazi yenye elimu, ujuzi na ubunifu;

(iv) Mageuzi ya kiuchumi yanayolenga kuharakisha ukuaji wa uchumi na upatikanaji wa kazi kwa ajili ya nguvukazi iliyopo; na

(v) Mageuzi ya Sera ili kuvutia uwekezaji wa kigeni na kuhakikisha uwajibikaji hasa katika rasilimali za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhima ya Mpango wetu wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 – 2020/2021 ni kujenga uchumi wa viwanda ili kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu. Mpango huu wa Pili umejikita zaidi katika uwekezaji wa kimkakati katika Sekta ya Viwanda kuimarisha miundombinu ya usafiri na usafirishaji, kusambaza umeme mijini na vijijini, kusambaza pembejeo za kilimo kwa wakati, kutatua changamoto ya muda mrefu ya upatikanaji wa umeme wa uhakika kwa kujenga bwawa kubwa la kufua umeme katika Mto Rufiji na kuimarisha huduma za jamii kwa kujenga na kukarabati miundombinu ya maji, hospitali na Vituo vya Afya vya Umma, shule pamoja na kutekeleza kwa ufanisi Sera ya Elimu Bila Malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi inayoendelea kutekelezwa na Serikali ya Awamu ya Tano inalenga kufungamanisha fursa za kiuchumi na ongezeko la idadi ya watu; na jitihada hizi zinalandana na mambo yaliyopendekezwa kwenye ripoti ya utafiti ya idadi ya watu duniani na athari zake. Hata hivyo, matokeo chanya yataonekana kama kila Mtanzania atashiriki kikamilifu katika uzalishaji mali na huduma za jamii kuanzia ngazi ya kaya hadi Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo jambo baya kudhibiti ongezeko la idadi ya watu kama familia au Taifa limefikia kiwango cha mwisho cha kutumia rasilimali (*optimal*)

*utilization*) ya rasilimali zake za asili pamoja na mikakati mingine mbadala. Hata hivyo, Taifa letu bado lina rasilimali asili za kutosha kama vile ardhi ya kulima, bahari, maziwa, mito na mabonde, madini, misitu, jioografia ya usafiri na usafirishaji pamoja na fursa za utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jukumu letu kama Taifa kuanzia ngazi ya kaya kuakisi jitihada zinazofanywa na Serikali yetu na hatimaye kutumia fursa hizi kwa ufanisi kwa lengo la kuongeza kasi ya uzalishaji mali pamoja na kuongeza kasi ya kupunguza umasikini badala ya kuogopa ongezeko la idadi ya watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sasa Serikali imejielekeza zaidi katika kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji na kufanya biashara na hivyo kutumia ongezeko la idadi ya watu kama fursa ya nguvukazi ya kuzalisha mali pamoja na soko la bidhaa na huduma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Amejieleza vizuri, tumeyaona kwenye karatasi hapo na yapo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya watu katika nchi yetu inaongezeka na toka tumepata uhuru mwaka 1961 na Muungano 1964 tumeendelea kupambana na maadui watatu ambao ni ujinga, maradhi na umasikini. Angalau haya mawili ya maradhi na ujinga tunaelekea kuyamudu ndiyo maana idadi ya watu inaongezeka.

**MWENYEKITI:** Swali, swali!

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali; Serikali ina mpango gani sasa wa kupambana na adui



namba moja ambaye ni umasikini unaoongezeka katika maeneo mengi hasa maeneo ya vijijini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kumekuwa na makundi makubwa ya vijana wanaohitimu elimu hasa Elimu ya Vyuo Vikuu. Sasa ndhi yetu ipo kwenye mkakati wa kujenga viwanda: Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwekeza katika viwanda vya *Labor Intensive* badala ya *Capital Intensive* ili kukidhi makundi makubwa ya vijana yanayohitimu shule na kwa sababu fursa tunazo? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wazirui, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba umasikini ndani ya nchi yetu hauongezeki, unapungua kila mwaka. Hii naisema, siyo maneno yangu, ni maneno ya utafiti ambao umefanyika. Utafiti wa mapato na matumizi ya kaya binafsi uliofanyika mwaka 2018 na Mheshimiwa Waziri Mkuu akauzindua utafiti huu, unaonesha kwamba umasikini wa kipato umepungua kutoka asilimia 28.2 toka mwaka 2012 na sasa umefika asilimia 26.8 mwaka 2018. Hivyo siyo sahihi kuendelea kuimba wimbo wa Taifa letu kwamba watu wanazidi kuwa masikini. Siyo sahihi hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti huu pia unaonesha umasikini wa chakula kwa Watanzania katika kila kaya, mwaka 2012 ulikuwa asilimia 9.7; mwaka 2018 umasikini wa chakula kwa kaya ya kila Mtanzania ni asilimia 4.4. Kwa hiyo, tunaomba Watanzania wafahamu kwamba jitihada za Serikali yao na wao Watanzania wamejitolea kuelewa jitihada hizi za Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali yake wanafanya kazi kwa jitihada zote. Umasikini wa kipato na umasikini wa chakula umepungua kutokana na tafiti zilizofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili kwamba tuwekeze kwenye viwanda ambavyo vinatumia rasilimali watu zaidi kuliko kutumia *capital intensive*. Naomba

kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika viwanda ambavyo vimeanzishwa na vinaendelea kujengwa kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa uwekezaji asubuhi, ni viwanda vinavyotumia zaidi rasilimali watu. Viwanda hivi ni vile ambavyo vipo katika maeneo ya nguo. Tunafahamu hatujafanya vizuri zaidi, lakini jitihada zinaendelea kufanyika. Viwanda vya kutengeneza *tiles* havitumii mashine, vinatumia rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vingine ni vya kuchakata mazao yetu, havitumii *capital*, vinatumia zaidi rasilimali watu. Nawaomba Watanzania wanaomaliza Vyuo Vikuu waweze kwenda kufanya kazi kwa tija kwenye viwanda hivyo.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba.

Na. 96

### Hitaji la Mahakama ya Wilaya – Itilima

**MHE. ANATHROPIA L. THEONEST (K.n.y. MHE. GIMBI D. MASABA)** Aliuliza:

Wilaya mpya ya Itilima haina Mahakama ya Wilaya, jambo linalosababisha usumbufu mkubwa kwa wananchi kwenda Wilaya jirani ya Bariadi kupata huduma hiyo:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya Itilima?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Gimbi Dotto Masamba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Wilaya ya Itilima kwa sasa haina Mahakama ya Wilaya na wananchi wanalazimika

kusafiri umbali mrefu takriban kilometa 37 kufuata huduma katika Wilaya ya Bariadi. Aidha, changamoto hii ipo kwenye Wilaya 27 nchini, ambazo zinapata huduma katika wilaya za jirani. Hii inatokana na ukweli kwamba Mahakama ya Tanzania bado inakabiliwa na uhaba wa majengo katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimekuwa nikieleza katika Bunge lako, Mahakama imejiwekea mkakati wa kutatua changamoto hii hatua kwa hatua kupitia mpango wake wa miaka mitano na kujenga na kukarabati majengo ya Mahakama kwa ngazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Wilaya ya Itilima ipo kwenye mpango wa kujengwa kwa mwaka 2019/2020 pamoja na Mahakama nyingine za Wilaya za Busega, Kyerwa, Misenyi, Gairo, Mbogwe, Songwe, Rufiji, Kibiti, Nyang'hwale, Mvomero, Uyui, Kaliua, Uvinza, Buhigwe, Kakonko, Chamwino, Chemba, Ikungi, Mkalama, Butiama, Rorya, Ubungo, Malinyi, Tanganyika, Mkinga, Kilosa, Kilombero, Hanang na Nkasi. *(Makoff)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima kwa kutupatia kiwanja cha kujenga Mahakama ya Wilaya yenye ukubwa wa mita za mraba 5,028. Aidha, nitoe pia shukrani zangu za dhati kwa Halmashauri za Wilaya zote nilizozitaja kwa kutupatia viwanja kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Mahakama. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Masaba, kwa niaba yake Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya Serikali kuahidi kwamba inaenda kujenga jengo hilo la Mahakama ya Wilaya katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, bado Mahakama ya Bariadi inapitia changamoto ya upungufu wa Mahakimu, hivyo kusababisha kesi nyingi kuchelewa: Je, Serikali ina mpango gani kwa wakati huu mfupi kuisaidia Mahakama ya Bariadi ili iweze kukidhi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wakati wananchi wa Itilima wanatembea kilometa 37, wenzao wa Wilaya ya Kyerwa wanatembea zaidi ya kilometa 100. Wananchi wa Murongo, Kaisho, Bugomora, Bugara, wanatembea umbali mrefu kufuata hiyo huduma katika Mahakama iliyoko Wilaya ya jirani...

**MWENYEKITI:** Swali! Uliza swali!

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali. Ni mkakati gani wa muda mfupi kuwasaidia wananchi wa Kyerwa waweze kupata huduma katika wilaya yao kabla ya kufikia mwaka 2019/2020. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama ya Bariadi inafanya kazi nzuri sana. Hivi karibuni nilipitia kule na nikaona msongamano wa kesi mbalimbali. Ni moja ya majukumu makubwa ya Wizara hii, siyo tu kujenga Mahakama katika ngazi mbalimbali, lakini kutoa mafunzo kwa Mahakimu kadri ujenzi unavyoendelea. Hii inaenda sambamba na kuwasaidia wananchi kwa kuwapa haki ya kusimamia mashauri yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili. Mahakama ya Wilaya ya Kyerwa inahitaji kupata Mahakama yake mara moja. Katika mpango wa Mahakama ya Tanzania kama nilivyoeleza siyo tu tunataka kuleta Mahakama karibu na wananchi, lakini kuhakikisha kwamba tunapunguza kero ambazo wananchi wanapata ili kupata haki yao na kwa wakati. Kutokana na mkakati huo, tutaendelea kusomesha Mahakimu katika ngazi mbalimbali na tutaendelea kupanua ujenzi wa Mahakama katika ngazi mbalimbali hasa katika wilaya hiyo ambayo Mheshimiwa umeizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu mazuri. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Eng. Christopher Kajoro Chiza, Mbunge wa Buyungu aulize swali lake.

Na. 97

### **Kutokukamilika kwa Miradi ya Maji – Kakonko**

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA** Aliuliza:-

Serikali ilitoa zaidi ya shilingi bilioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji ya Nyabibuye, Gwanumpu, Muhange, Kiduduye, Nyangwijima na Kakonko Mjini. Miradi hiyo sasa inahitaji ukarabati mkubwa hata kabla ya kuanza uzalishaji na mingine utekelezaji upo chini ya asilimia 10:-

(a) Je, ni kasoro gani zimesababisha miradi yote sita kutotekelezwa kwa mwaka uliopangwa?

(b) Serikali imechukua hatua gani kuhakikisha miradi hiyo inakamilika?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christopher Chiza Mbunge wa Buyungu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi ya Muhange, Kiduduye na Nyangwijima ulikamilika lakini ulishindwa kuwanufaisha wananchi kutokana na kasoro mbalimbali zilizojitokeza ikiwemo eneo la kisima cha pampu cha mradi wa Muhange kujaa tope; na pia kwa mradi wa maji Nyagwijima na Kiduduye eneo la chanzo kushindwa kuzuia maji kuyapeleka kwenye kisima chenye pampu hii imetokana na matatizo ya usanifu yaliyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha miradi hii inatoa huduma kwa wananchi kama ilivyokusudiwa, Serikali imechukua hatua mbalimbali kwa miradi ya Muhange, Kiduduye na Nyagwijima, Wizara imefanya mapitio ya usanifu ambapo kiasi cha shilingi milioni 300 kimekadiriwa ili kurekebisha kasoro zilizojitokeza. Tayari Serikali imetoa kiasi cha shilingi milioni 120 kwa ajili ya maboresho ya mradi wa maji Muhange ambapo utekelezaji unaendelea na umefikia asilimia 45. Serikali itaendelea kutenga na kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha pia miradi ya Nyagwijima na Kiduduye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji Gwanumpu, Nyabibuye na Kakonko Mjini utekelezaji wake ulichelewa kutokana na wakandarasi kujenga miradi hiyo kwa kasi ndogo kutokana na uwezo mdogo wa kifedha. Hali hii ilisababisha baadhi kusitishwa mikataba yao. Mkandarasi wa Mradi wa Gwanumpu yupo eneo la mradi na anaendelea na kazi ambapo amefikia asilimia 40. Kwa Mradi wa Maji wa Nyabibuye na Kakonko Mjini taratibu za kusaini mikataba na wakandarasi wapya zinaendelea ili waweze kukamilisha utekelezaji wa miradi hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Chiza.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza niishukuru sana Serikali kwa kuanza kutekeleza ahadi yak. Baada ya Waziri kutembelea na kusikia kilio cha wananchi imetenga shilingi milioni 300 na tayari wamepeleka shilingi milioni 20 na wataalam wameanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza. Katika *lot* ya miradi ya Kiduduye, Nyagwijima na Muhange, kwa kuwa tayari mradi wa Muhange unatekelezwa: Je, ni lini sasa Serikali itapeleka wataalam na fedha kwa ajili ya miradi miwili ya Nyagwijima na Kiduduye kuanza kutekelezwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Wakati Mheshimiwa Waziri wa Maji akihitimisha hotuba yake ya Bajeti

ya mwaka huu, alituhamasisha Wabunge wote kupeleka orodha ya visima vinavyofaa kuchimbwa katika Majimbo yetu, nami nilikuwa wa kwanza kumkabidhi orodha ya visima 15 vilivyofanyiwa utafiti: Je sasa, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuniambia au kuwaambia wananchi wa Buyungu ni lini sasa ligi itapelekwa katika Jimbo la Buyungu kuanza kuchimba visima hivi 15? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kwa muda mfupi tangu amechaguliwa na wananchi wake. Kikubwa amekuwa mfuatiliaji, nasi kama Wizara hatutakuwa kikwazo kum-*support* kuhakikisha tunatatua tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa sana kusuasua kwa miradi ya maji kulikuwa kunatokana na wakandarasi wababishaji. Sisi kama Wizara ya Maji, tumejipanga, sasa hivi tumeanzisha Wakala wa Maji kwa maana ya *RUWASA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie, kwa miradi ile ambayo imekuwa ikisuasua, tutaitekeleza kwa kutumia wataalam wetu wa ndani ili kuweza kukamilisha miradi ile kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, miradi hiyo tutaifanya kwa wataalam wetu na tutawa-*support* kuwapatia fedha ili miradi iweze kukamilika na wananchi wako, waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ahadi ya visima, ahadi ni deni. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tukutane tufanye mazungumzo na wenzetu wa *DDC* ili tuwatume waende kuchimba visima kwa wananchi wake waweze kupata huduma hii muhimu ya maji safi na salama.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Madini, Mheshimiwa Janet Mbene.

Na. 98

### **Kufanya Mapitio ya *Geological Survey* Ileje**

**MHE. JANET Z. MBENE** Aliuliza:-

*Geological Surveys* za Wilaya au Mkoa mingi ni za miaka mingi tangu enzi za ukoloni. *Surveys* hizi nyingi zimejikita kwenye aina moja ya migodi kwa mfano Mkoa wa Songwe *Survey* imezungumzia machimbo ya mawe peke yake:-

(a) Je, ni lini Serikali itafanya mapitio ili kupata *Geological Surveys* zenye kujumuisha aina nyingine za madini ambayo yanapatikana katika Mkoa wa Songwe hususan Ileje?

(b) Je, Serikali ipo tayari kwenda kuwaelimisha wananchi wa Ileje juu ya madini yaliyopo na kuhamasisha uwekezaji kwa wachimbaji wadogo?

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** Alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janet Zebedayo Mbene, Mbunge wa Ileje, lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (*GST*) imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali za jiolojia kwa ajili ya kuainisha madini mbalimbali yaliyopo nchini tangu kipindi cha mkoloni hadi sasa. Aidha, *GST* kwa ushirikiano na ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya watu wa Korea imeanza kufanya utafiti wa kina wa kijiolojia ili kuongeza na kuboresha taarifa za uwepo wa madini mengine katika Mkoa wa Songwe na mikoa mingine nchini.



Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zilizofanyika Mkoa wa Songwe zinaonesha kuwa Wilaya ya Ileje ina madini yafuatayo; moja ikiwa ni madini ya metali aina ya dhahabu yanayopatikana katika maeneo ya Mwalisi na Ikinga, Madini ya Viwandani aina ya Ulanga, yanayopatikana katika maeneo ya vilima vya Bundali na Ileje, madini ya nishati aina ya makaa ya mawe (*Coal*) yanapatikana katika maeneo ya Songwe, Kiwira na madini ya *apatite* na *niobium* yanayopatikana katika miamba ya *carbonatite* iliyopo maeneo ya kilima cha Nachendazwaya, ikiwa ni pamoja na madini mengine kama *marble* na madini mengine ya ujenzi.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania itaendelea kufanya tafiti mbalimbali za madini katika Wilaya ya Ileje na maeneo mengine ya nchi kwa kadri ya upatikanaji wa rasilimali ya fedha na kutoa elimu kwa wananchi juu ya upatikanaji wa madini katika maeneo mbalimbali ya nchi ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya madini kwa wachimbaji wadogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbene.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Naibu Waziri kwa majibu ingawa ningefurahi zaidi yangukuwa siyo ya kijumla kiasi hicho kwa sababu ningependa japo nisikie tu kuwa kama wapo tayari kuja kufanya hata mafunzo tu kwa ajili ya vijana wetu ambao wanajishughulisha na shughuli hizi. Hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza:

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni kuhusiana na ule Mgodi wa Kiwira ule wa *underground*. Mgodi ule umesimama kwa muda mrefu sana na hivi sasa tunavyozungumza hatuna hakika yaani kuna sintofahamu ya kujua ni nani mwekezaji na lini ataanza kufanya kazi ili tuweze kuona mafanikio ya mgodi ule?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni kuwa mwaka 2010 Kamati ya Kudumu ya Bunge ilishauri kuwa mgodi ule

uwekwe chini ya *STAMICO* na *TANESCO* kwa sababu madhumuni ya mgodi ule ilikuwa ni kuzalisha umeme, lakini mpaka sasa hivi tunaona uko chini ya *STAMICO* lakini hatuoni ule ubia na *TANESCO* ambao ungesaidia sasa katika kuhakikisha kuwa umeme unapatikana? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba ule Mgodi wa Kiwira umesimama kwa muda mrefu sasa na tatizo lilikuwa ni moja tu, baada ya ile kampuni ya *TAN Power Resources* kutoka pale ilitakiwa kwamba wahamishe zile *share* zao ili ziweze kuchukuliwa na Serikali na *share* hizo tungeweza kuzipeleka *STAMICO* kwa ajili ya kuanzisha au kuendeleza mradi ule.

Sasa wale *TAN Power Resources* walikuwa na deni ambalo walitakiwa walipe (*capital gain tax*) ambayo ilikuwa ni deni la bilioni 2.9 hawajalipa lile deni na Serikali kupitia *TRA* ni kwamba wanafatilia kuweza kuwabana wale wahusika waweze kulipa deni hilo ili tuweze kupata *tax clearance* na kuhamisha zile *share* ziweze kwenda Serikalini au *STAMICO* ili kuweza kuanzisha mradi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi *TRA* wanaendelea kufatilia hawa *TAN Power Resources* na inasemekana hawapo na watu hawa ambao hawapo sasa hivi kuna hatua inayofuata ya kufatilia kuwajua ma-*director* wa ile *TAN Power Resources* na kuweza kuwabana ikiwezekana kwenda kuchukua *passport* zao binafsi ili waweze kulipa lile deni la 2.9 bilioni. Baada ya kufanya hivyo *STAMICO* wakishachukua mradi huo mara moja mradi ule utaanza na uchimbaji utaendelea. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa maswali yetu yamekwisha sasa ni kipindi cha wageni. Wageni wa Mheshimiwa Spika ambao wako Jukwaa la Spika ni Balozi wa Pakistan nchini Tanzania Mheshimiwa Amer Mohamed Khan, *welcome to the Parliament of Tanzania. (Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii wageni waliopo Jukwaa la Spika wageni 11 wa Mheshimiwa Spika kutoka Jukwaa la Maendeleo Endelevu Jijini Dar es Salaam ambao ni Ndugu Richard Angelo, Ndugu Getrude Mugizi, Ngd. Stephen Chacha, Ndugu Iman Khatib, Ndugu Prisca Kowa, Ndugu Reynad Maeda, Ndugu Vivian Ngowi, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 18 wa Mheshimiwa Spika, kutoka Benki ya NBC ambao ni Mameneja wa Kanda, Mameneja wa Mauzo na Mameneja Mahusiano wa Benki hiyo wakiongozwa na Mkurugenzi wa Wateja Binafsi - NBCNdugu Elibariki Masuke, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Spika ni waandaaji wa Kipindi cha AMINIA 255 (Najivunia Tanzania) cha Kampuni ya Clouds Media, Simon Simalenga - Mwenyekiti, Jerome Risasi - Katibu, Dotto Bahema - Mjumbe, Kijakazi Yunus - Mjumbe, na Hassan Ngoma - Mjumbe, karibuni sana na hongereni kwa kazi nzuri mnayoifanya. *(Makofi)*

Wageni 13 wa Mheshimiwa Naibu Spika, na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa Mbunge Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi ambao ni Viongozi wa CCM Mbeya, wakiongozwa na Ndugu Afrey Nsomba - Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbeya Mjini, Ndugu Gervas Ndaki - Katibu wa CCM Wilaya ya Mbeya Mjini na Ndugu Philemon Mng'ong'o - Katibu Mwenezi wa CCM Mbeya Mjini. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa Waziri wa Viwanda na Biashara kutoka Chama cha Wasioona Tanzania ambao wamekuja kama wageni wangu kushuhudia Azimio la Kuridhia Mkataba wa Marrakesh wakifuatana na Mwenyekiti wao Ndugu Luis Benedict na Emmanuel Saimon. *(Makofi)*

Wageni saba wa Mheshimiwa Prof. Aderaldus Kilangi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambao ni watumishi kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Zanzibar wakiongozwa

na Naibu Mwanansheria Mkuu Ndugu Mzee Ali Haji, karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Dkt. Harrisom Mwakyembe Waziri wa Habari Sanaa, Utamaduni na Michezo ambao ni vingozi kutoka *Multi Choice Tanzania*, Tasnia ya Filamu Tanzania na *The Look Company Ltd.*wakiongozwa na Mratibu wa Mashindano ya Miss Tanzania na *Miss World* Ndugu Basila Mwanukuzi, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni Wawili wa Mheshimiwa Dotto Biteko, Waziri wa Madini ambao ni wapiga kura wake kutoka Bukombe wakiongozwa na Madiwani Mheshimiwa Masanja Maduhu, karibuni. *(Makofi)*

Wageni Watatuwa Mheshimiwa Omary Mgumba Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni wadau wa Sekta ya Kilimo kutoka Mkoa wa Iringa Ndugu Sosthenes Mushi, Ndugu Edger Msengi na Ndugu Joshua Muna.Wageni wa Mheshimiwa Mwita Waitara Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais- TAMISEMI ambaye ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Wilaya ya Ilala kutoka Kivule jijini Dar es Salaam Ndugu Yansika Getama, karibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 12 wa Mheshimiwa Elias Kwandikwa ambao ni Kamati ya Siasa Wilaya ya Kahama kutoka Mkoa wa Shinyanga wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya Ndugu Thomas Muyonga, karibuni Waziri wenu anafanya kazi vizuri sana kwa hiyo msifanye makosa.Wageni Watatuwa Mheshimiwa Hussein Bashe Naibu Waziri wa Kilimo kutoka Shirika la Chakula Duniani (WFP) Ofisi ya Tanzania wakiongozwa na Mkurugenzi Mkaazi Ndugu Michael Banford, karibuni Bungeni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ambaye ni mpiga kura wake kutoka Jijini Dar es Salaam Ndugu Yona Kilatu Msoma, karibu. Mgeni wa Mheshimiwa Rashid Shangazi Mbunge ambaye ni ndugu yake kutoka Jijini Arusha Ndugu Likoko Piniel, Karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 47 wa Mheshimiwa Sonia Magogo ambao ni Walimu na wanafunzi (Scout) wa Shule ya Msingi St. Maxmillian iliyopo Tabata Segerea kutoka jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Mwalimu Constantine Magehema, karibuni. *(Makofi)*

Wageni Wawiliwa Mheshimiwa Anatropia Theonest ambao ni ndugu zake kutoka Jijini Dar es Salaam Ndugu Renatha Theonest na Ndugu Brito Burere. Wageni 17 wa Mheshimiwa Hamida Abdallah ambao ni Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Chipukizi Taifa kutoka Mkoa wa Lindi wakiongozwa na Ndugu Paksens Kisamo. Karibuni. Wageni Wawiliwa Mheshimiwa Joseph Kakunda ambao ni walimu wa Shule ya Sekondari ya Oldonyosambo ya Jijini Arusha Ndugu Nyangusi Kissangai na Ndugu Namnyaki Laizer, karibuni. *(Makofi)*

Wageni Sabawa Mheshimiwa Sikudhani Chikambo ambao ni jamaa zake. Salum Mohamed mtoto wake Dalia Halid Mwenyekiti wa Wawalemavu Tunduru, Rehema Burhan Tunduru, Amos Mpita ndugu yake, Amir Ngwale ndugu yake Hanifa Mkura ndugu yake, Ndugu Said Athuman ndugu yake. Wageni 2 wa Mheshimiwa Ally Ungando ambao ni wapigakura wake kutoka Jimbo la Kibiti Mkoa wa Pwani Ndugu Daniel Motera na Ndugu Ally Ismail, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 4 wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambao ni viongozi wa Machinga kutoka Mkoa wa Mwanza wakiongozwa na Ndugu Jamal Said. Pia tunao wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo wanafunzi 40 kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Mwongozo Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niombe mwongozo kwa

mujibu wa Kanuni ya 68 (7), na kwa kuwa muda wenyewe tunakimbizana nao sina sababu ya kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi wakati wa kipindi cha maswali na majibu Mheshimiwa Naibu Waziri rafiki yangu Hussein Bashe akijibu swali kuhusu masuala ya Sumukuvu alisema Sumukuvu iliwapata wagonjwa ama iliwapata watu katika Wilaya ya Kondoa na wanahitaji msaada ikiwa ni pamoja na mbegu. Sasa naomba mwongozo wako ugonjwa huu wa Sumukuvu ulitokea Wilaya ya Chemba katika vijiji vya Kinkima na Mlongia ambako zaidi ya wagonjwa 35 waliathirika isipokuwa walikwenda kulazwa kwenye Hospitali ya Wilaya ya Kondoa kwa sababu Chemba hospitali yetu bado haijaanza kazi. Sasa nilikuwa naomba mwongozo wako wananchi wale vyakula vyao vimemwagwa wakitegemea kupata vyakula kutoka Serikalini, hiyo ni namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namba mbili, pamoja na mbegu zao zote zimemwagwa, sasa nilikuwa naomba mwongozo wako ni lini Serikali itawapelekea chakula wananchi hawa wa Wilaya ya Chemba na siyo Kondoa nasisitiza tena ambao waliathirika, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri amekusikia baadaye mtakaa, mta-*caucus* mtajadili. Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI-KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAAZIMIO**

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya pamoja ya ziada ya Nagoya-Kuala Lumpur kuhusu Uwajibikaji Kisheria na Fidha kwa

Madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya Bioteknolojia ya Kisasa katika Kutekeleza Itifaki ya Cartagena (*Nagoya – Kuala Lumpur Supplementary Protocol on Liability and Redress on Cartagena Protocol on Biosafety*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki ya ziada ya Nagoya Kuala Lumpur kuhusu uwajibikaji Kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya Bioteknolojia ya Kisasa ilianzishwa ili kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Cartagena inayohusu matumizi salama ya Bioteknolojia ya kisasa iliyopitishwa na nchi wanachama wa Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai mwaka 2000 ambapo Tanzania iliridhia itifaki mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la Itifaki ya Cartagena ni kudhibiti na kusimamia matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa miongoni mwa nchi wanachama. Katika kutekeleza Itifaki hii Tanzania imepata fursa ya kujengewa uwezo wa kitaasisi na kitaalamu kuhusu usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa hususani katika masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuweka mfumo wa Kitaifa wa usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa, kuandaa na kutekeleza kanuni za matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa za mwaka 2009 na miongozo mbalimbali kuhusu matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa na kutoa mafunzo ya vifaa kwa taasisi zinazohusika kwa tafiti pamoja na usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupitishwa kwa Itifaki ya Cartagena masuala yanayohusu taratibu za uwajibikaji kisheria na fidia hayakupata muafaka wa nchi wanachama kutokana na kuwepo kwa msimamo tofauti kati ya nchi zilizoendelea na zinazoendelea. Nchi Zilizoendelea zilikuwa na msimamo kuwa kusiwepo na utaratibu wa pamoja wa Kimataifa wa kusimamia suala la uwajibikaji kisheria na fidia na badala yake kila nchi itumie sheria zake za ndani au misingi ya kisheria za Kimataifa zilizopo. Aidha, nchi

zinazoendelea ikiwemo Tanzania zilipendekeza kuwepo na mfumo wa Kimataifa kuhusu uwajibikaji kisheria na fidia endapo madhara yatatokea kutokana matumizi ya bioteknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kushindwa kufikia mwakafaka kuhusu suala hilo nchi wanachama zilikubaliana kuwa Ibara ya 27 ya Itifaki ya Cartagena ielekeze nchi wananchama kuendeleza majadiliano ya kuweka taratibu za Kitamaifa kuhusu uwajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya bioteknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa maelekezo ya Ibara ya 27 ya Itifaki hiyo mkutano wa kwanza wanchi wanachama uliofanyika jijini Kuala Lumpur mwaka 2004 ulianzisha majadiliano ambayo yalikalilika katika mkutano wa tano wanchi wanachama uliofanyika Jijini Nagoya Japan mwaka 2010. Kukamilika kwa majadiliano kulipitisha itifaki ya ziada ya Nagoya Kuala Lumpur inayoweza utaratibu wa Kimaitafa kwa wajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokana na matumizi ya bioteknolojia ya kisasa. Aidha, utekelezaji wa itifaki hii ya zaida umeanza rasmi tarehe 5 Machi, 2018 baada ya nchi 40 kuridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuridhia itifaki hii Tanzania itaimarisha ushirikiano wanchi wananchama katika kusimamia na kutekeleza masuala yanayohusu masuala ya uwajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya bioteknolojia ya kisasa hususan bidhaa au mazao ambayo yanatoka nje ya nchi. Vilevile, kuridhia itifaki hii kutaongeza upatikanaji wa fursa za kujenga uwezo wa wataalamu nchini katika kusimamia matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa. Aidha, utekelezaji wa itifaki hii utasimamiwa na sheria za Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 Sura ya 191 na Kanuni za Usimamizi wa Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa ya mwaka 2009. Pia kwa sasa sheria na kanuni hizo hazihitaji kufanyiwa marekebisho.



Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo nchi haitaridhia Itifaki hii itakuwa vigumu kutumia utaratibu huu wa uwajibishaji kisheria na kupata fidia kutoka kwa makampuni, wafanyabiashara ambao bidhaa zao na mazao yatakanayo na bioteknolojia ya kisasa yanaweza kuleta madhara kwa afya za binadamu na mazingira hapa nchini. Madhara hayo ni pamoja na uharibifu wa viumbe ambavyo havikukusudiwa, uharibifu wa bioanuai na uoto wa asili, uchavushaji wa mazao yasiyohusika. Ongezeko la mzio yaani *allergy*, usugu wa baadhi ya dawa kujitokeza kwa magugu sugu na kuibuka kwa visumbufu sugu vya mazao. Vilevile nchi yetu itakosa fursa ya kujenga uwezo wa kitaalamu na kisheria katika kusimamia matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo hayo vipengele muhimu ya itifaki hii ni pamoja na vifuaavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 1 Lengo la Itifaki. Ibara hii inahusu lengo la itifaki hii ambayo ni kuchangia juhudi za kuhifadhi mazingira na matumizi endelevu ya bioanuai kwa kutambua madhara yanayoweza kutokea katika afya za binadamu kutokana na matumizi ya mazao au bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki kwa njia ya bioteknolojia ya kisasa. Hivyo itifaki hii imeweka taratibu za Kimataifa za kusimamia masuala ya uwajibikaji kisheria na fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 2 Ibara ya 3 Mawanda ya Itifaki. Ibara hii inahusu utaratibu wa uwajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya mazao au bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao au bidhaa zifuatazo zinahusika na ibara hii; mazao au bidhaa zinazoweza kutumiwa katika chakula cha binadamu au mifugo ama kutumika viwandani na mazao au bidhaa zinazoweza kutumika katika utafiti. Ibara hii pia inahusu usimamizi wa mazao au bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya *ki-genetic* ambazo zinaweza kuingia nchini kutoka nchi nyingine bila

kukusudiwa, mfano uchavushaji wa mimea (*pollination*) kwa njia ya upepo au wadudu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara hii inahusu pia mazao au bidhaa zinazoweza kuingizwa nchini kinyume na sheria za nchi. Aidha, itifaki hii itatumika kwa nchi wanachama tu na endapo kutatokea madhara yatokanayo na matumizi ya mazao au bidhaa zitokanazo na bioteknolojia ya kisasa zinazozalishwa hapa nchini uwajibishaji kisheria na fidia utafuata sheria za nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 4, Kisababishi cha Madhara. Ibara hii inaelekeza kutumia sheria za nchi husika kuainisha chanzo cha madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya mazao au bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya *ki-genetic* kwa kutumia *Bioteknolojia* ya kisasa. Na kwa hili lina manufaa kwa nchi yetu kwani kutumia sheria za kimataifa kuainisha chanzo cha madhara hayo kunaweza kusababisha kushindwa kutoa haki stahiki kulingana na mazingira ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 5, ni Hatua za Kukabiliana na madhara. Ibara hii inahusu hatua za kuchukua na kukabiliana na madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya mazao au bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya *ki-genetic* zitakazochukuliwa kwa mujibu wa sheria ya nchi husika. Gharama za kukabiliana na madhara hayo zitakuwa juu ya kampuni, kiwanda, au mtu yeyote aliyesababisha madhara hayo. Takwa hili la itifaki lina manufaa kwa nchi yetu kwani kutumia sheria za kimataifa kuainisha hatua zakukabiliana na mdahara hayo kunaweza kusababisha kushindwa kutoa haki kwa watakapoathirika na matumizi ya mazao au bidhaa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 12, Utekelezaji na Uhusiano wa Mifumo ya uwajibishaji. Ibara hii inaelekeza nchi wanachama kuweka mifumo ya kisheria ya uwajibishaji na fidia kwa madhara ambayo yanaweza kutokea kutokana na matumizi ya mazao au bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya *ki-genetic* kwa kutumia njia ya *Bioteknolojia* ya kisasa.

Mifumo iliyopo ni ya aina tatu; mfumo wa kwanza ni kumuwajibisha mmiliki au msambazaji wa *Bioteknolojia* ya kisasa kwa madhara yanayoweza kutokea kwa mtumiaji wa mazao au bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya ki-*genetic* bila kujali kama mmiliki alikuwa na lengo la kumdhuru mtumiaji (*Strictly Liability*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfumo wa pili unahusisha kumuwajibisha aliyesababisha madhara baada ya mtumiaji wa mazao au bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya ki-*genetic* kudhibitisha kudhurika kutokana na bidhaa hizo (*Fault Based Liability*) na Mfumo wa tatu ni mfumo wa uwajibishaji mseto (*Strict Liability* na *Fault Based Liability*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania suala la uwajibikaji, sheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya mazao au bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya ki-*genetic* limezingatiwa katika Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, Sura ya 191 hata kabla ya kupitishwa kwa itifaki hii na katika kanuni za matumizi salama za *Bioteknolojia* ya kisasa ya mwaka 2009. Kanuni hii imeweka mfumo wa *strict liability* katika uwajibishaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya mazao au bidhaa hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza kanuni hii baadhi ya wadau walikuwa na hoja kuwa, kanuni hii inaathiri shughuli za utafiti kutokana na mfumo wa *strict liability*. Kuwakosesha fursa watafiti wa ndani ya nchi kushiriki na wadau kutoka nje ya nchi, hususan makampuni yanayojihusisha na shughuli ya utafiti wa masuala ya *Bioteknolojia* ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kuona umuhimu wa masuala ya utafiti katika eneo hili kanuni za matumizi ya salama za *Bioteknolojia* ya kisasa za mwaka 2009 zilirekebisha mwaka 2015 kwa kuondoa mfumo wa *strict liability* katika shughuli za utafiti na kuweka mfumo wa *fault based liability*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 16, inaelezea Uhusiano Baina ya Mikataba na Itifaki ya Katagena. Ibara hii inaeleza uhusiano uliopo kati ya itifaki hii ya mikataba ya hifadhi ya *bioanuai* na Itifaki ya Katagena katika kusimamia hifadhi ya mazingira na matumizi endelevu ya bioanuai. Itifaki ya ziada ya Nagoya - Kuala Lumpur inatekeleza Ibara ya 27 ya Itifaki ya Katagena na utekelezaji wa itifaki hii hauathiri wajibu na majukumu ya nchi wanachama, Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai ya wa Itifaki ya Katagena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 20, inahusu Uhuru wa Kujitoa. Nchi mwanachama ina uhuru wa kujitoa katika itifaki ya ziada baada ya miaka miwili tangu kuanza kutekelezwa kwake. Vilevile nchi ikijitoa katika Itifaki ya Katagena itahesabika kuwa imejitoa pia, kwenye itifaki hii ya ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla kuridhia kwa itifaki hii kutasaidia kuimarisha uhifadhi wa mazingira, kulinda afya za binadamu na wanyama dhidi ya madhara yatokanayo na matumizi ya *Bioteknolojia* ya kisasa. Matokeo mengine mahususi ni pamoja na:-

(i) Kurahisisha uwajibishaji kisheria na upatikanaji wa fidia kutokana na makampuni au wafanyabiashara wa nchi wanachama wa itifaki hii ambao wameingiza mazao au bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya ki-*genetic* na matumizi yake kuleta madhara kwa afya ya binadamu na mazingira hapa nchini;

(ii) Kuimarika kwa ushirikiano baina ya Tanzania na nchi nyingine wanachama wa itifaki hii katika kusimamia uwajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya mazao au bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya ki-*genetic* kwa kutumia njia ya ki-*Bioteknolojia* ya kisasa;

(iii) Kukuza uelewa wa wataalam wa ndani wakiwemo Wanasheria katika kusimamia masuala ya uwajibikaji kisheria

na fidia kwa madhara yatokanayo na matumizi ya *Bioteknolojia* au bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya ki-*genetic*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itifaki hii inaweza kuathiri uwekezaji katika *Bioteknolojia* ya kisasa kutoka nje ya nchi, hususan makampuni au wafanyabisahara kwa kuhofia kuwa, utaratibu unaopendekezwa unaweza kuwa na gharama kubwa kwao iwapo madhara ya matumizi ya bidhaa hizo yatajitokeza kwa mazingira na afya ya binadamu na wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, uwekezaji ambao hauzingatii usalama wa afya na mazingira unaweza kuwa na hasara kubwa kuliko faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili itifaki hii iweze kutekelezwa ni lazima nchi zilizosaini itifaki ziridhie. Utaratibu wa kuridhia itifaki hii umeoneshwa katika Ibara ya 18 ya itifaki yenyewe ambayo inazitaka nchi hizo kuridhia itifaki hii na kuwasilisha hati ya kuridhia kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ambaye ana jukumu la kupokea na kuhifadhi hati hizo.

Aidha, itifaki hii imeanza rasmi kutekelezwa tarehe 05 Machi, 2018 baada ya nchi ya 40 kuridhia itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya sasa naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki hii kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, Tanzania ni nchi mwanachama wa Itifaki ya Katagena inayohusu matumizi salama ya *Bioteknolojia* ya kisasa ya mwaka 2000 na lengo kuu la itifaki hiyo ni kusimamia matumizi salama ya *Bioteknolojia* ya kisasa miongoni mwa nchi wanachama.

Na kwa kuwa, Tanzania iliridhia itifaki hii mwaka 2003.

Na kwa kuwa, wakati wa kupitisha Itifaki ya Katagena nchi wanachama zilikubaliana kuendeleza majadiliano kuhusu utaratibu wa kimataifa wa uwajibikaji kisheria na fidia

kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya *Bioteknolojia* ya kisasa kuweka Ibara ya 27 iliyoelekeza kuendelezwa kwa majadiliano ya suala hilo.

Na kwa kuwa, majadiliano hayo yalikamilika katika mkutano wa tano wa nchi wanachama wa Itifaki ya Katagena wa mwaka 2010 uliofanyika Nagoya, Japan na kupitishwa rasmi itifaki ya ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur inayoweza utaratibu wa kimataifa wa uwajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya *Bioteknolojia* ya kisasa miongoni mwa nchi wanachama ambayo ilianza kutekelezwa rasmi tarehe 05 Machi, 2018 hadi sasa jumla ya nchi 45 zimeridhia itifaki hii.

Na kwa kuwa, kwa kuridhia Itifaki ya Ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur Tanzania itaimarisha usalama wa afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya *Bioteknolojia* ya kisasa hususan kwa bidhaa za mazao yanayotoka nje ya nchi.

Na kwa kuwa, kwa kuridhia itifaki hii kutaongeza upatikanaji wa fursa ya kujenga uwezo wa wataalam nchini katika kusimamia matumizi salama ya *Bioteknolojia* ya kisasa katika nyanja za kisheria, kisayansi na kiteknolojia.

Hivyo basi, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na itifaki hii kwa Tanzania na kwa wanachama wengine. Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Sita na sasa liazimie kuridhia kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Itifaki ya Ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur kuhusu uwajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya Bioteknolojia ya kisasa katika kuetekeleza itifaki ya Cartagena (*Nagoya – Kuala Lumpur Supplementary Protocol on Liability and Redress to The Katagena Protocol on Biosafety*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, ahsante. Sasa namuita Mwenyekiti Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS - K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Ziada ya Nagoya - Kuala Lumpur ya Uwajibikaji wa Kisheria na Fidha kwa Madhara Yanayoweza Kutokea Kutokana na Matumizi ya *Bioteknolojia* ya Kisasa Katika Kutekeleza Itifaki ya Cartagena. (*Nagoya - Kuala Lumpur supplementary Protocol on Liability and Redress to The Cartagena Protocol Biosafety*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b). Kanuni ya Kudumu ya Bunge ya Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira Kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Ziada ya Nagoya, Kuala Lumpur inayolenga kuweka utaratibu wa uwajibikaji kisheria na fidha kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya *Bioteknolojia* ya kisasa katika kutekeleza Itifaki ya Cartagena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Masharti ya Fasili ya 6(b), Kifungu cha 53, ikisomwa pamoja na Fasili ya 1(b) ya Kifungu cha 7 cha Nyongeza ya 8 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira inalo jukumu la kushughulikia mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa hoja ya Serikali kuhusu Bunge kuridhia Itifaki ya Ziada ya Nagoya - Kuala Lumpur ilileta kwenye Kamati ya

Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa mujibu wa kanuni ya 53(3) ya Kanuni za Bunge. Kamati ilijadili, kuichambua hoja hii na hatimaye kuja na maoni ya ushauri ambayo yamelenga kuboresha utekelezaji wa itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kushughulikia hoja hii kamati ilikutana katika Ofisi za Bunge, Dodoma ambapo ilitekeleza shughuli zifuatazo kwa ajili ya kuwezesha uchambuzi wa kina wa itifaki hii:-

(i) Semina ya Kuijengea Uelewa Kamati Juu ya Itifaki ya Ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur ambapo tarehe 01 Septemba, 2019 kamati ilikutana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na kupatiwa semina hii. Kupitia semina hii Kamati ilipata uelewa juu ya itifaki husika na kuwa katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii;

(ii) Kupokea maelezo ya Serikali ambayo yaliwasilishwa na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira siku ya tarehe 04 Septemba, 2019;

(iii) Kupokea maoni ya wadau. Kamati ilipokuwa inatekeleza jukumu lake kuhusiana na hoja hii ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117(9) kuhusu utaratibu wa Kamati wa kuwaalika wadau. Kamati inawashukuru sana wadau wote walioweza kushiriki kwa kuwa maoni yao yalisaidia kuboresha maoni ya kamati kuhusu itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni moja ya nchi mwanachama wa Itifaki kwa Hofadhi ya bioanuai (*the Conversation on Biological Diversity*) na tuliridhia mwaka 1996. Mkataba huo ulikuwa na malengo matatu ambayo ni kuhifadhi bioanuai, matumizi endelevu ya bioanuai na mgawanyo sahihi wa faida zinazotokana na bioanuai na matumizi yake katika kutekeleza mkataba huu ilizaliwa Itifaki ya Cartagena mwaka 2000 kwa lengo la kuhifadhi na kusimamia matumizi salama *Bioteknolojia* ya kisasa kwa lengo la kuleta matumizi endelevu ya *bio-anuai* Tanzania iliridhia itifaki ya Cartagena mwaka 2003.



Mheshimiwa Mwenyekiti, bada ya kupitisha Itifaki ya Cartagena mwaka 2003 masuala yaliyohusu taratibu za uwajibikaji kisheria na fidia hayakufikiwa muafaka kutokana na kuwepo kwa msimamo tofauti baina ya nchi wanachama, jambo lililosababisha kukubaliana majadiliano yaendeleo. Katika vikao vilivyofuata nchi wanachama walikubaliana kuunda kamati ndogo ya wataalamu wa masuala ya matumizi ya *Bioteknolojia* ya kisasa na Wanasheria. Matokeo ya kazi iliyofanywa na kamati hiyo yalohitimisha mjadala ambapo nchi wanachama walikubaliana kupitisha Itifaki ya Ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur Mwaka 2010 iliyoweka utaratibu wa kimataifa wa uwajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea katokana na matumizi ya *Bioteknolojia* ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Bioteknolojia* ya kisasa, *technology* ya uhandisi *gene modern Bioteknolojia*, *genetic engineering* ni nyenzo ya kisayansi inayoweza uhamishaji wa vinasaba kutoka kiumbe kimoja kwenda kiumbe kingine ili kukipatia kiumbe kingine sifa inayokusudiwa kwa lengo la kuboresha kiumbe hicho na kuongeza tija ya uzalishaji. Pamoja na faida nyingi za matumizi ya *Bioteknolojia* ya kisasa bado matumizi ya bidhaa zitokanazo na teknolojia hii yanaweza kuleta madhara katika afya za binadamu na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo, kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati ilizingatia mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika kufanyia kazi Hoja ya Serikali iliyo mezani leo. Kamati ilianguka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na baadhi ya sheria zinazohusiana moja kwa moja na maudhui ya itifaki iliyopendekezwa ambapo ilibaini kuwa, itifaki hii haikuwa inakinzana na Katiba wala sheria za nchi, bali ilikuwa inaongezea nguvu Sheria ya Taifa ya Mazingira katika kusimamia uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia, ilitafakari faida zipatikanazo kutokana na kuridhia itifaki hii ambazo ni;

(i) Kurahisisha uwajibikaji wa kisheria na upatikanaji wa fidia kutoka kwa makampuni, wafanyabiashara wa nchi wanachama wa itifaki hii ambao mazao au bidhaa zao zinafanyiwa mabadiliko ya ki-*genetic* kama matumizi yake yameleta madhara kwa afya au mazingira na;

(ii) Kuimarika kwa ushirikiano baina ya Tanzania na nchi nyingine wanachama wa itifaki hii katika kusimamia uwajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kwa matumizi ya mazao au bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya ki-*genetic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati iliangalia hasara ambazo zinaweza kupatikana kutokana na kutoridhia mkataba huu. Kamati ilifahamishwa hasara moja kubwa ambayo nchi inaweza kuipata kama haitaridhia ni kuwa itajinyima haki yake ya kufidiwa endapo madhara yanaweza yakapatikana yakadhihirika kuwa yametokana na matumizi ya bidhaa au mazao yaliyofanyiwa mabadiliko ya ki-*genetic*. Ni vyema Tanzania tuzingatie kuwa Tanzania inaruhusu uingizwaji wa bidhaa mbalimbali nchini kwa kuwa, kati ya bidhaa zinazolingia kuna baadhi yake zimefanyiwa mabadiliko ya ki-*genetic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijiridhisha pia, na maudhui ya itifaki husika. Ibara ya kwanza na mkataba imeweka wazi dhamira ya itifaki hii kuwa inalenga kuweka matumizi endelevu ya bioanuai kwa kutambua madhara ya afya ya binadamu kwa kuweka taratibu za kimataifa za kusimamia masuala ya uwajibikaji kisheria na fidia endapo yatapatikana madhara kutokana na matumizi ya bidhaa au mazao yaliyofanyiwa mabadiliko ya ki-*genetic*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nanukuu, *Article 1*; “*The objective of this Supplementary Protocol is to contribute to the conservation and sustainably use of biological diversity taking also into account risk to human health by providing international rules and procedure in the field of liability and redress relating to living modified organism,*” mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maudhui ya ibara hiyo Tanzania ikiridhia inajiweka katika nafasi ya kunufaika ukizingatia bidhaa na mzao yanayofanyiwa mabadiliko ya ki-*genetic* yanaendelea kuingia na kutumika hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Tanzania haijaruhusu matumizi ya bioteknolojia ya kisasa katika uzalishaji wa bidhaa yoyote kwa maana kuwa Tanzania hatuzalishi bidhaa wala mazao yatokanayo na teknolojia hiyo lakini kwa uhakika mazao na bidhaa zitokanazo na teknolojia hii zimeendelea kuingia nchini na tumeendelea kuzitumia. Hivyo basi, kuna haja ya nchi kuridhia Itifaki hii ili tuweze kulinda haki yetu pindi madhara yanapobainika. Pamoja na umuhimu wa kuridhia, yapo baadhi ya maeneo ambayo ni vyema nchi tukayaweka sawa kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Itifaki hii umeonyesha kuwa na uhusiano na ushirikiano wa moja kwa moja na sheria za nchi husika mfano Ibara ya 6(2) inataka sheria za nchi husika kufafanua *exemption* na *mitigation* kwa namnawanavyoona inafaa. Pia Ibara ya 8 inataka sheria ya nchi husika kuweka kiwango cha fidia kwa ajili ya madhara yaliyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali baada ya kuridhia Itifaki hii jipange kuzipitia na kuboresha sheria za nchi na kutunga sheria ambazo zitaenda sambamba na malengo ya Itifaki hii kwa kuhakikisha kama nchi tunanufaika na siyo kupoteza. Vilevile ili kuweza kutekeleza kikamilifu masharti ya Ibara hizo, Kamati inaona upo umuhimu kwa nchi wanachama kuangalia namna ya kuoanisha sheria, sera na programu zinazohusiana katika utekelezaji wa Itifaki hii kwa lengo la kuwa na manufaa linganifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamii bado ina uelewa mdogo juu ya matumizi, faida na madhara ya bioteknolojia ya kisasa. Ili kunufaika na Itifaki hii, Kamati inaishauri Serikali

kuweka jitihada za dhati kuhakikisha jamii inapatiwa uelewa juu ya uwepo wa bidhaa au mazao yanayofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki. Pia jamii iwekwe wazi kuwa pamoja na uzuri wa jambo hili bado uwezekano wa kupata madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa hizo. Vilevile jamii ijulishwe juu ya uwepo wa Itifaki hii na namna inavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki hii imeipa nchi Mwanachama nafasi kubwa ya kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Itifaki ndani ya nchi yake (utaalamu na teknolojia ya nchi katika kupima na kubaini madhara). Kamati inaona uwezo wa nchi katika kutekeleza Itifaki hii bado hautoshelezi. Kamati inaishauri Serikali kuzijengea uwezo taasisi zake ambazo zitaenda kuratibu utekelezaji wa Itifaki hii kwa kuwa ndiyo zitategemewa kusimamia na kuhakikisha mhanga anapata haki zake pindi itakapotokea tukio lolote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Nimshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kuwashukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Mussa Ramadhan Sima, Makatibu Wakuu pamoja na wataalamu wote wa ofisi hiyo muhimu kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kujadili Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kuipitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni yao juu ya Azimio hili mbele ya Bunge lako Tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapo chini na kwa rufusa yako naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini si kwa umuhimu, nawashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake.

Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati, Ndugu Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi, Sehemu ya Fedha na Uchumi, Ndugu Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati, Bi. Zainab Mkamba na Bi. Mwajuma Ramadhani na Msaidizi wa Kamati, Bi. Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio hili.

**MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA,  
BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU AZIMIO LA BUNGE  
KURIDHIA ITIFAKI YA ZIADA YA NAGOYA – KUALA LUMPUR LA  
UWAJIBIKAJI KISHERIA NA FIDIA KWA MADHARA  
YANAYOWEZA KUTOKEA KUTOKANA NA MATUMIZI YA  
BIOTEKNOLOJIA YA KISASA KATIKA KUTEKELEZA ITIFAKI YA  
CARTAGENA - KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

*(Nagoya – Kuala Lumpur Supplementary Protocol on  
Liability and Redress to the Cartagena Protocol on  
Biosafety) Kama yalivyowasilishwa Mezani*

---

## **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b), ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Bunge Kuridhia Itifaki ya Ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur inayolenga kuweka utaratibu wa uwajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya Bioteknolojia ya kisasa katika kutekeleza itifaki ya Cartagena *(Nagoya – Kuala Lumpur Supplementary Protocol on Liability and Redress to the Cartagena Protocol on Biosafety)*.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya fasili ya 6(b), Kifungu cha 53 ikisomwa pamoja na fasili ya 1(b) ya Kifungu cha 7, cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira inalo jukumu la kushughulikia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Hoja ya Serikali kuhusu Bunge kuridhia Itifaki ya Ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur ililetwa kwenye Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (3) ya Kanuni za Bunge. Kamati ilijadili na kuichambua hoja hii na hatimaye kuja na maoni na ushauri ambao umelenga kuboresha utekelezaji wa Itifaki hii.

## 2.0 NAMNA KAMATI ILIVYOSHUGHULIKIA HOJA HII

**Mheshimiwa Spika**, katika kushughulikia hoja hii Kamati ilikutana katika Ofisi za Bunge Dodoma ambapo ilitekeleza shughuli zifuatazo kwa ajili ya kuwezesha uchambuzi wa kina wa Itifaki hii:-

i) Semina ya kuijengea uelewa Kamati juu ya Itifaki ya Ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur, ambapo tarehe 1 September, 2019 Kamati ilikutana na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira na kupatiwa semina hii. Kupitia semina hii Kamati ilipata uelewa juu ya itifaki husika na kuwa katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii.

ii) Kupokea Maelezo ya Serikali ambayo yaliwasilishwa na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira siku ya tarehe 04 September, 2019. Kikao hiki kilitoa fursa kwa Ofisi hiyo kufafanua kwa kina madhumuni ya Itifaki hii kwa lengo la kuishawishi Kamati na hatimaye kulishawishi Bunge kuridhia.

iii) Kupokea maoni ya wadau, Kamati ilipokuwa inatekeleza jukumu lake kuhusiana na hoja hii, ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117 (9) kuhusu utaratibu wa Kamati

kuwaalika wadau. Kamati inawashukuru sana wadau wote walioweza kushiriki kwa kuwa maoni yao yalisaidia kuboresha maoni ya Kamati kuhusu Itifaki hii.

### 3.0 CHIMBUKO LA MKATABA WA MAREKEBISHO

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni moja ya nchi Mwanachama wa Mkataba wa hifadhi ya Bioanuai (*The Convention on Biological Diversity*) na tuliuridhia mwaka 1996. Mkataba huo ulikuwa na Malengo matatu ambayo ni kuhifadhi bioanuai, matumizi endelevu ya bioanuai na mgawanyo sahihi wa faida zinazotokana na matumizi yake. Katika kutekeleza Mkataba huu ilizaliwa Itifaki ya Cartagena mwaka 2000 kwa lengo la kudhibiti na kusimamia matumizi salama ya Bioteknolojia ya kisasa kwa lengo la kuleta matumizi endelevu ya bioanuai. Tanzania iliridhia itifaki Cartagena mnamo mwaka 2003.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupitisha Itifaki ya Cartagena ya mwaka 2003 masuala yanayohusu taratibu za uwajibikaji kisheria na fidia hayakufikiwa muafaka kutokana na kuwepo kwa misimamo tofauti baina ya nchi wanachama jambo lililopelekea kukubaliana majadiliano uendeleo.

Katika vikao vilivyofuata Nchi wanachama walikubaliana kuunda Kamati ndogo ya wataalamu wa masuala ya matumizi ya bioteknolojia ya kisasa na wanasheria. Matokeo ya kazi iliyofanywa na Kamati hiyo yalithimisha mjadala ambapo nchi wanachama walikubaliana kupitisha Itifaki ya Ziada ya Nagoya - Kuala Lumpur ya Mwaka 2010 inayoweka utaratibu wa kimataifa wa uwajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya bioteknolojia ya kisasa.

**Mheshimiwa Spika**, Bioteknolojia ya kisasa/teknolojia ya Uhandisi Jeni (Modern Biotechnology/Genetic Engineering) ni nyenzo ya kisayansi inayoweza uhamishaji wa vinasaba kutoka kiumbe kimoja kwenda kiumbe kingine ili kukipatia kiumbe kingine sifa inayokusudiwa kwa lengo la kuboresha kiumbe hicho na kuongeza tija na uzalishaji. Pamoja na faida nyingi za matumizi ya bioteknolojia ya kisasa bado matumizi

ya bidhaa zitokanazo na teknolojia hii yanaweza kuleta madhara katika afya ya binadamu na mazingira.

#### 4.0 MAMBO YA MSINGI YALIYOZINGATIWA NA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati ilizingatia mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika kuifanyia kazi hoja ya Serikali iliyo mezani leo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati iliangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na baadhi ya Sheria za nchi zinazohusiana moja kwa moja na maudhui ya Itifaki inaopendekezwa ambapo ilibainika kuwa Itifaki hii haikuwa ina kinzana na Katiba wala Sheria za nchi bali ilikuwa inaiongezea nguvu Sheria ya Taifa ya Mazingira katika kusimamia uhifadhi wa mazingira.

Kamati pia ilitafakari faida zipatikanao kutokana na kuridhia Itifaki hii ambazo ni pamoja na;-

i) Kurahisisha uwajibikaji kisheria na upatikanaji wa fidia kutoka kwa makampuni/wafanyabiashara wa nchi wanachama wa Itifaki hii ambao mazao au bidhaa zao zilizofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki matumizi yake yameleta madhara kwa afya au mazingira; na

ii) Kuimarika kwa ushirikiano baina ya Tanzania na nchi nyingie wanachama wa Itifaki hii katika kusimamia uwajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kwa matumizi ya mazao au bidhaa zilizofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki.

Vilevile Kamati iliangalia hasara ambazo zinaweza kupatikana kutokuridhia Mkataba huu. Kamati ilifahamishwa hasara moja kubwa ambayo nchi inaweza kuipata kama haitaridhia ni kuwa itajinyima haki yake ya kufidiwa endapo madhara yanaweza kupatikana na yakadhihirika kuwa yametokana na matumizi ya bidhaa au mazao yaliyofanyiwa



mabadiliko ya kijenetiki. Tuzingatie kuwa Tanzania inaruhusu uingizwaji wa bidhaa mbalimbali nchini na kuwa kati ya bidhaa zinazolingia kuna baadhi yake zimefanyiwa mabadiliko ya kijenetiki.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijiridhisha pia na maudhui ya Itifaki husika ambapo **Ibara 1** ya Mkataba imeweka wazi dhamira ya Itifaki hii kuwa inalenga kuweka matumizi endelevu ya bioanuai kwa kutambua madhara kwa afya ya binadamu kwa kuweka taratibu za kimataifa za kusimamia masuala ya uwajibikaji kisheria na fidia endepo yatapatikana madhara kutokana na matumizi ya bidhaa au mazao yaliyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki.

**Nanukuu: Article 1** *“The objective of this Supplementary Protocol is to contribute to the conservation and sustainable use of biological diversity, taking also into account risk to human health, by providing international rules and procedures in the field of liability and redress relating to living modified organisms”* **Mwisho wa kunukuu.**

Kwa kuzingatia maudhui ya Ibara hiyo Tanzania ikiridhia inajiweka katika nafasi ya kunufaika ukizingatia bidhaa na mazao yaliyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki vinaendelea kuingia na kutumika nchini.

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania haijaruhusu matumizi ya bioteknolojia ya kisasa katika uzalishaji wa aina yeyote, kwa maana kuwa Tanzania hatuzalishi bidhaa wala mazao yatokanayo na teknolojia hiyo, lakini kwa uhakika mazao na bidhaa zitokanazo na teknolojia hii zimeendelea kuingia nchini na tumeendelea kuzitumia. Hivyo basi kuna haja ya nchi kuridhia itifaki hii ili tuweze kulinda haki yetu pindi madhara yanapobainika. Pamoja na umuhimu wa kuridhia, yapo baadhi ya maeneo ambayo ni vyema Nchi tukayaweka sawa kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa mkataba huu.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa itifaki hii umeonyesha kuwa na uhusiano na ushirikiano wa moja kwa moja na sheria za nchi husika. Mfano **Ibara ya 6 (2)** inaitaka Sheria za nchi husika kufafanua *exemption na mitigation* kwa namna wanavyoona inafaa, lakini pia **Ibara ya 8** inaitaka Sheria ya nchi husika kuweka kiwango cha fidia kwa ajili ya madhara yaliyopatikana. Kamati inaishauri Serikali baada ya Kuridhia Itifaki hii ijipange kuzipitia na kuboresha sheria za nchi au kutunga Sheria ambazo zitaenda sambamba na malengo ya Itifaki hii kwa kuhakikisha kama nchi tunanufaika na si kupoteza.

Vilevile, ili kuweza kutekeleza kikamilifu masharti ya Ibara hizo, Kamati inaona upo umuhimu kwa nchi wanachama kuangalia namna ya kuoanisha Sheria, sera na program zinazohusika katika utekelezaji wa Itifaki hii kwa lengo la kuwa na manufaa linganifu.

**Mheshimiwa Spika**, jamii bado ina uelewa mdogo juu ya matumizi, faida na madhara ya Bioteknolojia ya kisasa, kwa lengo la kunufaika na Itifaki hii Kamati inaishauri Serikali kuweka jitihada za dhati kuhakikisha jamii inapatiwa uelewa juu ya uwepo wa bidhaa au mazao yaliyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki. Pia jamii iwekwe wazi kuwa pamoja na uzuri wa jambo hili bado kuna uwezekano wa kupata madhara yatokanayo na matumizi ya bidhaa hizo. Vilevile jamii ijulishwe juu ya uwepo wa Itifaki hii na namna inavyofanya kazi.

**Mheshimiwa Spika**, Itifaki hii imeipa nchi Mwanachama nafasi kubwa ya kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Itifaki ndani ya nchi yake (utaalamu na teknolojia ya nchi katika kupima na kubaini madhara). Kamati inaona uwezo wa nchi katika kutekeleza itifaki hii bado hautoshelezi, Kamati inaishauri Serikali kuzijengea uwezo taasisi zake ambazo zitaenda kuratibu utekelezaji wa Itifaki hii kwa kuwa ndio zitategemewa kusimamia na kuhakikisha mhanga anapata haki zake pindi itakapotokea tukio lolote.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na kwa kunipa ruhusa ya kuwasilisha

maoni haya ya Kamati. Nimshukuru pia Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais-Muungano na Mazingira Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb), Naibu Waziri wake Mhe. Musa Ramadhani Sima (Mb), Makatibu Wakuu, pamoja na wataalamu wote wa Ofisi hiyo muhimu kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kujadili Azimio hili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano walioutoa wakati wa kupitia kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni yao juu ya Azimio hili mbele ya Bunge hili tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapo chini na kwa ruhusa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge: -

- |                                            |              |
|--------------------------------------------|--------------|
| 1. Mhe. Suleiman Ahmed Sadiq, Mb           | Mwenyekiti   |
| 2. Mhe. Kanal (Mst.) Masoud Ali Khamis, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. Mhe. Gimbi Dotto Masaba, Mb             | Mjumbe       |
| 4. Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb          | Mjumbe       |
| 5. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb          | Mjumbe       |
| 6. Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb          | Mjumbe       |
| 7. Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb          | Mjumbe       |
| 8. Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb         | Mjumbe       |
| 9. Mhe. Musa Rashid Ntimizi, Mb            | Mjumbe       |
| 10. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb            | Mjumbe       |
| 11. Mhe. Khamis Ali Vuai, Mb               | Mjumbe       |
| 12. Mhe. Zainabu Mndolwa Amiri, Mb         | Mjumbe       |
| 13. Mhe. Machano Othman Said, Mb           | Mjumbe       |
| 14. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb   | Mjumbe       |
| 15. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb      | Mjumbe       |
| 16. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb          | Mjumbe       |
| 17. Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb            | Mjumbe       |
| 18. Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb             | Mjumbe       |
| 19. Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb        | Mjumbe       |
| 20. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb       | Mjumbe       |

- |                                 |        |
|---------------------------------|--------|
| 21. Mhe. David Cecil Mwambe, Mb | Mjumbe |
| 22. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb  | Mjumbe |
| 23. Mhe. Jafar Sanya Jussa, Mb  | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bw. Athumani Hussein; Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bw. Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bi. Zainabu Mkamba na Bi. Mwajuma Ramadhani na Msaidizi wa Kamati Bi Paulina Mavunde kwa kuratibu shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio.

Suleiman Ahmed Sadiq, (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA  
MAZINGIRA**

11 Septemba, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) atatoa maoni ya Upinzani kuhusu Azimio hilo, Mheshimiwa Lathifah.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa ruhusa yako, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote tuweze kuwakumbuka wale wote waliopoteza maisha katika shambulio lililotokea nchini Marekani tarehe kama ya leo Septemba 11, miaka 18 iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kambi Rasmi Bungeni kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Nyongeza ya Nagoya – Kuala Lumpur Kuhusu Uwajibikaji Kisheria na Fidia Kutokana na Madhara nanayoweza Kutokea Kutokana na

Matumizi na Bioteknolojia ya Kisasa (*Nagoya – Kuala Lumpur Supplementary Protocol on Liability and Redress to the Cartagena Protocol on Biosafety*) yanayotolewa kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Bunge, Kanuni ya 53(6)(c).

Mheshimiwa Mwenyekiti, bioteknolojia ya kisasa inaweza kuleta manufaa mengi lakini kuna hofu kwamba inaweza kuwa na madhara makubwa kwa bioanuai na kwa afya ya binadamu. Kwa sababu hiyo, lengo la kuanzishwa kwa Itifaki ya Nyongeza ya Nagoya, Kuala Lumpur lilikuwa ni kuendeleza uhifadhi wa mazingira na kufanya matumizi endelevu ya bioanuai yaani mtawanyiko, muingiliano na kutegemeana baina ya viumbe hai na mazingira ili kukabiliana na madhara yatokanayo na matumizi ya bioteknolojia

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa bioanuai ni suala la kimataifa; na kwa kuwa athari zitokanazo na uharibifu wa bioanuai zinavuka mipaka ya nchi moja kwenda nyingine ilionekana ni jambo muhimu na lenye afya katika utunzaji wa bioanuai yenyewe pamoja na mazingira kwa ujumla wake kuweka kanuni na taratibu za kimataifa na hasa katika dhana ya uwajibikaji kisheria na pia kulipia fidia ikiwa kutatokea madhara yanayohusiana na viumbe hai vilivyofanyiwa maboresho ya vinasaba (*living modified organisms*). Ni katika maudhi hayo ambapo kifungu cha 3 cha Itifaki hii kinaeleza bayana kwamba Itifaki ya Nyongeza itahusu madhara yatokanayo na viumbe hai vilivyopandikizwa vinasaba tofauti kwa lengo la kuviboresha ambavyo katika kuishi kwake vinakuwa mipaka ya nchi moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Itifaki hii madhara yanayotokana na matumizi ya bioteknolojia inayopelekea uharibifu wa mazingira na bioanuai yatahesabiwa kuwa ni madhara ikiwa yatakuwa yanaonekana, yanapimika na yenye athari kwa afya ya binadamu. Aidha, Itifaki inaelekeza kwamba ili mtu aweze kuwajibika na au kulipa fidia ni lazima mlalamikaji aweze

kuthibitisha kuwa madhara hayo yanauhusiano wa moja kwa moja na viumbe vilivyofanyiwa maboresho na vinasaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya msingi ya kuzingatia kabla ya kuridhia Itifaki. Pamoja na ukweli kwamba Itifaki hii inaonekana kuwa na nia njema ya kupambana na kuzuia madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya bioteknolojia kwa kuweka kanuni za Kimataifa za uwajibikaji kisheria na kulipia faida kwa madhara ya namna hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa Serikali na Bunge kuzingatia mambo yafuatayo kabla ya kuridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa nchi katika sayansi ya na teknolojia. Kama ilivyoelezwa hapo awali, Itifaki hii katika mawanda mapana inahusu kukabiliana na madhara yatokanayo na matumizi ya bioteknolojia na hususan upandikizaji wa vinasaba katika viumbe hai. Hili ni jambo linalohitaji uwezo mkubwa wa kisayansi na kiteknolojia. Tofauti na nchi zilizoendelea nchi ambazo ziko nyuma kimaendeleo ikiwemo Tanzania, bado hazina uwezo mkubwa katika sayansi na teknolojia kuweza kufanya tafiti na gunduzi za kisayansi kama vile *genetic engineering* au masuala yanayofanana na hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Itifaki hii ili mlalamikaji aweze kulipwa fidia kutokana na madhara ya matumizi ya bioteknolojia ni lazima aweze kuthibitisha kwamba madhara hayo yanatokana na viumbe vilivyofanyiwa maboresho ya vinasaba. Kwa maneno mengine ni kwamba nchi itaathirika kutokana na matumizi ya bioteknolojia kutoka nje. Ni lazima tuwe na maabara madhubuti na watafiti waliobobea katika sayansi ili kuweza kugundua kama madhara tuliyopata yanauhusiano wa moja kwa moja na viumbe vilivyopandikizwa vinasaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba jambo hili litakuwa gumu sana hasa kwa nchi yetu kutokana na Serikali kutoipa kipaumbele Tume yetu ya Sayansi na Teknolojia. Kwa mfano,

kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/2017 - 2020/2021, Serikali ilijiwekea kiwango cha kutenga asilimia moja ya pato ghafi la Taifa (*GDP*) kwa ajili ya shughuli za sayansi, teknolojia na ugunduzi. Hata hivyo, Serikali haijawahi kutenga kiasi hicho tangu imejiwekea utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pato ghafi la Taifa kwa sasa ni dola za Kimarekani bilioni 52.09 ambazo ni sawa na shilingi trilioni 119.807. Hii ina maana kwamba ikiwa Serikali ingefuata utaratibu iliyojiwekea wa kutenga asilimia moja ya pato ghafi la Taifa ingetakiwa kutenga shilingi trilioni 1.19. Fedha iliyotengwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*) kwa ajili ya tafiti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni shilingi bilioni 7.57 sawa na asilimia 0.00632. Hiki ni kiwango kidogo kuliko vyote tangu Serikali hii ya Awamu ya Tano iingie madarakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa angalizo kwa Serikali kuwa makini katika suala hili la tafiti za kisayansi kwa kuwa kuna hatari ya Tanzania kuendelea kuwa watumwa wa teknolojia ya nje jambo ambalo litazidi kuweka Watanzania mbali katika kushiriki kujenga uchumi wa nchi yao. Mwenendo huu wa kuendelea kutenga fedha kidogo kwa ajili ya tafiti hauna afya hata kidogo kwa mustakabali wa sayansi, teknolojia na ugunduzi katika Taifa. Hata ndoto za Serikali za kujenga uchumi wa viwanda haziwezi kufikiwa ikiwa hakuna uwekezaji wa kutosha katika tafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa tafiti katika kukuza na kuendeleza sayansi na teknolojia, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kupitia CHADEMA imeeleza bayana katika Sera yake ya Elimu, Sura ya 6.1 inayohusu mfumo wa ugunduzi na ubunifu juu ya umuhimu wa tafiti. Sera hiyo inaeleza kama ifuatavyo: "CHADEMA inaamini kwamba msingi wa ugunduzi na ubunifu katika elimu unajengwa katika tafiti za kisayansi. Kwa hiyo, kwa kushirikiana na sekta binafsi, CHADEMA itawekeza kikamilifu katika elimu

ya utafiti kuanzia elimu ya awali ili kumjengea mtoto uwezo wa ubunifu". (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa wadau katika uchambuzi wa Itifaki. Kumekuwa na desturi mbaya ya kupitisha Maazimio ya Kuridhia Itifaki na Mikataba mbalimbali ya Kimataifa kwa ghafla ghafla bila kuwashirikisha kikamilifu wadau katika kufanya uchambuzi wa kina wa faida na au madhara ya Itifaki au Mikataba husika na wakati mwingine bila hata kujali kama akidi ya Bunge imetimia au la katika kupitisha uamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala gumu na lenye uhitaji na utaalamu wa kisayansi kama hili linalohusu matumizi ya bioteknolojia na madhara yake katika bioanuai, Serikali iwe inafanya uchambuzi wa kina juu ya athari za kuridhia Itifaki hii na kuwapatia Waheshimiwa Wabunge semina elimishi kwa Wabunge wote ili kuweza kulishawishi Bunge kuridhia jambo ambalo wanauielewa nalo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, haina hakika kama uchambuzi huo umefanyika na kama Wabunge wameshirikishwa kwa kiwango cha kutosha. Jambo hilo ni hatari kwa kuwa Bunge linaweza kuridhia jambo ambalo litakuwa na madhara baadaye kwa nchi yetu kutokana na kukosa uelewa kuhusu jambo lenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ambayo itifaki hii haitahusika yaani *exemptions*. Kifungu cha 16 cha Itifaki hii kinasema kwamba, naomba kunukuu: "*Parties may provide, in their domestic law, for the following exemptions:*

- a. *Act of God or force majeure; and*
- b. *Act of war or civil unrest.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba masharti ya Itifaki hii hayatatumika katika nyakati za vita au machafuko ya kisiasa na nyakati za majanga ya asili. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kuwa makini sana na kifungu hiki kwa kuwa kinatoa kinga ya kutowajibika kisheria au kulipa fidia kwa madhara



yatokanayo na matumizi ya bioteknolojia nyakati za vita au machafuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizoendelea kisayansi na kiteknolojia ambazo zimefikia hatua ya kutengeneza silaha za kibaolojia (*biological weapons*) zinaweza kutumia mwanya huu kupenyeza silaha za kibiolojia ambazo kwa asili ni za maangamizi makubwa (*weapons of mass destruction*) na wakakwepa kuwajibika kisheria na kulipa fidia kwa kisingizio kuwa ni wakati wa vita au machafuko. Katika mazingira kama hayo, nchi zilizo nyuma kimaendeleo zitabaki kuwa wahanga wa matukio kama hayo (*victims of circumstance*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya kuwa na stara (*reservation*) katika baadhi ya vifungu. Katika kifungu cha 19 cha Itifaki hii ambayo inazitaka nchi wanachama kuridhia mkataba bila stara (*no reservation may be made to this Supplementary Protocol*) ni wazi kuwa ibara hii ni ya kuangaliwa kwa mapana zaidi.

**MWENYEKITI:** Kengele ya kwanza hiyo.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tunatambua katika ulimwengu wa sasa vita kubwa inayopiganiwa kitaalamu na kisayansi ni vita ya kibaiolojia (*biological weapons*). Yapo magonjwa mengi ambayo yamezua mijadala mikubwa duniani ambapo wengi wa wataalam wanaamini ni magonjwa ya kutengenezwa ambayo kitaalamu yanatokana na *genetic modification*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, endapo nchi tutaridhia vifungu ambavyo tayari vinaonyesha walakini kama ilivyo katika Ibara ya 6 ya Itifaki hii, tunaweza kujikuta katika hatari kubwa. Ni dhahiri wakati wa vita, silaha za kibaiolojia ambazo zinatengenezwa na virusi au bakteria, vinaweza kupenyezwa katika maji, hewa, mifugo, ardhi, miili

iliyokufa na kadhalika ambazo huchukua muda mrefu kuweza kutafuta ushahidi au uthibitisho wa madhara. Hivyo, ni vyema Itifaki hii ikaongezewa muda wa kujumuishwa ili wataalamu mbalimbali wa sayansi waweze kuona namna bora zaidi ya kufanya kabla ya kuridhia Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; pamoja na ukweli kwamba Tanzania siyo kisiwa na kwamba tunalazimika kuingia katika mikataba na itifaki mbalimbali za kimataifa, ni lazima kama Taifa tuingie kwenye mikataba hiyo tukiwa na tahadhari hasa kwa vipengele ambavyo vinaweza kuwa na athari kwetu. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inashauri na kupendekeza kwamba tuendeleo kupigania haki ya kuwepo kwa kifungu kinachotoa haki ya kuwa na stara katika kuridhia Itifaki (*reservation*) hasa kwa vifungu vile ambavyo tunaona wazi kwamba vinaweza kuwa na madhara kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhitimisha kwa kusema kwamba ushiriki mpana wa wadau ni jambo muhimu kwani huko ndiko tunakoweza kupata maoni na mawazo mbadala na kujua faida na hasara za kuridhia Itifaki hii au mkataba wowote wa kimataifa. Kwa sababu hiyo, Serikali iwe inajipa muda wa kutosha wa kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali na kujiridhisha kwanza na maudhui ya Itifaki au Mkataba wowote kabla ya kuuleta Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ni kuhusu utekelezaji wa Itifaki na Mikataba ya kimataifa kwa kutunga sheria za ndani za kusaidia utekelezaji huo. Imekuwa ni desturi ya nchi yetu kwa miaka mingi sasa ya kuridhia Mikataba au Itifaki za Kimataifa na kutozitekeleza. Hivyo ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani...

**MWENYEKITI:** Sekunde 10.

**MHE. LATHIFAH H. CHANDE - MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Serikali kuleta haraka iwezekanavyo Muswada wa sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya ndani ya namna ya kuwajibika kisheria na kulipa fidia kwa wale wote wanaohusika na matumizi ya bioteknolojia kwa lengo la kulinda na kuhifadhi bionuai na mazingira kwa ujumla wake

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo yote, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU  
AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA ITIFAKI YA NYONGEZA YA  
NAGOYA – KUALA LUMPUR KUHUSU UWAJIBIKAJI KISHERIA  
NA FIDIA KUTOKANA NA MADHARA YANAYOWEZA KUTOKEA  
KUTOKANA NA MATUMIZI YA BIOTEKNOLOJIA YA KISASA  
KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

*“Yanatolewa kwa Mujibu wa Kanuni za kudumu za Bunge  
ya 53(6) (c)*

**A. UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, Bayoteknolojia ya kisasa inaweza kuleta manufaa mengi. Lakini, kuna hofu ya kwamba inaweza kuwa na madhara makubwa kwa bayoanwai na kwa afya ya binadamu. Kwa sababu hiyo, lengo la kuanzishwa kwa Itifaki ya Nyongeza ya Nagoya – Kuala Lumpur lilikuwa ni kuendeleza uhifadhi wa mazingira na kufanya matumizi endelevu ya bayoanwai (mtawanyiko, mwingiliano na kutegemeana baina ya viumbe hai na mazingira) ili kukabiliana na madhara yatokanayo na matumizi ya bioteknolojia.

2. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa bayoanwai suala la kimataifa; na kwa kuwa athari zitokanazo na uharibifu wa bayoanwai zinavuka mipaka ya nchi moja kwenda nyingine ilionekana ni jambo muhimu na lenye afya katika utunzaji wa bayoanwai yenyewe pamoja na mazingira kwa ujumla wake kuweka kanuni na taratibu za kimataifa na hasa katika dhana ya uwajikaji kisheria na pia kulipa fidia ikiwa kutatokea

madhara yanayohusiana na Viumbe Hai vilivyofanyiwa Maboresho ya Vinasaba (Living Modified Organisms)

3. **Mheshimiwa Spika**, ni katika maudhui hayo ambapo kifungu cha tatu cha itifaki hii kinaeleza bayana kwamba itifaki hii ya nyongeza itahusu madhara yatokanayo na Viumbe Hai vilivyopandikizwa vinasaba tofauti kwa lengo la kuviboresha ambavyo katika kuishi kwake vinavuka mipaka ya nchi moja kwenda nyinge.

4. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa itifaki hii, madhara yanayotokana na matumizi ya bioteknolojia inayopelekea uharibifu wa mazingira na bayoanwai yatahesabiwa kuwa ni madhara ikiwa yatakuwa yanaonekana yanapimika na yenye athari kwa afya ya binadamu. Aidha, itifaki inaelekeza kwamba ili mtu iweze kuwajibika na au kulipa fidia ni lazima mlalamikaji aweze kuthibitisha kuwa madhara hayo yana uhusiano wa moja kwa moja na viumbe vilivyofanyiwa maboresho ya vinasaba.

## B. MAMBO YA MSINGI YA KUZINGATIA KABLA KURIDHIA ITIFAKI

5. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na ukweli kwamba itifaki hii inaonekana kuwa na nia njema ya kupambana na kuzuia madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya bioteknolojia; kwa kuweka kanuni za kimataifa za kuiwajibikaji kisheria na kulipa fidia kwa madhara ya namna hiyo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa Serikali na Bunge kuzingatia mambo yafuatayo kabla ya kuridhia itifaki hii:-

### *i. Uwezo wa Nchi katika Sayansi na Teknolojia*

6. **Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelezwa hapo awali, itifaki hii katika mawanda mapana inahusu kukabiliana na madhara yatokanayo na matumizi ya bioteknolojia na hususan upandikizaji wa vinasaba katika viumbe hai. Hili ni jambo linalohitaji uwezo mkubwa wa kisayansi na kiteknolojia. Tofauti na nchi zilizoendelea, nchi ambazo ziko nyuma kimaendeleo ikiwemo Tanzania bado hazina uwezo mkubwa katika sayansi na teknolojia kuweza kufanya tafiti na gunduzi za kisayansi kama vile '*genetic engineering*' masuala yanayofanana na hayo.

**7. Mheshimwa Spika**, kwa mujibu wa itifaki hii, ili mlalamikaji aweze kulipwa fidia kutokana na madhara ya matumizi ya bioteknolojia ni lazima aweze kuthibitisha kwamba madhara hayo yanatokana na viumbe vilivyofanyiwa maboresho ya vinasaba. Kwa maneno mengine ni kwamba kama nchi itaathirika kutokana na matumizi ya bioteknolojia kutoka nje, ni lazima tuwe na maabara madhubuti na watafiti waliobobea katika sayansi ili kuweza kugundua kama madhara tuliyopata yana uhusiano wa moja kwa moja na viumbe vilivyopandikizwa vinasaba.

**8. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba jambo hili litakuwa gumu sana hasa kwa nchi yetu kutokana na Serikali kutoipa kipaumbele Tume yetu ya Sayansi na Teknolojia. Kwa mfano; kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21, Serikali ilijiwekea kiwango cha kutenga asilimia moja (1%) ya pato ghafi la Taifa (GDP) kwa ajili ya shughuli Sayansi, Teknolojia na Ugunduzi<sup>1</sup> . Hata hivyo, Serikali haijawahi kutenga kiasi hicho tangu imejiwekea utaratibu huo.

**9. Mheshimiwa Spika**, pato ghafi la taifa kwa sasa ni dola za Kimarekani bilioni 52.09 ambazo ni sawa na shilingi 119,807,000,000,000 (trilioni 119.807) Hii ina maana kwamba ikiwa Serikali ingefuata utaratibu iliyojiwekea wa kutenga asilimia moja ya Pato Ghafi la Taifa, ingetakiwa kutenga shilingi 1, 198,070,000,000 (trilioni 1.198).

**10. Mheshimiwa Spika**, fedha iliyotengwa kwa Tume ya Sayansi na Teknolojia - COSTECH kwa ajili ya tafiti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni shilingi bilioni 7.574 sawa na asilimia 0.00632. Hiki ni kiwango kidogo kuliko vyote tangu Serikali hii ya awamu ya tano iingie marakani.

**11. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa angalizo kwa Serikali kuwa makini katika suala hili la tafiti za kisayansi kwa kuwa kuna hatari ya Tanzania kuendelea kuwa watumwa wa teknolojia ya nje jambo ambalo litazidi

kuwaweka watanzania mbali katika kushiriki kujenga uchumi wa nchi yao. Mwenendo huu wa kuendelea kutenga fedha kidogo kwa ajili ya tafiti hauna afya hata kidogo kwa mustakabali wa Sayansi, Teknolojia na Ugunduzi katika taifa. Hata ndoto za Serikali za kujenga uchumi wa viwanda hazizwezi kufikiwa ikiwa hakuna uwekezaji wa kutosha katika tafiti.

**12. Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua umuhimu wa tafiti katika kukuza na kuendeleza Sayansi na Teknolojia; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupitia CHADEMA imeeleza bayana katika sera yake ya elimu sura ya 6.1 inayohusu Mfumo wa Ugunduzi na Ubunifu juu ya umuhimu wa tafiti. Sera hiyo inaeleza kama ifuatavyo: *“Chadema inaamini kwamba msingi wa ugunduzi na ubunifu katika elimu unajengwa katika tafiti za kisayansi. Kwa hiyo, kwa kushirikiana na sekta binafsi, Chadema itawekeza kikamilifu katika elimu ya utafiti kuanzia elimu ya awali ili kumjengea mtoto uwezo wa ubunifu”*.

*ii. Ushiriki wa Wadau katika Uchambuzi wa Itifaki*

**13. Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na desturi mbaya ya kupitisha maazimio ya kuridhia itifaki na mikataba mbalimbali ya kimataifa kwa ghafla ghafla, bila kuwashirikisha kikamilifu wadau katika kufanya uchambuzi wa kina wa faida na au madhara ya itifaki au mikataba husika na wakati mwingine bila hata kujali kama akidi ya Bunge imetimia au la katika kupitisha uamuzi.

**14. Mheshimiwa Spika**, katika suala gumu na lenye kuhitaji utaalamu wa kisayansi kama hili linalohusu matumizi ya bayoteknolojia na madhara yake katika bayoanwai; Serikali iwe imefanya uchambuzi wa kina juu ya athari za kuridhia itafaki hii na kuwapatia waheshimiwa wabunge semina elimishi ili kuweza kulishawishi Bunge kuridhia jambo ambalo wana uelewa nalo.

**15. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina hakika kama uchambuzi huo umefanyika na kama wabunge wameshirikishwa kwa kiwango cha kutosha. Jambo

hilo ni hatari kwa kuwa Bunge linaweza kuridhia jambo ambalo litakuwa na madhara baadaye kwa nchi yetu kutokana na kukosa uelewa kuhusu jambo lenyewe.

*iii. Masuala ambayo Itifaki hii Haitahusika (Exemptions)*

**16. Mheshimiwa Spika**, kifungu cha 16 cha itifaki hii kinasema kwamba; naomba kunukuu:-

*“Parties may provide, in their domestic law, for the following exemptions:*

*a. Act of God or force majeure; and*

*b. Act of war or civil unrest.*

**17. Mheshimiwa Spika**, kwa tafsiri isiyo rasmi ni kwamba masharti ya itifaki hii hayatumika katika nyakati za vita au machafuko ya kisiasa na nyakati za majanga ya asili. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuwa makini sana na kifungu hiki kwa kuwa kinatoa kinatoa kinga ya kutowajika kisheria au kulipa fidia kwa madhara yatoakanayo na matumizi ya bioteknolojia nyakati za vita au machafuko.

**18. Mheshimiwa Spika**, nchi zilizoendelea kisayansi na kiteknolojia ambazo zimefikia hatua ya kutengeneza silaha za kibaiolojia (biological weapons) zinaweza kutumia mwanya huu kupenyeza silaha za kibaiolojia ambazo kwa asili ni za maangamizi makubwa (weapons of mass distruction) na wakakwepa kuwajibika kisheria au kulipa fidia kwa kisingizio kuwa ni wakati wa vita au machafuko. Katika mazingira kama hayo, nchi zilizo nyuma kimaendeleo zitabaki kuwa wahanga wa matukio kama hayo (victims of circumstance).

*iv. Haki ya Kuwa na Stara (Reservation) katika Baadhi ya Vifungu*

**19. Mheshimiwa Spika**, katika kifungu cha 19 cha Itifaki hii ambayo inazitaka nchi wanachama kuridhia mkataba bila stara *‘No reservation may be made to this Suplimentary Protoco’* ni wazi kuwa Ibara hii ni ya kuangaliwa kwa mapana zaidi. Sote tunatambua katika ulimwengu wa sasa vita kubwa inayopiganwa kitaalamu na kisayansi ni vita ya kibaiolojia yaani biological weapons. Yapo magonjwa mengi ambayo

yamezua mijadala mikubwa duniani ambapo wengi wa wataalamu wanaamini ni magonjwa ya kutengenezwa ambayo kitaalamu yamtokana na genetic modification.

**20. Mheshimiwa Spika**, kwa mantiki hiyo , endapo nchi tutaridhia vifungu ambavyo tayari vinaonyesha walakini kama ilivyo kwa Ibara ya sita ya Itifaki hii tunaweza kujikuta katika hatari kubwa. Ni dhahiri wakati wa vita silaha za kibaolojia ambazo zinatengenezwa na virus au bakteria vinaweza kupenyezwa katika maji, hewa, mifugo, ardhi, miili iliyokufa n.k ambazo huchukua muda mrefu kuweza kutafuta ushahidi au uthibitisho wa madhara. Hivyo, ni vyema, Itifaki hii kaongezewa muda wa kujumuisha zaidi wataalamu mbalimbali wa sayansi ili kuona namna bra zaidi ya kufanya kabla ya kuridhia itifaki hii.

### C. HITIMISHO

**21. Mheshimiwa Spika**, pamoja na ukweli kwamba Tanzania sio kisiwa, na kwamba tunalazimika kuingia katika mikataba na itifaki mbalimbali za kimataifa; ni lazima kama taifa tuingie kwenye mikataba hiyo tukiwa na tahadhari hasa kwa vipengele ambayo vinaweza kuwa na athari kwetu. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba; tuendeleee kupigania haki ya kuwepo kwa kifungu kinachotoa haki ya kuwa na stara katika kuridhia itifaki (reservation) hasa kwa vifungu vile ambayo tunaona wazi kwamba vinaweza kuwa na madhara kwetu.

**22. Mheshimiwa Spika**, napenda kuhitimisha kwa kusema kwamba ushiriki mpana wa wadau ni jambo muhimu kwani huko ndiko tunakoweza kupata maoni na mawazo mbadala na kujua faida na hasara za kuridhia itifaki au mkataba wowote wa kimataifa. Kwa sababu hiyo, Serikali iwe inajipa muda wa kutosha wa kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali na kujiridhisha kwanza na maudhuri ya itifaki au mkataba wowote kabla ya kuuleta Bungeni.

**23. Mwisho kabisa Mheshimiwa Spika**, ni kuhusu utekelezaji wa itifaki na mikataba ya kimataifa kwa kutunga sheria za ndani za kusaidia utekelezaji huo. Imekuwa ni desturi



ya nchi yetu kwa miaka mingi sasa ya kuridhia mikataba na itifaki za kimataifa na kutozitekeleza. Hivyo ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Serikali kuleta haraka iwezekanavyo Muswada wa Sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya ndani ya namna ya kuwajibika kisheria na kulipa fidia kwa wale wote wanaohusika na matumizi ya bioteknolojia kwa lengo la kulinda na kuhifadhi bayoanwai na mazingira kwa ujumla wake.

**24. Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha.

Lathifah H. Chande (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI  
KATIKA OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA**

11 September, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Waziri wa Kilimo ili awasilishe Azimio la Kuridhia Itifaki ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Kulinda Haki Miliki za Wagunduzi wa aina mpya za Mbegu za Mimea.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za kusini mwa Afrika kuhusu kulinda haki miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea (*Protocol for Protection of New Varieties of Plants (Plant Breeder's Rights) in The Southern African Development Community – SADC*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini kwa ushauri waliutoa wakati wa kujadili azimio hili. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Azimio hili limezingatia ushauri na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chimbuko la Azimio hili ni Mkataba wa Kuanzishwa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za

Kusini mwa Afrika (*Southern Africa Development Community – SADC*). Ibara ya 22 ya Mkataba wa *SADC (SADC Treaty)* wa mwaka 1992 umebainisha umuhimu wa kuandaa itifaki za kutoa miongozo ya ushirikiano kwenye masuala ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi wanachama wa *SADC* ziliandaa Itifaki ya *SADC* ya kulinda haki miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea mwezi Mei mwaka 2017. Itifaki hiyo ilidhinishwa na Mawaziri wa Katiba na Sheria wa nchi za *SADC* Julai, 2017 na baadaye ilithibitishwa na Baraza la Mawaziri wa Kilimo la *SADC* Agosti, 2017, Mjini Izulwini, Eswatini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la itifaki hii ni kutoa mwongozo kuhusu kulinda haki miliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea ili kuhamasisha ugunduzi wa mbegu mpya katika ukanda wa *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi sasa nchi zilizosaini Itifaki hii ni saba ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ilisaini tarehe 18 mwezi Agosti mwaka 2019 wakati wa mkutano wa nchi wanachama wa *SADC* uliofanyika Windhoek, Namibia. Aidha, mnamo tarehe 31 mwezi Oktoba mwaka 2018, Baraza la Mapinduzi la Zanzibar liliridhia mapendekezo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwasilisha Itifaki hiyo Bungeni ili iweze kuridhiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itifaki hii ina sehemu kumi; sehemu ya utangulizi (*preamble*) ina kipengele cha kwanza kinachotoa tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika ndani ya Itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza yenye ibara tano inabainisha malengo na mawanda ya Itifaki hiyo. Miongoni mwa malengo hayo ni kutoa hakimiliki kwa wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea ili kuhamasisha ugunduzi wa aina mpya za mbegu za mazao

ya kilimo na kuwawezesha kuwa na mfumo thabiti wa kulinda hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili yenye ibara tano, ambapo Ibara ya 7 inaweka vigezo vya masharti ya kuzingatia katika utoaji wa hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea. Mbegu itakayohusika inapaswa kuwa mpya inayotofautiana na nyingine (*distinct*) na inayofanana (*uniformity*) na isiyobadilika (*stable*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu na ya nne zenye ibara 14 inabainisha utaratibu utakaotumika katika utoaji wa hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya ya mbegu za mimea na namna ya kushughulikia maombi wa hakimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano inahusu muda wa hakimiliki uliotolewa chini ya itifaki ambao utadumu kwa miaka 25 kwa mazao ya miti ya jamii ya mizabibu na miaka 20 kwa mazao mengine. Aidha, sehemu hii inahusu haki za wagunduzi waliopewa hakimiliki. Mgunduzi atakuwa na haki ya kuidhinisha uzalishaji wa mbegu husika na kuruhusu kuuzwa kwa mbegu husika, kusafirisha mbegu au kuhifadhi mbegu husika. Vilevile sehemu hii inaweka zuio kuwa ni kinyume cha sheria kwa mtu mwingine kutumia mbegu yenye hakimiliki kibiashara bila idhini ya mgunduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya sita, saba na ya nane inaruhusu utoaji wa leseni na uhaulishaji wa hakimiliki ambapo Ibara ya 34 inaweka masharti kwa ajili ya uhaulishaji wa hakimiliki. Aidha, Ibara ya 35 inatoa fursa ya kurudisha hakimiliki ambapo Ibara ya 36 inatoa mwongozo wa kubatilisha na Ibara ya 37 inahusu kufuta hakimiliki kwa mujibu wa itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tisa na ya kumi inahusu masuala ya jumla ambapo Ibara ya 43 inahusu usuluhishi wa mgogogo (*dispute settlement*) na inabainisha kuwa migogoro kati ya nchi wanachama wa SADC kuhusu utekelezaji wa Itifaki hiyo iliyoshindwa kupata suluhu kwa mazungumzo itawasilishwa kwa Mawaziri wa Kilimo na

Usalama wa Chakula wa Nchi Wanachama wa SADC. Aidha, kama hakutakuwa na suluhu katika ngazi ya Mawaziri wa Kilimo na Usalama wa Chakula, suala hili litawasilishwa Baraza la Usuluhishi wa Migogoro la SADC (*SADC Tribunal*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 44 inaruhusu haki ya nchi wanachama kujitoa kwenye Itifaki hii. Kwa mujibu wa ibara hiyo, nchi mwanachama inaweza kujitoa baada ya kupita miezi 12 kutoka siku itakayotoa *notice* ya kujitoa. Pia inabainisha kuwa nchi inayotoa *notice* haltapata haki na faida zinazoambatana na Itifaki hii katika kipindi cha kusubiri maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mapendekezo ya kuridhiwa kwa Itifaki hii, Azimio hili linaweka sharti (*reservation*) itakayoivezesha Tanzania kutolazimika kutekeleza masharti ya Itifaki ambayo yanaweza kuathiri maslahi ya Taifa. Utaratibu huu unatambuliwa kimataifa kupitia sehemu ya pili ya Itifaki ya *Vienna Convention on the Law of Treaties* uliosainiwa mwaka 1969 ambapo Tanzania ni mojawapo ya nchi iliyoridhia kutumia mkataba huu tarehe 12 mwezi Aprili, 1974.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia maelezo hayo, naomba sasa kuwasilisha Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika Kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea kama ifuatavyo:-

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*The Southern Africa Development Community – SADC*) kwa mujibu wa mkataba ulioanzishwa jumuiya hii ambao ulisainiwa na Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika mnamo mwaka 1992;

KWA KUWA, Mkataba huu unazitaka nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini

Mwa Afrika kushirikiana kwenye masuala yenye maslahi kwa maendeleo na ustawi wa wananchi wa nchi hizo;

KWA KUWA, Ibara ya 22 ya Mkataba wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika wa Mwaka 1992 umebainisha umuhimu wa nchi wanachama kuandaa itifaki zitakazotumika kutoa miongozo ya ushirikiano kwenye masuala yenye maslahi kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa wananchi wa nchi hizo;

NA KWA KUWA, mkataba huu unaelekeza kwamba kila Itifaki itakayoandaliwa itaidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini Mwa Afrika na ikapaswa kusainiwa na kuridhiwa na nchi wanachama;

KWA KUWA, katika kutoa mwongozo kuhusu kulinda hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya ya mbegu za mimea (*protection on new varieties of plants*), nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini Mwa Afrika ziliandaa Itifaki ya Kulinda Kakimiliki ya Wagunduzi wa Aina Mpya ya Mbegu za Mimea ya Mwezi Mei, 2017 ambao iliidhinishwa na Mawaziri wa Katiba na Sheria wa Nchi za SADC mwezi Julai, 2017 na baadaye ilithibitishwa na Baraza la Mawaziri wa Kilimo wa SADC mwezi Agosti, 2017;

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Biashara Duniani (*World Trade Organization*) kuanzia tarehe 1 Januari, 1995 na kama mwanachama wa WTO inalazimika kutekeleza makubaliano mbalimbali yaliyoridhiwa na wanachama wa shirika hilo na miongoni mwa makubaliano hayo ni kuhusu makubaliano ya utekelezaji wa masuala ya hakimiliki (*trade related aspect of intellectual property rights*);

KWA KUWA, Itifaki ya Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (*The Protocol For Protection of New Varieties of Plants (Plant Breeder's Rights) in the Sothern Africa Development Community – SADC*) ilisainiwa mwezi Agosti, 2018 Jijini Windhoek, Namibia katika

Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika;

KWA KUWA, madhumuni ya Itifaki hiyo kama yalivyoainishwa katika Ibara ya 2 ni pamoja na (a) kuwezesha kuwa na mfumo thabiti wa kulinda hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea; (b) kuhamasisha ugunduzi wa aina mpya za mbegu za mazao ya kilimo; na (c) kutoa hakimiliki kwa wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea;

KWA KUWA, Tanzania imesaini kuridhia na kutekeleza mikataba mingine inayohusiana na hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea ambao ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (*UPOV Convention*) ambao mikataba hii ni muhimu ikatekelezwa kwa pamoja;

NA KWA KUWA, kuridhiwa kwa Itifaki hii kutakuwa na matokeo chanya yafuatayo: (a) Kuweka mfumo wa kulinda hakimiliki za wagunduzi wa mbegu unaokubalika na kutekelezwa katika nchi za *SADC* na hivyo kuimarisha mahusiano ya nchi yetu na nchi nyingine; (b) Hakimiliki itakayotolewa chini ya Itifaki ya *SADC* itatambuliwa ndani ya nchi zote wanachama wa *SADC* na hivyo kuchochea uwekezaji katika nyanja ya utafiti na ugunduzi wa mbegu mpya za sekta binafsi; (c) Kupanua wigo na kurahisisha biashara ya mbegu na hivyo kuhamasisha ushindani katika tasnia ya mbegu; (d) Kuhamasisha na kutoa fursa za utafiti unaolenga kuongeza uzalishaji wa mbegu mpya na hatimaye kuwezesha wakulima kupata mbegu bora; (e) Kuongeza upatikanaji wa mbegu bora, kupunguza gharama za usafirishaji na hivyo kupunguza bei ya mbegu kwa mkulima; na (f) Kuwezesha upatikanaji wa mbegu zenye ukinzani wa magonjwa, wadudu wa mimea na kuhimili mabadiliko ya tabianchi;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Itifaki hii kwa Tanzania na kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika na pia

umuhimu wa kuridhia Itifaki hii, Bunge hili kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 linaazimia kuridhia Itifaki ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (*Protocol for Protection of New Varieties of Plants (Plant Breeder's Rights) in The Southern African Development Community – SADC*) bila kulazimika kutekeleza masharti ya mkataba ambayo yanaweza kuathiri maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuridhia Azimio ninaloliwasilisha ili kuwezesha nchi yetu kunufaika na Itifaki ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea katika Ukanda wa SADC.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono, sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, atawasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu Azimio hilo. Dakika 10.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Nakushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hii taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, naomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika Kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Itifaki hii inahusu Nchi Wanachama zilizo Kusini Mwa Afrika (*SADC*), kabla ya kuanza wasilisho langu, kwa niaba ya Kamati nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *SADC*. Kamati inaamini kutokana na uwezo wake mahiri pamoja na mambo mengine wagunduzi wa Tanzania na wenzao kutoka Nchi Wanachama wa *SADC* watanufaika na maudhui yalimo kwenye Itikafi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu madhumuni na malengo; Ibara ya 2 ya Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za *SADC* kuhusu kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu:-

(a) Kuwezesha kuanzisha mfumo thabiti wa kulinda hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea;

(b) Kuendeleza na kuhamasisha ugunduzi wa aina mpya za mbegu za mazao ya mimea kwa manufaa ya nchi wanachama katika Jumuiya ya *SADC*; na

(c) Kutoa hakimiliki kwa wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Itifaki. Itifaki hii imegawanyika katika sehemu kuu 10 na ina jumla ya Ibara 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati kufanya uchambuzi kwenye sehemu hizo za Itifaki, Kamati ilitaka kujiridhisha kwenye maeneo ya msingi na hivyo kuhitaji ufafanuzi kwenye maeneo hayo ambayo ni pamoja na:-

(i) Kwa nini nchi zenye uchumi mkubwa na ambazo zinafanya vizuri katika tasnia ya mbegu na kilimo kama Afrika Kusini, aidha nchi za Mauritius na Seychelles ambazo zina uchumi mkubwa hazijasaini Itifaki hii?



(ii) Kuna uharaka gani wa kuridhia Itifaki hii wakati ni nchi saba tu kati ya nchi 15 Wanachama wa *SADC* ndizo zimesaini Itifaki hii?

(iii) Je Itifaki hii haiwezi kusababisha ukiritimba kutoka katika makampuni makubwa ya mbegu katika tasnia ya mbegu?

(iv) Je vituo vya Afrika kwa ajili ya masuala ya hakiubunifu vya *ARIPO* na *PAIPO* (Chini ya Umoja wa Afrika) haviwezi kuingilliana na kusigana na Itifaki hii?

(v) Ni kwa kiasi gani uhuru wa mkulima mdogo katika uzalishaji mbegu umezingatiwa kwenye Itifaki hii?

(vi) Ni kwa kiasi gani kama nchi tumewekeza katika tafiti za mbegu ili kuweza kumudu ushindani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati imeridhishwa na ufafanuzi uliotolewa na Serikali kuhusu hoja zilizoibuliwa na Waheshimiwa Wabunge. Aidha, Kamati ilifanya kikao na wagunduzi wa watafiti za mbegu waliotoka Serikalini na katika Sekta Binafsi ambao Itifaki hii inawagusa moja kwa moja. Kupitia mjadala huu wadau hao waliihakikishia Kamati kuwa kuridhiwa kwa Itifaki hii kutakuwa na manufaa yafuatayo: -

(1) Serikali itanufaika na fedha ilizowekeza kwenye utafiti;

(2) Uwepo wa mrabaha utakaopatikana kutokana na gawio ambapo Serikali itapata mapato yatakayotokana na gawio;

(3) Kuongeza motisha kwa Watafiti;

(4) Kuongezeka kwa ushindani na ubunifu miongoni mwa watafiti;

(5) Kutarahisisha upatikanaji wa mbegu bora, mpya kwa haraka;

(6) Kuridhiwa kwa Itifaki hii kutaongeza uzalishaji wa chakula kwa kuwa wakulima watapata mbegu bora na mpya na hivyo kuhakikishia Taifa usalama wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya uchambuzi wa Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika Kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea, Kamati inakubaliana na dhamira njema ya Itifaki hii kwa Taifa na kwa Wagunduzi wa ndani. Pamoja na dhamira njema iliyopo, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao:-

Moja, Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya vituo vya utafiti ili kuwezesha watafiti kufanya tafiti kwa kutumia fedha zetu za ndani na siyo kama ilivyo sasa ambapo tafiti nyingi hufanyika kwa kutegemea fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo. Bila ya kuwezesha vituo vya utafiti na wagunduzi wa mbegu, Itifaki hii inaweza kunufaisha wagunduzi wa mbegu kutoka Mataifa mengine na sisi kubaki kuwa watazamaji tu. *(Makofi)*

Pili, ni muhimu kwa sera na sheria zinazohusiana na mbegu zikafanyiwa mapitio ili ziweze kuendana na maudhui ya Itifaki hii.

Tatu, Serikali ifanye mapitio na maboresho ya Sheria ya Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea ya Mwaka 2012 ili sheria hii iweze kujumuisha maudhui ya Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika na kurekebisha baadhi ya upungufu ulioko kwenye sheria ikiwa ni pamoja na kipengele kinachoeleza hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu kutovuka mipaka ya Tanzania.

Nne, Serikali iweke mazingira wezeshi kwa ajili ya kuvutia uzalishaji wa mbegu nchini. Uzalishaji mbegu, pamoja

na mambo mengine yafuatayo kutaongeza motisha kwa wagunduzi wa mbegu kugundua aina mpya za mbegu, kuokoa fedha nyingi za kigeni zinazotumika kuagiza mbegu nje ya nchi, kiasi cha shilingi bilioni 860 hutumika kuagiza mbegu kutoka nje ya nchi na kuongezeka kwa mapato ya Serikali, ajira na ujuzi kwa wananchi wazawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti,napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Japhet Hasunga Mbunge, Manaibu Waziri Mheshimiwa Omary Mgumba Mbunge na Mheshimiwa Hussein Bashe Mbunge, na Makatibu Wakuu wa Wizara ya Kilimo, Mhandisi Mathew Mtigumwe na Profesa Siza Tumbo pamoja na Wataalam wote wa Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano walioutoa wakati Kamati ilipokuwa ikichambua Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nawashukuru wadau wote waliotoa michango kwa maandishi na kwa kufika katika mbele ya Kamati. Kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kuchambua na kujadili Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za BungeNdugu Michael Chikokoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee na lijadili na liridhie Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Kulinda Hakilimiki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA ITIFAKI YA  
MAENDELEO YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA KUHUSU  
KULINDA HAKIMILIKI ZA WAGUNDUZI WA AINA MPYA ZA  
MBEGU ZA MIMEA (THE PROTOCOL FOR PROTECTION OF NEW  
VARIETIES OF PLANT [PLANT BREEDER'S RIGHTS] IN  
THE SOUTHERN AFRICAN DEVELOPMENT  
COMMUNITY – SADC) – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika Kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (*The Protocol for Protection of New Varieties of Plant [Plant Breeder's Rights] In The Southern African Development Community – SADC*).

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Itifaki hii inahusu Nchi Wanachama zilizo Kusini Mwa Afrika (SADC), kabla ya kuanza wasilisho langu, kwa niaba ya Kamati naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Nchi za SADC. Kamati inaamini kutokana na uwezo wake mahiri pamoja na mambo mengine Wagunduzi wa Tanzania na wenzao kutoka nchi Wanachama wa SADC watanufaika na maudhui yalimo kwenye Itikafi hii.

**Mheshimiwa Spika**, Nyongeza ya Nane Kifungu cha 7(1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, inazipa Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria, Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia. Aidha, jukumu hili pia ni jukumu la Kikatiba chini ya Ibara ya 63(3)(e) ya

Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 12 Novemba, 2018 uliiletea Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kazi ya kushughulikia Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika (*The Protocol For Protection of New Varieties of Plant [Plant Breeder's Rights] In The Southern African Development Community – SADC*) kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea kama lilivyowasilishwa na Serikali ili Kamati iweze kuchambua mapendekezo ya Azimio husika na hatimae kutoa maoni na ushauri kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyo ada, Kamati ilianza kuchambua Itifaki husika kwa kushirikiana na wadau waliofika mbele ya Kamati na wale waliotuma maoni yao kwa njia ya maandishi ili kufahamu madhumuni na faida zinazoambatana na kuridhiwa kwa Itifaki hii. Hata hivyo, baada ya kushauriana na Serikali ilibainika kuna umuhimu wa kuongeza muda ili Kamati iweze kufanyia kazi zaidi ili matokeo chanya yaliobainishwa kwenye Itifaki hii yaweze kuleta maslahi kwa wananchi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, kwa hekima na busara uliridhia kuongezwa kwa muda wa kushughulikiwa kwa Itifaki hii ambapo tarehe 28 Agosti, 2019 uliiletea tena Kamati kazi ya kushughulikia Itifaki tajwa. Tarehe 04 Septemba, 2019 Kamati ilianza kazi ya kushughulikia Itifaki hii ambalo liliwasilishwa mbele ya Kamati na Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. Omary Mgumba, (Mb).

## **2.0 MADHUMUNI/MALENGO YA ITIFAKI**

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 2 ya Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika (SADC) kuhusu kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea ina madhumuni ya msingi yafuatayo: -

- (a) Kuwezesha kuanzisha mfumo thabiti wa kulinda hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea;
- (b) Kuendeleza na kuhamasisha ugunduzi wa aina mpya za mbegu za mazao ya mimea kwa manufaa ya nchi wanachama katika Jumuiya ya SADC; na
- (c) Kutoa Hakimiliki kwa Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea.

### **3.0 UCHAMBUZI WA ITIFAKI**

**Mheshimiwa Spika**, Itifaki hii imegawanyika katika sehemu kuu kumi (10) na ina jumla ya Ibara 50 ambazo maudhui yake ni kama ifuatavyo: -

#### **Sehemu ya Kwanza**

**Ibara ya 1** ya Itifaki inahusu masharti ya jumla ambayo inaanzia Ibara ya 2 hadi ya 6.

**Ibara ya 2** inahusu madhumuni ya Itifaki ambayo yameelezwa hapo juu.

**Ibara ya 3** inahusu mawanda na maeneo ambayo itifaki hii itatumika.

**Ibara ya 4** ya itifaki inaanzisha Ofisi ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Mbegu za Mimea katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia utekelezaji wa itifaki hii.

**Ibara ya 5** ya itifaki inaanzisha Kamati ya Ushauri ya SADC kwa ajili ya kuishauri Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki za Wagunduzi wa Mbegu za Mimea katika mambo ya jumla na mahsus kuhusiana na utekelezaji wa majukumu yake na mambo mengine yanayohusiana na itifaki hii.

**Ibara ya 6** inaanzisha Rejista ya Usajili wa Hakimiliki kwa Wagunduzi wa Mbegu za Mimea ambayo itatunzwa na Msajili.

## Sehemu ya Pili

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ya itifaki inaanzia **Ibara ya 7 hadi 11** na inahusu masharti ya utoaji wa Hakimiliki za Ugunduzi ambapo ibara hizo zimefafanua kwa undani vigezo vitakavyotumika kutoa hakimiliki hizo.

## Sehemu ya Tatu

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya tatu ya itifaki imeanzia **Ibara ya 12 hadi 22** ambapo ibara hizi zimeweka utaratibu wa jinsi ya kutuma maombi ya kupewa hakimiliki ya ugunduzi wa mbegu za mimea. Aidha, ibara hizi zimefafanua kiundani watu wanaostahili kuomba hakimiliki, utaratibu wa kutuma maombi, haki ya kipaumbele katika kushughulikia maombi pamoja na mambo mengine yanayoendana na maombi ya hakimiliki.

## Sehemu ya Nne

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya nne inaanzia **Ibara ya 23 hadi 25** na inaeleza vigezo ambavyo vitatumika katika kufikiria maombi ya utoaji hakimiliki.

## Sehemu ya Tano

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inahusu **Ibara ya 26 hadi 31** na inaeleza kuhusu haki za mmiliki wa hakimiliki. Aidha ukomo wa muda wa matumizi ya hakimiliki kwa mbegu za miti umeelezwa utakuwa miaka ishirini na tano (25) tangu siku ya kutolewa na kwa mbegu nyingine za mimea ukomo wa hakimiliki utakuwa miaka ishirini (20). Hata hivyo ukomo wa muda kwa mbegu nyingine za mimea, unaweza kuongezwa na Msajili kutokana na mapendekezo yatakayotolewa kwake na Kamati inaweza kuongeza muda usiozidi miaka mitano (5).

## Sehemu ya Sita

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ambayo ina **Ibara ya 32 na 33**, inaelezea kuhusu utoaji wa leseni zinazohusiana na uzalishaji

wa mbegu za mimea kutoka kwa mmiliki wa hakimiliki ya Wagunduzi wa mbegu za mimea.

### Sehemu ya Saba

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inalbara moja ambayo ni ya 34 na inaweka masharti kuhusu uhamishaji wa hakimiliki ya Wagunduzi wa mbegu za mimea.

### Sehemu ya Nane

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inalbara ya 35, 36, na 37 na inaeleza utaratibu wa kurudisha, kubatilisha na kufutwa kwa hakimiliki.

### Sehemu ya Tisa

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inalbara moja ya 38 ambayo inaanzisha Bodi ya Rufaa kwa ajili ya rufaa kwa mtu ambaye hataridhika na maamuzi ya Msajili.

### Sehemu ya Kumi

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya kumi inaanzia Ibara ya 39 hadi 50 inaelezea masharti ya jumla ikiwemo utungaji wa Kanuni na taratibu za uendeshaji wa Itifaki, kulinda aina za mbegu ambazo zilikuwepo kabla ya Itifaki hii, masuala ya fedha, marekebisho ya Itifaki hii, utatuzi wa migogoro, utaratibu wa nchi kujiondoa katika Itifaki hii, utiaji saini wa Itifaki hii, utaratibu wa kuridhia, kuanza kutumika kwa Itifaki, uwasilishwaji wa Hati Idhini na Utekelezaji wa Itifaki.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kufanya uchambuzi kwenye sehemu hizo za Itifaki, Kamati ilitaka kujiridhisha kwenye maeneo ya msingi na hivyo kuhitaji ufafanuzi kwenye maeneo hayo ambayo ni pamoja na:-

i) Kwa nini nchi zenye uchumi mkubwa na ambazo zinafanya vizuri katika tasnia ya mbegu na kilimo kama Afrika kusini, Aidha nchi za Mauritius na Shelisheli ambazo zina uchumi mkubwa hazijasaini Itifaki hii?.



ii) Kuna uharaka gani wa kuridhia Itifaki hii wakati ni nchi saba (7) tu kati ya nchi kumi na tano (15) wanachama wa SADC ndio zimesaini Itifaki hii?.

iii) Je Itifaki hii haiwezi kusababisha ukiritimba (*monopoly*) kutoka katika makampuni makubwa ya mbegu katika tasnia ya mbegu?.

iv) Je vituo vya Afrika kwa ajili ya maswala ya hakiubunifu vya ARIPO (Harare-Zimbabwe), OAPI (Africa Magharibi) na PAIPO (Chini ya Umoja wa Afrika) haviwezi kuingiliana na kusigana na Itifaki hii?.

v) Ni kwa kiasi gani uhuru wa mkulima mdogo katika uzalishaji mbegu umezingatiwa kwenye Itifaki hii?.

vi) Ni kwa kiasi gani kama nchi tumewekeza katika tafiti za mbegu ili kuweza kumudu ushindani wa nchi Wanachama wa SADC katika ugunduzi, uzalishaji na biashara ya mbegu;

vii) Ni kwa kiasi gani Itifaki hii imezingatia utofauti wa maendeleo ya kiuchumi uliko miongoni mwa nchi wanachama wa SADC? na

viii) Je kuna ulazima gani wa kuridhia Itifaki ya SADC wakati katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ambayo Tanzania ni mwanachama haina utaratibu wa Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Mbegu?.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa Kamati imeridhishwa na ufafanuzi uliotolewa na Serikali kuhusu hoja zilizoibuliwa na Wabunge. Aidha, Kamati ilifanya kikao na Wagunduzi na Watafiti wa mbegu waliotoka Serikalini na katika Sekta Binafsi ambao Itifaki hii inawagusa moja kwa moja. Kupitia mjadala huu wadao hao waliiakikishia Kamati kuwa kuridhiwa kwa Itifaki hii kutakuwa na manufaa yafuatayo: -

- Serikali itanufaika na fedha ilizowekeza kwenye utafiti wa mbegu kwa kulinda kazi za utafiti wa mbegu zilizozalishwa na wataalamu wake;

- Uwepo wa mrabaha utakaopatikana kutokana na gawio ambapo Serikali itapata mapato yatakayotokana na gawio, mgunduzi atapata gawio na kiasi kingine cha mrabaha kitatumika kuendeleza ugunduzi wa aina mpya za mbegu;
- Kuongeza motisha kwa Watafiti na Wagunduzi wa mbegu na hivyo kuongeza uzalishaji wa mbegu ambazo zatumika nchini na zingine kuuzwa nje ya nchi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kupunguza gharama kubwa ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mbegu nje ya nchi;
- Kuongezeka kwa ushindani na ubunifu miongoni mwa Watafiti/Wagunduzi wa mbegu
- Kutarahisisha upatikanaji wa mbegu bora na mpya kwa haraka na
- Kuridhiwa kwa Itifaki hii kutaongeza uzalishaji wa chakula kwa kuwa wakulima watapata mbegu bora na mpya na hivyo kuhakikishia taifa usalama wa chakula.

#### 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kufanya uchambuzi wa Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika Kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea, Kamati inakubaliana na dhamira njema ya Itifaki hii kwa Taifa na kwa Wagunduzi wa ndani. Pamoja na dhamira njema iliyopo, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao: -

(a) Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya vituo vya utafiti ili kuwezesha watafiti kufanya tafiti kwa kutumia fedha zetu za ndani na sio kama ilivyo sasa ambapo tafiti nyingi hufanyika kwa kutegemea fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo. Bila ya kuwezesha vituo vya utafiti na wagunduzi wa mbegu, Itifaki hii inaweza kunufaisha wagunduzi wa mbegu kutoka mataifa mengine na sisi kubaki kuwa watazamaji tu.

(b) Ni muhimu kwa Sera na Sheria zinazohusiana na Mbegu zikafanyiwa mapitio ili ziweze kuendana na maudhui ya Itifaki hii.

(c) Serikali ifanye mapitio na maboresho ya Sheria ya Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea ya Mwaka 2012 ili Sheria hii iweze kujumuisha maudhui ya Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika na kurekebisha baadhi ya mapungufu yaliyoko kwenye Sheria ikiwa ni pamoja na kipengele kinachoeleza Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu kutovuka mipaka ya Tanzania.

(d) Serikali iweke mazingira wezeshi kwa ajili ya kuvutia uzalishaji mbegu nchini. Uzalishaji mbegu, pamoja na mambo mengine utaongeza:-

- Motisha kwa wagunduzi wa mbegu kugundua aina mpya za mbegu;
- Kuokoa fedha nyingi za kigeni zinazotumika kuagiza mbegu nje ya nchi – kiasi cha shilingi bilioni 860 hutumika kuagiza mbegu kutoka nje ya nchi na
- Kuongezeka kwa mapato ya Serikali, ajira na ujuzi kwa wananchi wazawa.

## 5.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Kilimo, Mhe. Japhet Hasunga (Mb), Manaibu Waziri Mhe. Omary Mgumba (Mb) na Mhe. Hussein Bashe (Mb), Makatibu Wakuu wa Wizara ya Kilimo, Mhandisi Mathew Mtigumwe na Prof. Siza Tumbo pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano walioutoa wakati Kamati ilipokuwa ikichambua Azimio hili.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru wadau wote waliotoa michango yao kwa maandishi na kwa kufika mbele ya Kamati. Michango yao ilisaidia kuijengea uwezo Kamati na kuwawezesha Wajumbe kuwa na uelewa mpana kuhusiana na Azimio hili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kuchambua na kujadili Azimio hili. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Mahmoud Hassan Mгимwa Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb M/Mwenyekiti
3. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb Mjumbe
4. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb "
5. Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani, Mb "
6. Mhe. Katani Ahmad Katani Mb "
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb "
8. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb "
9. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb "
10. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb "
11. Mhe. Lucy Simon Magereli, "
12. Mhe. Justin Joseph Monko "
13. Mhe. Omar Abdallah Kigoda, Mb "
14. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb "
15. Mhe. Pascal Yohana Haonga "
16. Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb "
17. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb "
18. Mhe. Devotha Methew Minja, Mb "
19. Mhe. Haji Ameir Haji, Mb "
20. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb "
21. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb "
22. Mhe. Juma Ali Juma, Mb "
23. Mhe. Emmanuel Papian John, Mb "
24. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb "
25. Mhe. Anthony Calist Komu, Mb "
26. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb "

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kwa namna ya kipekee naishukuru Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Virgil Mtui na Ndg. Rachel Nyega pamoja na msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John kwa kuihudumia Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na liridhie Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika kuhusu Kulinda Hakilimiki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Dkt. Christine G. Ishengoma, (Mb)  
**M/MWENYEKITI,**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO,**  
**MIFUGO NA MAJI**  
11 Septemba, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Kilimo atatoa maoni ya Upinzani kuhusu Azimio hilo, Mheshimiwa Haongadakika kumi. (*Makofi*)

**MHE. PASCAL Y. HAONGA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Kulinda Hakilimiki za Ugunduzi wa aina mpya za Mbegu za Mimea (*The Protocol for Protection of New Varieties of Plants (Plant Breeder's Rights) in the Southern African Development Community-SADC*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Azimio hili ni dhahiri Tanzania haiwezi kujitenga na Mataifa au Jumuiya nyingine hasa katika kushirikiana kwenye masuala mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuliona hili la ushirikiano na kuzidisha mahusiano baina ya Mataifa, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(3),(e) inataja kuwa miongoni kwa kazi za Bunge ni "Kujadili na Kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa Masharti yake inahitaji Kuridhiwa".

Mheshimiwa Mwenyekiti, japokuwa ni jukumu la Bunge letu kufanya kazi hiyo, ni muhimu sana kufahamu umuhimu wa mbegu katika mustakabali mzima wa jamii yetu ya Kitanzania na pia katika uchumi wetu. Hatupingani na ukweli kuwa uzalishaji mazao unahitaji mbegu bora, lakini ni ukweli kwamba uzalishaji huo wa mbegu bora unaweza pia kupatikana ndani ya jamii zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo kuja kwa Azimio hili ni fursa kubwa kwa nchi yetu katika kuongeza jitihada za tafiti juu ya mbegu mbalimbali, kupanua masoko ya mbegu duniani hususani katika nchi za SADC, kuruhusu watafiti wetu, wagunduzi na wabunifu kupata hakimiliki za mbegu au mimea wanayoigundua, kuongeza ubora wa mbegu zetu na zaidi ya yote kuongeza ubora wa mbegu zetu za asili ili kupata mazao bora zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa moja ya malengo katika Azimio hili linasisitiza mashirikiano baina ya nchi wanachama na uwekaji wa mifumo ya kisheria katika kutoa hakimiliki kwa wagunduzi bado ndani ya mkataba huu haujazungumzia ipasavyo au kuangalia maslahi mapana ya kundi kubwa la wananchi ambao ni wakulima wadogo wadogo ambao pia wana aina zao za mbegu kulingana na mazingira yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa pamoja na malengo mazuri ya mkataba huu ambayo yanalenga

kuwasaidia na kuwalinda wagunduzi wa mbegu mbalimbali ni ukweli usiopingika kuwa umilikishaji wa mbegu kwa wagunduzi unatoa maana kwamba mnyororo mzima wa mbegu unakuwa ni kwa faida ya wagunduzi waliosajiliwa na kutambuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti,jambo hili la umiliki binafsi linaondoa utamaduni wa wakulima wadogo hususani maeneo ya vijijini kuweza kuendelea na utamaduni wa kubadilishana na kuuziana mbegu. Huu ni utamaduni ambao umekuwa ukitumika kwa miaka mingi. Tukumbuke kuwa kundi hili la wakulima wadogo ndilo kundi la wazalishaji wakubwa wa mazao ya chakula na yanayoingizwa mataifa yetu katika nchi wanachama wa *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo, utaratibu huu wa kutumia haki miliki usiporatibiwa vyema tutakuta wananchi wetu hususani vijijini wakipata tabu sana. Zipo jamii zenye aina za upekee wa mbegu kama vile maharage, karanga na kadhalika ambazo kimsingi kama jamii zinapaswa kupewa hakimiliki kunufaika ni vyema kama Taifa tukaliangalia jambo hilo kwa manufaa ya wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti,maslahi ya nchi nilazima yaanzie kwenye maslahi ya wananchi, kama jambo lolote tunalolifanya hapa Bungeni halina maslahi mapana kwa wananchi walio wengi ni dhahiri kwamba jambo hilo halitakuwa na maslahi yoyote kwa nchi pia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya Mkulima na Jamii katika kumiliki mbegu.Katika nchi nyingi zinazoendelea zimekuwa zikiweka masharti ya aina za mazao wanayohitaji kuyanunua. Hivyo, nchi hizo zimekuwa ndiyo wazalishaji wakubwa wa mbegu ambazo ndizo huingia katika nchi zinazoendelea (yaani ulimwengu wa tatu) bila kujali aina ya mazingira ikiwa ni pamoja na udongo, hali ya hewa na kadhalika mbegu hizo zimekuwa zikiuzwa kiholela kitendo ambacho kimeleta athari kubwa kwa mbegu zetu za asili, na pia athari za kimazingira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii yote ni kutokana na Mataifa mengi barani Afrika kukosa haki miliki za mazao yao, kutangaza na kuongeza thamani ya mbegu zao ili ziweze kuwanufaisha wananchi walio wengi ambao ni wakulima wadogo. Pamoja na mabadiliko makubwa yanayotokea katika sekta ya kilimo hususani masuala ya upatikanaji na uhifadhi wa mbegu bado nchi nyingi Barani Afrika hutumia mfumo wa asili ambao umejikita zaidi katika mila, desturi na tamaduni zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ni ukweli kwamba katika mfumo asilia mbegu huchaguliwa mapema kutoka shambani na kuhifadhiwa kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo. Taaluma na teknolojia inayotumika katika uchaguzi wa mbegu kutoka shambani, utunzaji wa mbegu hizo na njia zinazotumika katika kuuziana au kupeana ni jambo ambalo ni lazima liangaliwe vema katika mfumo mzima wa kisheria wa umiliki wa rasilimali za jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kuwa tumechelewa sana katika kuhakikisha mbegu zetu za asili zinaboreshwa na zinapata haki miliki ili kuhakikisha wakulima wanapata mazao mengi na bora. Lakini ni lazima tuweze kutambua changamoto zitakazokuja na mkataba huu kwa kuwa wakulima watalazimika kuendana na mahitaji ya soko. Ni dhahiri kuwa mkataba huu utachocheza tafiti nyingi za mbegu na hivyo mbegu za asili zitatoweka. Kutokana na umaskini au ugumu wa maisha ya wakulima wetu nchini, wengi wao watajikuta wanashindwa kumudu kilimo kutokana na kuongezeka kwa mahitaji katika kilimo ikiwa na maana ya manunuzi ya mbegu na madawa na mahitaji ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti,sambamba na hili ni lazima Serikali iweke mfumo mzuri ambao jamii nzima itaweza kunufaika endapo kama jamii hiyo imeweza kugundua mbegu za aina fulani. Hii ikiwa na maana kwamba jamii ikishirikiana kwa pamoja wanaweza kuwa mbegu waliyoifanyia utafiti kulingana na maeneo hayo. Hivyo, Serikali



haina budi kuhakikisha inaweka mazingira mazuri ili jamii za namna hii ziweze kunufaika ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuridhia mkataba huu Serikali pia ina wajibu mkubwa wa kuwaandaa watu wake katika soko la ushindani wa mbegu. Mpaka sasa kama nchi tujiulize tumewaandaa je watalaamu wetu wanaofanya tafiti za kilimo katika soko la ushindani? Bajeti zinazotolewa kwa ajili ya tafiti zote ni mashahidi kuwa bajeti hizo hazitoshelezi, vitendea kazi bado ni duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa ugani wengi wanafanya kazi katika mazingira duni sana. Maeneo mengi ya wakulima hayana ofisi za maafisa ugani. Hii inatoa tafsiri tosha ya kujipima kama Taifa kuwa tunapoenda kuridhia itifaki hii tumejiandaa je kupambana katika soko la ushindani wa mbegu ili kuhakikisha nchi yetu haitakuwa dampo la mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya changamoto kubwa tunayokumbana nayo katika sekta ya kilimo ni pamoja na ufinyu wa bajeti. Ukirejea kifungu cha 41 '*Financial Provisions*' Mkataba huu umezitaka nchi wanachama kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mkataba huu "*State Parties shall endeavor to allocate the necessary funds for the effective implementation of this Protocol at the National and Regional level.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mkataba huu kukazia upatikanaji wa fedha ni dhahiri katika bajeti za serikali zilizopita katika Sekta ya Kilimo ambayo ni sekta muhimu sana kwa uchumi na ustawi na Taifa letu kiasi cha fedha zilizotengwa na zinazotolewa ni kidogo sana. Mathalani, mwaka 2016/2017 fedha iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge ilikuwa kiasi cha shilingi bilioni 100.527 lakini mpaka Machi ni shilingi bilioni 2.2 tu ndio ilitolewa. Hali kadhalika kwa mwaka 2017/2018 ambapo ilitolewa asilimia 11 tu ya fedha za maendeleo zilizokuwa zimetengwa katika Sekta hiyo. Kwa mantiki hiyo, utekelezaji wa mkataba huu utakuwa ni mgumu endapo Serikali na Taasisi zake zinazoshughulika na kilimo

hazitafanya jitihada madhubuti ya kutafuta pesa ili kuinua Sekta hii ikiwa ni pamoja na kuwekeza ipasavyo katika tafiti za mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Azimio hili ambalo utekelezaji wake utaenda sambamba na Sheria yetu ya mwaka 2002 "*The Protection of New Plants (Plant Breeder's Act 2002)*" ambapo Sheria hii pia huangalia hakimiliki kwa jamii na mkulima, ni vema sana Serikali ihakikishe inawekeza ipasavyo katika elimu, tafiti, kutangaza na kutafuta masoko kwa ajili ya mbegu zetu. Hii itawasaidia wakulima wetu kupata mbegu bora zaidi, kupunguza uingizwaji wa mbegu nchini ambazo siyo rafiki kwa mazingira, itapunguza gharama kwa kuwa wakulima watapata mbegu zinazozalishwa hapa hapa nchini kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, pamoja na umuhimu wa kuridhia Itifaki hii ni vema Serikali ikaandaa na mfumo ambao utaongeza ushindani katika masoko ya mbegu. Serikali haina budi kuwekeza ipasavyo katika teknolojia na tafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali italazimika kuacha kuwekeza fedha nyingi katika miradi ambayo haina tija ya moja kwa moja na wananchi na badala yake kuwekeza ipasavyo katika miradi yenye tija kubwa kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuwekeza katika kilimo chenye tija, kuwekeza katika mifumo yenye kulinda maslahi ya wananchi wake katika masoko ya kimataifa na zaidi kuwekeza katika kuwasaidia wakulima wadogo wadogo ili kuondokana katika jinamizi la ujinga, umaskini na maradhi ambalo limeandama Taifa letu kwa kipindi cha miongo mingi tangu uhuru mpaka sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU AZIMIO LA KURIDHIA ITIFAKI YA JUMUIYA YA MAENDELEO YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA KUHUSU KULINDA HAKIMILIKI ZA WAGUNDUZI WA AINA MPYA ZA MBEGU ZA MIMBA (*The Protocol for Protection of New Varieties of Plants {Plant Breeder's Rights} in the Southern African Development Community-SADC*)- KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

**(Yanatolewa chini ya Kanuni ya 53 (6) (c) ya Kanuni za Bunge, toleo la mwaka 2016)**

**A. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa azimio hili ni dhahiri Tanzania haiwezi kujitenga na mataifa au jumuiya nyingine hasa katika kushirikiana kwenye masuala mbalimbali ya kiuchumi na kijamii.

**2. Mheshimiwa Spika**, katika kuliona hili la ushirikiano na kuzidisha mahusiano baina ya mataifa, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 63(3) (e) inataja kuwa miongoni kwa kazi za Bunge ni *“Kujadili na Kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa Masharti yake inahitaji Kuridhiwa”*.

**3. Mheshimiwa Spika**, japokuwa ni jukumu la Bunge letu kufanya kazi hiyo, ni muhimu sana kufahamu umuhimu wa mbegu katika mustakabali mzima wa jamii yetu ya Kitanzania na pia katika uchumi wetu. Hatupingani na ukweli kuwa uzalishaji mazao unahitaji mbegu bora, lakini ni ukweli kwamba uzalishaji huo wa mbegu bora unaweza pia kupatikana ndani ya jamii zetu.

**4. Mheshimiwa Spika**, hivyo kuja kwa azimio hili ni fursa kubwa kwa nchi yetu katika kuongeza jitihada za tafiti juu ya mbegu mbalimbali, kupanua masoko ya mbegu duniani hususani katika nchi za SADC, kuruhusu watafiti wetu, wagunduzi na wabunifu kupata hakimiliki za mbegu au mimea wanayoigundua, kuongeza ubora wa mbegu zetu na zaidi ya yote kuongeza ubora wa mbegu zetu za asili ili kupata mazao bora zaidi.

**B. MAELEZO YA UJUMLA**

5. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa moja ya malengo katika azimio hili linasisitiza mashirikiano baina ya nchi wanachama nauwekaji wa mifumo ya kisheria katika kutoa haki miliki kwa wagunduzi bado ndani ya mkataba huu haujazungumzia ipasavyo au kuangalia maslahi mapana ya kundi kubwa la wananchi ambao ni wakulima wadogo wadogo ambao pia wana aina zao za mbegu kulingana na mazingira yao.

6. **Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa pamoja na malengo mazuri ya mkataba huu ambayo yanalenga kuwasaidia na kuwalinda wagunduzi wa mbegu mbalimbali ni ukweli usiopingika kuwa umilikishaji wa mbegu kwa wagunduzi unatoa maana kwamba mnyororo mzima wa mbegu unakuwa ni kwa faida ya wagunduzi waliosajiliwa na kutambuliwa.

7. **Mheshimiwa Spika**, jambo hili la umiliki binafsi linaondoa utamaduni wa wakulima wadogo hususani maeneo ya vijijini kuweza kuendelea na utamaduni wa kubadilishana na kuuziana mbegu (*customary practices*).Huu ni utamaduni ambao umekuwa ukitumika kwa miaka mingi.Tukumbuke kuwa kundi hili la wakulima wadogo ndilo kundi la wazalishaji wakubwa wa mazao ya chakula na wanao yaingia kwenye mataifa yetu katika nchi wanachama wa SADC . Endapo, utaratibu huu wa kutumia haki miliki usiporatibiwa vyema tutakuta wananchi wetu hususani vijijii wakipata tabu sana. Zipo jamii zenye aina za upekee wa mbegu kama vile maharage, karanga n.k ambazo kimsingi kama jamii zinapaswa kupewa haki miliki ili kunufaika. Ni vyema kama taifa tukaliangalia jambo hilo kwa manufaa ya wananchi walio wengi.

8. **Mheshimiwa Spika**, maslahi ya nchi nilazima yaanzie kwenye maslahi ya wananchi, kama jambo lolote tunalolifanya hapa Bungeni halina maslahi mapana kwa wananchi walio wengi ni dhahiri kwamba jambo hilo halitakuwa na maslahi yoyote kwa nchi pia.

**C. HAKI YA MKULIMA NA JAMII KATIKA KUMILIKI MBEGU**

**9. Mheshimiwa Spika**, Katika nchi nyingi zilizoendelea zimekuwa zikiweka masharti ya aina za mazao wanayoyahitaji kuyanunua. Hivyo, nchi hizo zimekuwa ndio wazalishaji wakubwa wa mbegu ambazo ndizo huingia katika nchi zinazoendelea (ulimwengu wa tatu). Bila kujali aina ya mazingira ikiwa ni pamoja na udongo, hali ya hewa n.k mbegu hizo zimekuwa zikiuzwa kiholela kitendo ambacho kimeleta athari kubwa kwa mbegu zetu za asili, na pia athari za kimazingira.

**10. Mheshimiwa Spika**, hii yote ni kutokana na mataifa mengi barani Afrika kukosa haki miliki za mazao yao, kutangaza (promote) na kuongeza thamani ya mbegu zao ili ziweze kuwanufaisha wananchi walio wengi ambao ni wakulima wadogo. Pamoja na mabadiliko makubwa yanayotokea katika sekta ya kilimo hususani masuala ya upatikanaji na uhifadhi wa mbegu bado nchi nyingi barani Afrika hutumia mfumo wa asili ambao umejikita zaidi katika mila, desturi na tamaduni zetu.

**11. Mheshimiwa Spika**,ni ukweli kwamba katika mfumo asilia mbegu huchaguliwa mapema kutoka shambani na kuhifadhiwa kwa ajili ya msimu ujao wa kilimo. Taaluma na teknolojia inayotumika katika uchaguzi wa mbegu (mass selection- technology) kutoka shambani, utunzaji wa mbegu hizo na njia zinazotumika katika kuuziana au kupeana ni jambo ambalo ni lazima liangaliwe vyema katika mfumo mzima wa kisheria wa umiliki wa rasilimali za jamii.

**12. Mheshimiwa Spika**, ni wazi kuwa tumechelewa sana katika kuhakikisha mbegu zetu za asili zinaboreshwa na zinapata haki miliki ili kuhakikisha wakulima wanapata mazao mengi na bora. Lakini ni lazima tuweze kutambua changamoto zitakazokuja na mkataba huu kwa kuwa wakulima watalazimika kuendana na mahitaji ya soko. Ni dhahiri kuwa mkataba huu utachocheza tafiti nyingi za mbegu na hivyo mbegu za asili zitatoweka. Kutokana na umaskini au ugumu wa maisha ya wakulima wetu nchini ,

wengi wao watajikuta wanashindwa kumudu kilimo kutokana na kuongezeka kwa mahitaji katika kilimo ikiwa na maana ya manunuzi ya mbegu madawa na mahitaji ya umwagiliaji.

**13. Mheshimiwa Spika**, sambamba na hili ni lazima serikali iweke mfumo mzuri ambao jamii nzima itaweza kunufaika endapo kama jamii hiyo imeweza kugundua mbegu za aina fulani. Hii ikiwa na maana kwamba jamii ikishirikiana kwa pamoja wanaweza kuwa mbegu waliyoifanyia utafiti kulingana na maeneo hayo. Hivyo, serikali haina budi kuhakikisha inaweka mazingira mazuri ili jamii za namna hii ziweze kunufaika ipasavyo.

**14. Mheshimiwa Spika**, katika kuridhia mkataba huu serikali pia ina wajibu mkubwa wa kuwaandaa watu wake katika soko la ushindani wa mbegu. Mpaka sasa kama nchi tujjulize tumewaandaa je wataalamu wetu wanaofanya tafiti za kilimo katika soko la ushindani? Bajeti zinazotolewa kwa ajili ya tafiti zote ni mashahidi kuwa bajeti hizo hazitoshelezi, vitendea kazi bado ni duni n.k.

**15. Mheshimiwa Spika**, maafisa ugani wengi wanafanya kazi katika mazingira duni sana. Maeneo mengi ya wakulima hayana ofisi za maafisa ugani. Hii inatoa tafsiri tosha ya kujipima kama taifa kuwa tunapoenda kuridhia itifaki hii tumejiandaaje kupambana katika soko la ushindani wa mbegu ili kuhakikisha nchi yetu haitakuwa dampo la mbegu.

**16. Mheshimiwa Spika**, moja ya changamoto kubwa tunayokumbana nayo katika sekta ya kilimo ni pamoja na ufinyu wa bajeti. Ukirejea kifungu cha 41 'Financial Provisions' Mkataba huu umezitaka nchi wanachama kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mkataba huu "*State Parties shall endeavor to allocate the necessary funds for the effective implementation of this Protocol at the national and regional level*"

**17. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mkataba huu kukazia upatikanaji wa fedha ni dhahiri katika bajeti za serikali zilizopita katika sekta ya kilimo ambayo ni sekta muhimu sana

kwa uchumi na ustawi na taifa letu kiasi cha fedha zinazotengwa na zinazotolewa ni kidogo sana. Mathalani , mwaka 2016/2017 fedha iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge ilikuwa kiasi cha shilingi bilioni 100.527 lakini mpaka Machi ni shilingi bilioni 2.22 tu ndio ilitolewa. Hali kadhalika kwa mwaka 2017/2018 ambapo ilitolewa asilimia 11% tu ya fedha za maendeleo zilizokuwa zimetengwa katika sekta hiyo.Kwa mantiki hiyo, utekelezaji wa mkataba huu utakuwa ni mgumu endapo serikali na taasisi zake zinazoshulika kilimo hazitafanya jitihada madhubuti ya kutafuta pesa ili kuinua sekta hii ikiwa ni pamoja na kuwekeza ipasavyo katika tafiti za mbegu.

**18. Mheshimiwa Spika,** pamoja na azimio hili ambalo utekelezaji wake utaenda sambamba na sheria yetu ya Mwaka 2002" The Protection of New Plants (Plant Breeder's Act 2002) ambapo Sheria hii pia huangalia hakimiliki kwa jamii na Mkulima, ni vyema sana serikali ihakikishe inawekeza ipasavyo katika elimu, tafiti, kutangaza na kutafuta masoko kwa ajili ya mbegu zetu. Hii itawasaidia wakulima wetu kupata mbegu bora zaidi, kupunguza uingizwaji wa mbegu nchini ambazo sio rafiki kwa mazingira, itapunguza gharama kwa kuwa wakulima watapata mbegu zinazozalishwa hapa hapa nchini kwa bei nafuu.

#### **D. HITIMISHO**

**19. Mheshimiwa Spika,** pamoja na umuhimu wa kuridhia Itifaki hii; ni vyema Serikali ikaandaa na mfumo ambao utaongeza ushindani katika masoko ya mbegu. Serikali haina budi kuwekeza ipasavyo katika teknolojia na tafiti. Serikali italazimika kuacha kuwekeza fedha nyingi katika miradi ambayo haina tija ya moja kwa moja kwa wananchi na badala yake kuwekeza ipasavyo katika miradi yenye tija kubwa kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuwekeza katika kilimo chenye tija, kuwekeza katika mifumo yenye kulinda maslahi ya wananchi wake katika masoko ya kimataifa na zaidi kuwekeza katika kuwasaidia wakulima wadogo wadogo ili kuondokana katika jinamizi la ujinga, umaskini na maradhi ambalo limeandama taifa letu kwa kipindi cha miongo mingi tangu uhuru mpaka sasa.

**20. Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....  
Pascal Yohana Haonga (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI  
KATIKA WIZARA YA KILIMO**

10 Septemba, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara ili awasilishe Azimio la Kuridhia Itifaki ya *Marrakesh* inawezesha upatikanaji wa kazi zilizochapishwa kwa watu wasioona wenye uoni hafifu na ulemavuunaofanya mtu kushindwa kusoma mwaka wa 2013. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri dakika kumi.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Azimio la Kuridhia Mkataba wa *Marrakesh* wa mwaka 2013 unaowezesha upatikanaji wa kazi zilizochapishwa kwa watu wasioona wenye uoni hafifu au ulemavu unaomfanya mtu kushindwa kusoma yaani (*The Marrakesh Treaty To Facilitate Access To Publish Work For Persons Who Are Blind Visually Impaired or Otherwise Print Disabled*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Kimataifa wa *Marrakesh* unazingatia Kanuni Tano za haki za Binadamu ambazo ni, Kutobagua, kutoa fursa sawa kwa wananchi, ufikikaji yaani *accessibility* ushiriki kikamilivu kwa wasioona katika shughuli za kijamii na kuendeleza ushirikiano wa Kimataifa kutekeleza malengo ya watu wenye ulemavu wa kuona duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maandalizi ya kuridhia Mkataba huu Serikali imeshirikisha Wadau mbalimbali



kutoka Tanzania bara na Zanzibar Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao maoni yao yalisaidia sana katika kupata uelewa mpana na kuweka mkakati wa namna bora ya kutekeleza Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa *Marrakesh* unazingatia Ibara za 11(1)(3) na Ibara ya 18(2) za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania zinazoelekeza haki ya kila mtu kupata elimu na taarifa kuhusu matukio mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo makuu ya Mkataba wa Kimataifa wa *Marrakesh* ni kuwawezesha watu wasioona kabisa na wale wenye huoni hafifu kupata na kutumia kazi za uandishi zilizochapishwa kwa wino wa kawaida kwenye miundo mbadala inafikika kwao, kama vile maandishi ya nukta nundu yaani *brelly* kurekodi katika sauti, kuwekwa katika maandishi yaliyokuzwa n.k.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa nafasi ya kipekee kabisa napenda kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuwajali ndugu zetu wenye ulemavu nchini, katika kulithibitisha hilo uteuzi wa Naibu Waziri Mheshimiwa Stella Ikupa, uteuzi wa Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi Balazi wa Tanzania Nchini Ujerumani, uteuzi wa Bwana Amon Mpanju kuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na Watendaji wengine ndani ya Serikali ni kielelezo cha jinsi gani Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali ya Awamu ya Tano anayoiongoza inavyotekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa kujali wananchi wote wakiwemo ndugu zetu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uandaaji na utekelezaji wa Mkataba wa *Marrakesh* upo kwenye Awamu Mbili za utekelezaji kwanza ni kuandaa na kukamilisha mchakato wa kusaini na kuridhia Mkataba Bungeni jambo ambalo ni matumaini yangu kwamba Waheshimiwa Wabunge mtatusaidia kukamilisha hatua hii leo hii kwenye Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hatua ya pili ni kuwasilisha nyenzo ya kuridhiwa na Bunge kwenye Makao Makuu ya Shirika la Miliki bunifu Duniani yaani *World Intellectual Property Organization* lililopo Geneva Switzerland kwa ajili ya kusajiliwa rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kuwasilisha Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Marrakesh ya Mwaka 2013 kama ifuatavyo:-

KWA KUWA,Tanzania ni nchi Mwanachama wa Shirika la Miliki Bunifu Duniani yaani *World Intellectual Property Organization* Wipe ambapo ilijunga na Shirika hilo mwaka 1983, Shirika hilo linasimamia masuala ya Miliki Bunifu Duniani ambayo ni miundo bunifu yaani *Industrial property* na haki miliki yaani *copyright* na kwa kuwa Tanzania ni nchi mwanachama iliyoshiriki Mkutano wa Marrakesh Morocco tarehe 27 Juni mwaka 2013 ambao ulipitisha Mkataba huu unaowezesha upatikanaji wa kazi zilizochapishwa kwa watu wasioona wenye uoni hafifu au ulemavu unaomfanya mtu kushindwa kusoma kwa njia rahisi;

NA KWA KUWA,Tanzania ilikubaliana na Mkataba huu lakini haikutia saina kwa mujibu wa Ibara ya 17 ya Mkataba huu kwa lengo la kujipa muda ili kupata maoni ya wadau;

NA KWA KUWA,Mkataba wa Marrakesh unaendana na Mikataba mbalimbali ambayo Tanzania imekwisha ridhia ikiwemo Mkataba wa Berne wa Ulinzi wa Kazi za Maandishi na Kazi za Sanaa (*Berne Convection for the Protection of Literally and Artistic Works of 1986*) na makubaliano kuhusu Malengo Yanayohusu Sanaa na Biashara za Miliki Bunifu (*The Trade Related Aspects of Intellectual Property Agreement Treaty*);

NA KWA KUWA,Mkataba wa Berne na *TRIPS*kwa pamoja ina lengo la kusimamia kazi zinazolindwa na Hakimiliki katika kuzalisha, kutafsiri na kusambaza kazi za maandishi ambapo mtu yeyote haruhusiwi kutumia kazi za Hakimiliki bila idhini au kutoa malipo kwe mwenye Hakimiliki;

NA KWA KUWA, lengo la Mkataba huu ni kuwezesha wasioona, wenye uoni hafifu na wenye ulemavu wa kusoma kupata kazi zilizochapishwa katika muundo unaofikika, kutoa uelewa wa masuala mbalimbali juu ya changamoto za upatikanaji taarifa na habari katika muundo rafiki kwa walengwa, kuwezesha walengwa kupata elimu na vifaa vya kujifunzia yaani vitabu, kufanya tafiti na mawasiliano kufikia kazi andishi zilizochapishwa katika muundo unaofikika na kuimarisha uchangamano na ushirikiano katika shughuli za kijamii na za kiutamaduni;

NA KWA KUWA, Mkataba huu unatoa fursa ya upendeleo wa pekee kwenye Sheria za Hakimiliki ili kuruhusu uzalishaji, usambazaji na kuwezesha upatikanaji wa kazi zilizochapishwa katika mfumo wa rafiki kwa walengwa;

NA KWA KUWA, Tanzania kwa kuridhia mkataba huu na hatimaye kuutekeleza itanufaika na mambo yafuatayo:-

- (a) Kuwezesha upatikanaji wa elimu kwa njia rahisi;
- (b) Kuwezesha ubadilishanaji wa kazi nan chi nyingine;
- (c) Kujenga uelewa wa namna ya kutatua changamoto mbalimbali zinazowapata wasioona na wenye uoni hafifu wakati wakitafuta elimu;
- (d) Kuondoa umaskini na kuchangia katika pato la Taifa;
- (e) Kujenga uelewa katika masuala ya haki miliki;
- (f) Kurahisisha upatikanaji wa vitabu, magazeti na vitu vingine vinavyowasaidia walengwa katika kupata uelewa wa masuala ya kijamii; na
- (g) Kuwezesha mwingiliano wa kijamii katika jamii ya wasioona, wenye uoni hafifu na jamii isiyo na ulemavu huo.

HIVYO BASI, kwa kuzingatia manufaa yanayotokana na mkataba huu, Bunge hili katika Mkutano wa Kumi na Sita

na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, sasa linaazimia kuridhia mkataba wa *Marrakesh* wa mwaka 2013, unaowezesha upatikanaji wa kazi zilizochapishwa kwa watu wasioona, wenye uoni hafifu na ulemavu unaomfanya mtu kushindwa kusoma (*The Marrakesh Treaty, to Facilitate Access to Published Works for persons who are Blind, visually impaired or otherwise print disabled*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imeungwa mkono. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira, atawasilisha taarifa ya Kamati kuhusu azimio hilo dakika kumi! (*Makofi*)

**MHE. KITETO Z. KONSHUMA - K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE, VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Viwanda, Biashara na Mazingira, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Mkataba wa *Marrakesh* wa mwaka 2013, unaolenga kuwezesha upatikanaji wa kazi zilizochapishwa kwa watu wasioona, wenye uoni hafifu au ulemavu unaomfanya mtu kushindwa kusoma (*The Marrakesh Treaty to Facilitate Access to Published Works for Persons who are Blind, Visually Impaired or Otherwise Print Disabled 2013*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6)(b), ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa *Marrakesh* unaolenga kuwezesha upatikanaji wa kazi zilizochapishwa kwa watu wasioona, wenye uoni hafifu au ulemavu unaomfanya mtu kushindwa kusoma wa Mwaka 2013 (*The Marrakesh Treaty to Facilitate Access to*

*Published Works for Persons who are Blind, Visually Impaired or Otherwise Print Disabled 2013).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia masharti ya fasili ya 6(b), Kifungu cha 53 ikisomwa pamoja na fasili ya 1(b) ya Kifungu cha 7, cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira ina jukumu la kushughulikia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Hoja ya Serikali kuhusu Bunge kuridhia Azimio la Kuridhia Mkataba wa *Marrakesh* ililetwa kwenye Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa mujibu wa Kanuni ya 53(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Kamati ililijadili na kulichambua na hatimaye kuja na maoni na ushauri ambao Kamati imeutoa kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna Kamati ilivyoshughulikia hoja hii, baada ya hoja hii kuwasilishwa kwenye Kamati, Kamati ilikutana katika Ofisi za Bunge Dodoma ambapo ilitekeleza shughuli zifuatazo kwa ajili ya kuwezesha uchambuzi wa kina wa Mkataba huu:-

(i) Semina ya kujengea uelewa Kamati juu ya Mkataba wa *Marrakesh*, ambapo tarehe 31 Agosti, 2019, Wizara ya Viwanda na Biashara iliwapitisha wajumbe katika Mkataba husika. Semina hii iliwezesha Kamati kupata uelewa na kuiweka katika nafasi nzuri ya kuifanyia kazi hoja hii na hatimaye kutoa maoni yake;

(ii) Kupokea Maelezo ya Serikali juu ya pendekezo la Kuridhia Mkataba wa *Marrakesh* wa Mwaka 2013 ambapo tarehe 4 Septemba, 2019 Kamati ilikutana na kupata maelezo ya Serikali kuhusu pendekezo la Kuridhia Azimio la Kuridhia Mkataba wa *Marrakesh*, maelezo hayo yaliyowasilishwa na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara yalifafanua nia ya Serikali kutaka kuingia mkataba huu kwa lengo la kutatua

changamoto ambayo wamekuwa wakikabiliana nayo walengwa wa Mkataba huu;

(iii) Kupokea Maoni ya Wadau, katika kutekeleza jukumu hili Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117 (9) kuhusu utaratibu wa kuwaalika wadau, wadau waliokuwa na maoni juu ya Mkataba wa *Marrakesh* walipata fursa ya kuyawasilisha. Kamati iliwashukuru wadau waliofanikiwa kuwasilisha maoni yao kuhusu Mkataba huu, maoni yenu yalisaidia kuboresha maoni ya Kamati kuhusu Mkataba huu na hatimaye kuishauri Serikali kwa lengo la kuboresha utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chimbuko la Itifaki, Mkataba wa *Marrakesh* unatekelezwa na Nchi Wanachama wa *WIPO* (*World Intellectual Property Organization*) ambapo Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ni Mwanachama. Mnamo tarehe 27 Juni, 2013 nchi wanachama wa *WIPO* walishiriki katika mkutano uliofanyika mjini *Marrakesh - Morocco* kwa lengo la kujadili na kupata muafaka wa kuwasaidia watu wenye ulemavu wa macho kuweza kupata haki ya kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kikao hicho kilipitisha azimio la kuanzishwa kwa Mkataba wa *Marrakesh* ambao ulilenga kuweka jitihada za pamoja ambazo zinatoa fursa ya upendeleo na upekee kwenye Sheria ya Hakimiliki ili ziruhusu uzalishaji, usambazaji na kuwezesha upatikanaji wa kazi za uandishi kuwa katika mifumo rafiki kwa watu wenye uoni haffu, wasioona na wenye ulemavu unaowapelekea kutokusoma kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya msingi yaliyozingatia na kamati, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza madaraka yake ipasavyo kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(e), kamati ilizingatia mambo mbalimbali yaliyo muhimu katika kuifanyia kazi hoja ya Serikali iliyo mezani leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati iliangalia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na baadhi ya Sheria za

nchi zinazohusiana moja kwa moja na maudhui ya Mkataba unaopendekezwa. Kamati ilibaini kuwa Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania inaelezea haki ya kupata habari na taarifa muhimu katika jamii, hivyo basi kuridhiwa kwa Mkataba huu kutawezesha wanufaika kupata haki ya kikatiba. Vilevile, Kamati ilitafakari na kujiridhisha juu ya Faida zinazoweza kupatikana kutokana na kuridhia kama ulivyo. Faida hizo ni pamoja na;-

- (i) Kujenga uelewa wa namna ya kutatua changamoto mbalimbali zinazowapata wasioona na wenye uoni hafifu wakati wa kutafuta elimu;
- (ii) Kurahisisha upatikanaji wa vitabu, magazeti na vitu vingine vitanavyowasidia walengwa katika kupata uelewa wa masuala ya kijamii; na
- (iii) Kuongeza ushiriki wa jamii ya wasioona na wenye uoni hafifu katika shughuli za kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati pia ilizingatia hasara au madhara yanayoweza kupatikana kwa kuridhia Mkataba huu ambapo haikuona madhara ya moja kwa moja yatokanayo na kuridhia Mkataba huu. Madhara ambayo yalikuwa yakitazamwa ni kuwa mkataba ungeweza kuruhusu uingizaji wa vitabu na machapisho ambayo yanapingana na mila na desturi zetu. Hofu hii imeondolewa na Ibara ya 12 ya Mkataba ambayo imeelezea kuwa, ubadilishanaji wa nakala za vitabu na machapisho baina ya nchi utazingatia Sheria, taratibu na utamaduni wa kila nchi inayohitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nanukuu: *Article 12(1)*  
*“Contracting parties recognize that a contracting Party may implement in its National Law, other copyright limitation and exception for the benefit of beneficiary persons than are provided by this Treaty having regard to that Contracting Party’s economic situation and its social and cultural needs in conformity with that Contracting Party’s international rights and obligations and in the case of a least-developed country taking into account its special needs and its particular*

*international rights and obligations and flexibilities thereof".*  
Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kamati ilijiridhisha hatua zilizofikiwa katika Mkataba huu ambapo ilibaini kuwa Mkataba ulianza kutekelezwa rasmi tarehe 30 Septemba, 2016 ambapo ilikuwa ni miezi mitatu (3) baada ya nchi mwanachama wa Ishirini (20) kuwasilisha Hati ya Kuridhia, kama inavyoelekezwa na Ibara ya 18 ya Mkataba. Nanukuu, *Article 18 "The Treaty shall enter into force three months after 20 eligible parties referred to Article 15 have deposited their instruments of ratification or accession".* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba pia unaruhusu Nchi Mwanachama kujitoa, na hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 20 ya Mkataba, kipengele hiki kinatoa Haki kwa Nchi Mwanachama kujitoa. Hii inatoa uhuru kwa wanachama wake pale wanapohisi hawanufaiki na mkataba. Nchi Mwanachama yenye kusudio la kujitoa itawasilisha ombi la kujitoa kwa Mkurugenzi Mkuu wa *WIPO* na ombi hilo litakubaliwa mwaka mmoja baada ya ombi hilo kuwasilishwa. Nanukuu, *Article 20'' This Treaty may be denounced by any Contracting Party by notification addressed to the Director General of WIPO. Any denunciation shall take effect one year from the date on which the Director General of WIPO receives the notification''.* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilitaka kujiridhisha kuhusu uhusiano wa Mikataba mingine ya Kimataifa ambayo inashabihiana na Mkataba wa *Marrakesh*. Ibara ya 1 ya Mkataba inafafanua kuwa hakuna kitakachobadili jukumu lolote ambalo nchi mwanachama imejifunga na mkataba. Nanukuu, *Article 1 "Nothing in this Treaty shall derogate from any obligation that Contracting Parties have to each other under any other treaties, nor shall it prejudice any right that a Contracting Party has under any other treaties"* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati, Mkataba wa *Marrakesh* unalenga kuwezesha watu



wasioona, wenye uoni hafifu au ulemavu unaomfanya mtu kushindwa kusoma kupata kazi zilizochapishwa kwa njia rahisi (maandishi ya nukta nundu, sauti zilizorekodiwa na maandishi yaliyokuzwa). Vilevile Mkataba huu unalenga kutoa uelewa wa masuala mbalimbali juu ya changamoto za upatikanaji wa taarifa na habari katika muundo rafiki kwa walengwa. Pia unawawezesha walengwa kupata elimu na vifaa vya kujifunzia jambo ambalo litaongeza na kuimarisha ushiriki wao katika shughuli za kijamii na utamaduni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa Mkataba huu, naomba nilishawishi Bunge lako Tukufu kuridhia Mkataba huu kwa lengo la kuwasaidia walengwa kuanza kunufaika. Pia naomba nitoe maoni na mapendekezo ya Kamati ambayo yamegusa maeneo ambayo Kamati inaona ni muhimu Serikali ikayazingatia kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 4 ya Mkataba inapingana na Sheria ya Hakishiriki na Hakishirikishi ya Mwaka 1999 ambayo inazuia upatikanaji wa Kazi zilizochapwa kuwekwa kwenye muundo unaofikika kwa wanufaika kama inavyotakiwa kwenye Mkataba wa *Marrakesh*. Kwa kuwa tunaenda kuridhia Mkataba huu Kamati inaitaka Serikali kukamilisha mchakato wa marekebisho wa Sheria ya Hakimiliki ili kuhakikisha Sheria hiyo inaendana na masharti ya ibara hii kwa lengo la kutoa fursa kwa wanufaika kuanza kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 4(5) ya Mkataba imeweka wazi kazi yoyote itakayochapishwa chini ya mkataba huu isifanyiwe biashara yaani isiuzwe, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha wanufaika wanapewa elimu juu ya sharti hili la mkataba.

Pia Serikali ihakikishe chombo kitakachopewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa mkataba huu kinakuwa na uwezo wa kufuatilia na kujiridhisha kuwa sharti hilo linazingatiwa na walengwa wanapata huduma. Vilevile kamati inashauri kuwa kama itabainika kuuzwa kazi ambazo

zimetolewa kwa ajili ya kuwanufaisha walengwa, hatua za kisheria zifuatwe kwa lengo la kukomesha vitendo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, naomba nikushukuru sana wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri na kwa kunipa ruhusa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa uongozi wake mahili pamoja na Naibu Spika, pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuratibu na kusimamia shughuli za Bunge kwa umakini na umahiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mbunge, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima Mbunge, Makatibu Wakuu, pamoja na wataalam wote wa Ofisi hii muhimu kwa ushirikiano waliutoa wakati wa kujadili Azimio hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa, kwa niaba ya Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano waliutoa wakati wa kupitia kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni yake juu ya Azimio hili mbele ya Bunge hili tukufu. Orodha yao ni kama inavyosomeka hapa chini na kwa ruhsa yako naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai; Mkurugenzi wa Idara ya Kamati Bwana Athumani Hussein; Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Fedha na Uchumi Bwana Michael Chikokoto; Makatibu wa Kamati Bi. Zainabu Mkamba na Bi. Mwajuma Ramadhani pamoja na Msaidizi wa Kamati Bi. Paulina Mavunde kwa kuratibu vema shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono Azimio. *(Makofi)*

**TAARIFA KUHUSU AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA ITIFAKI YA  
MAENDELEO YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA KUHUSU  
KULINDA HAKIMILIKI ZA WAGUNDUZI WA AINA MPYA ZA  
MBEGU ZA MIMEA (THE PROTOCOL FOR PROTECTION OF NEW  
VARIETIES OF PLANT [PLANT BREEDER'S RIGHTS] IN THE  
SOUTHERN AFRICAN DEVELOPMENT COMMUNITY – SADC) –  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## **6.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 53 (6) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, naomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika Kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (*The Protocol for Protection of New Varieties of Plant [Plant Breeder's Rights] In The Southern African Development Community – SADC*).

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa Itifaki hii inahusu Nchi Wanachama zilizo Kusini Mwa Afrika (SADC), kabla ya kuanza wasilisho langu, kwa niaba ya Kamati naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Nchi za SADC. Kamati inaamini kutokana na uwezo wake mahiri pamoja na mambo mengine Wagunduzi wa Tanzania na wenzao kutoka nchi Wanachama wa SADC watanufaika na maudhui yalimo kwenye Itikafi hii.

**Mheshimiwa Spika**, Nyongeza ya Nane Kifungu cha 7(1) (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, inazipa Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji jukumu la kushughulikia Miswada ya Sheria, Maazimio na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyo chini ya Wizara inazozisimamia. Aidha, jukumu hili pia ni jukumu la Kikatiba chini ya Ibara ya 63(3)(e) ya

Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 12 Novemba, 2018 uliiletea Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kazi ya kushughulikia Azimio la Bunge la kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika (*The Protocol For Protection of New Varieties of Plant [Plant Breeder's Rights] In The Southern African Development Community – SADC*) kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea kama lilivyowasilishwa na Serikali ili Kamati iweze kuchambua mapendekezo ya Azimio husika na hatimae kutoa maoni na ushauri kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyo ada, Kamati ilianza kuchambua Itifaki husika kwa kushirikiana na wadau waliofika mbele ya Kamati na wale waliotuma maoni yao kwa njia ya maandishi ili kufahamu madhumuni na faida zinazoambatana na kuridhiwa kwa Itifaki hii. Hata hivyo, baada ya kushauriana na Serikali ilibainika kuna umuhimu wa kuongeza muda ili Kamati iweze kufanyia kazi zaidi ili matokeo chanya yaliobainishwa kwenye Itifaki hii yaweze kuleta maslahi kwa wananchi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, kwa hekima na busara uliridhia kuongezwa kwa muda wa kushughulikiwa kwa Itifaki hii ambapo tarehe 28 Agosti, 2019 uliiletea tena Kamati kazi ya kushughulikia Itifaki tajwa. Tarehe 04 Septemba, 2019 Kamati ilianza kazi ya kushughulikia Itifaki hii ambalo liliwasilishwa mbele ya Kamati na Naibu Waziri wa Kilimo Mhe. Omary Mgumba, (Mb).

## 7.0 MADHUMUNI/MALENGO YA ITIFAKI

**Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 2 ya Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika (SADC) kuhusu kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea ina madhumuni ya msingi yafuatayo: -

(a) Kuwezesha kuanzisha mfumo thabiti wa kulinda hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea;

**(b)** Kuendeleza na kuhamasisha ugunduzi wa aina mpya za mbegu za mazao ya mimea kwa manufaa ya nchi wanachama katika Jumuiya ya SADC; na

**(c)** Kutoa Hakimiliki kwa Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea.

## **8.0 UCHAMBUZI WA ITIFAKI**

**Mheshimiwa Spika**, Itifaki hii imegawanyika katika sehemu kuu kumi (10) na ina jumla ya Ibara 50 ambazo maudhui yake ni kama ifuatavyo: -

### **Sehemu ya Kwanza**

**Ibara ya 1** ya Itifaki inahusu masharti ya jumla ambayo inaanzia Ibara ya 2 hadi ya 6.

**Ibara ya 2** inahusu madhumuni ya Itifaki ambayo yameelezwa hapo juu.

**Ibara ya 3** inahusu mawanda na maeneo ambayo itifaki hii itatumika.

**Ibara ya 4** ya itifaki inaanzia Ofisi ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Mbegu za Mimea katika Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) ambayo itakuwa na jukumu la kusimamia utekelezaji wa itifaki hii.

**Ibara ya 5** ya itifaki inaanzia Kamati ya Ushauri ya SADC kwa ajili ya kuishauri Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki za Wagunduzi wa Mbegu za Mimea katika mambo ya jumla na mahsus kuhusiana na utekelezaji wa majukumu yake na mambo mengine yanayohusiana na itifaki hii.

**Ibara ya 6** inaanzia Rejista ya Usajili wa Hakimiliki kwa Wagunduzi wa Mbegu za Mimea ambayo itatunzwa na Msajili.

### **Sehemu ya Pili**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ya itifaki inaanzia **Ibara ya 7 hadi 11** na inahusu masharti ya utoaji wa Hakimiliki za

Ugunduzi ambapo ibara hizo zimefafanua kwa undani vigezo vitakavyotumika kutoa hakimiliki hizo.

### **Sehemu ya Tatu**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya tatu ya itifaki imeanzia **Ibara ya 12 hadi 22** ambapo ibara hizi zimeweka utaratibu wa jinsi ya kutuma maombi ya kupewa hakimiliki ya ugunduzi wa mbegu za mimea. Aidha, ibara hizi zimefafanua kiundani watu wanaostahili kuomba hakimiliki, utaratibu wa kutuma maombi, haki ya kipaumbele katika kushughulikia maombi pamoja na mambo mengine yanayoendana na maombi ya hakimiliki.

### **Sehemu ya Nne**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya nne inaanzia **Ibara ya 23 hadi 25** na inaeleza vigezo ambavyo vitatumika katika kufikiria maombi ya utoaji hakimiliki.

### **Sehemu ya Tano**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inahusu **Ibara ya 26 hadi 31** na inaeleza kuhusu haki za mmiliki wa hakimiliki. Aidha ukomo wa muda wa matumizi ya hakimiliki kwa mbegu za miti umeelezwa utakuwa miaka ishirini na tano (25) tangu siku ya kutolewa na kwa mbegu nyingine za mimea ukomo wa hakimiliki utakuwa miaka ishirini (20). Hata hivyo ukomo wa muda kwa mbegu nyingine za mimea, unaweza kuongezwa na Msajili kutokana na mapendekezo yatakatolewa kwake na Kamati inaweza kuongeza muda usiozidi miaka mitano (5).

### **Sehemu ya Sita**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ambayo ina **Ibara ya 32 na 33**, inaelezea kuhusu utoaji wa leseni zinazohusiana na uzalishaji wa mbegu za mimea kutoka kwa mmiliki wa hakimiliki ya Wagunduzi wa mbegu za mimea.

### **Sehemu ya Saba**

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ina **Ibara moja** ambayo ni ya **34** na inaweka masharti kuhusu uhamishaji wa hakimiliki ya Wagunduzi wa mbegu za mimea.

### Sehemu ya Nane

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ina **Ibara ya 35, 36, na 37** na inaeleza utaratibu wa kurudisha, kubatilisha na kufutwa kwa hakimiliki.

### Sehemu ya Tisa

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii ina **Ibara moja ya 38** ambayo inaanzisha Bodi ya Rufaa kwa ajili ya rufaa kwa mtu ambae hataridhika na maamuzi ya Msajili.

### Sehemu ya Kumi

**Mheshimiwa Spika**, sehemu ya kumi inaanza **Ibara ya 39 hadi 50** inaelezea masharti ya jumla ikiwemo utungaji wa Kanuni na taratibu za uendeshaji wa Itifaki, kulinda aina za mbegu ambazo zilikuwepo kabla ya Itifaki hii, masuala ya fedha, marekebisho ya Itifaki hii, utatuzi wa migogoro, utaratibu wa nchi kujiondoa katika Itifaki hii, utiaji saine wa Itifaki hii, utaratibu wa kuridhia, kuanza kutumika kwa Itifaki, uwasilishwaji wa Hati Idhini na Utekelezaji wa Itifaki.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Kamati kufanya uchambuzi kwenye sehemu hizo za Itifaki, Kamati ilitaka kujiridhisha kwenye maeneo ya msingi na hivyo kuhitaji ufafanuzi kwenye maeneo hayo ambayo ni pamoja na:-

i) Kwa nini nchi zenye uchumi mkubwa na ambazo zinafanya vizuri katika tasnia ya mbegu na kilimo kama Afrika kusini, Aidha nchi za Mauritius na Shelisheli ambazo zina uchumi mkubwa hazijasaini Itifaki hii?.

ii) Kuna uharaka gani wa kuridhia Itifaki hii wakati ni nchi saba (7) tu kati ya nchi kumi na tano (15) wanachama wa SADC ndio zimesaini Itifaki hii?.

iii) Je Itifaki hii haiwezi kusababisha ukiritimba (*monopoly*) kutoka katika makampuni makubwa ya mbegu katika tasnia ya mbegu?.

iv) Je vituo vya Afrika kwa ajili ya maswala ya hakiubunifu vya ARIPO (Harare-Zimbabwe), OAPI (Africa Magharibi) na

PAIPO (Chini ya Umoja wa Afrika) haviwezi kuingiliana na kusigana na Itifaki hii?.

v) Ni kwa kiasi gani uhuru wa mkulima mdogo katika uzalishaji mbegu umezingatiwa kwenye Itifaki hii?.

vi) Ni kwa kiasi gani kama nchi tumewekeza katika tafiti za mbegu ili kuweza kumudu ushindani wa nchi Wanachama wa SADC katika ugunduzi, uzalishaji na biashara ya mbegu;

vii) Ni kwa kiasi gani Itifaki hii imezingatia utofauti wa maendeleo ya kiuchumi uliko miongoni mwa nchi wanachama wa SADC? na

viii) Je kuna ulazima gani wa kuridhia Itifaki ya SADC wakati katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ambayo Tanzania ni mwanachama haina utaratibu wa Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Mbegu?.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako kuwa Kamati imeridhishwa na ufafanuzi uliotolewa na Serikali kuhusu hoja zilizoibuliwa na Wabunge. Aidha, Kamati ilifanya kikao na Wagunduzi na Watafiti wa mbegu waliotoka Serikalini na katika Sekta Binafsi ambao Itifaki hii inawagusa moja kwa moja. Kupitia mjadala huu wadao hao waliakikishia Kamati kuwa kuridhiwa kwa Itifaki hii kutakuwa na manufaa yafuatayo: -

- Serikali itanufaika na fedha ilizowekeza kwenye utafiti wa mbegu kwa kulinda kazi za utafiti wa mbegu zilizozalishwa na wataalamu wake;
- Uwepo wa mrabaha utakaopatikana kutokana na gawio ambapo Serikali itapata mapato yatakayotokana na gawio, mgunduzi atapata gawio na kiasi kingine cha mrabaha kitatumika kuendeleza ugunduzi wa aina mpya za mbegu;
- Kuongeza motisha kwa Watafiti na Wagunduzi wa mbegu na hivyo kuongeza uzalishaji wa mbegu ambazo zitatumika nchini na zingine kuuzwa nje ya nchi na hivyo kuongeza



mapato ya Serikali pamoja na kupunguza gharama kubwa ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mbegu nje ya nchi;

- Kuongezeka kwa ushindani na ubunifu miongoni mwa Wafatiti/Wagunduzi wa mbegu
- Kutarahisisha upatikanaji wa mbegu bora na mpya kwa haraka na
- Kuridhiwa kwa Itifaki hii kutaongeza uzalishaji wa chakula kwa kuwa wakulima watapata mbegu bora na mpya na hivyo kuhakikishia taifa usalama wa chakula.

## 9.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kufanya uchambuzi wa Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika Kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea, Kamati inakubaliana na dhamira njema ya Itifaki hii kwa Taifa na kwa Wagunduzi wa ndani. Pamoja na dhamira njema iliyopo, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao: -

(a) Serikali itenge fedha za kutosha kwa ajili ya vituo vya utafiti ili kuwezesha watafiti kufanya tafiti kwa kutumia fedha zetu za ndani na sio kama ilivyo sasa ambapo tafiti nyingi hufanyika kwa kutegemea fedha kutoka kwa wadau wa maendeleo. Bila ya kuwezesha vituo vya utafiti na wagunduzi wa mbegu, Itifaki hii inaweza kunufaisha wagunduzi wa mbegu kutoka mataifa mengine na sisi kubaki kuwa watazamaji tu.

(b) Ni muhimu kwa Sera na Sheria zinazohusiana na Mbegu zikafanyiwa mapitio ili ziweze kuendana na maudhui ya Itifaki hii.

(c) Serikali ifanye mapitio na maboresho ya Sheria ya Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea ya Mwaka 2012 ili Sheria hii iweze kujumuisha maudhui ya Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa

Afrika na kurekebisha baadhi ya mapungufu yaliyoko kwenye Sheria ikiwa ni pamoja na kipengele kinachoeleza Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu kutovuka mipaka ya Tanzania.

(d) Serikali iweke mazingira wezeshi kwa ajili ya kuvutia uzalishaji mbegu nchini. Uzalishaji mbegu, pamoja na mambo mengine utaongeza:-

- Motisha kwa wagunduzi wa mbegu kugundua aina mpya za mbegu;
- Kuokoa fedha nyingi za kigeni zinazotumika kuagiza mbegu nje ya nchi – kiasi cha shilingi bilioni 860 hutumika kuagiza mbegu kutoka nje ya nchi na
- Kuongezeka kwa mapato ya Serikali, ajira na ujuzi kwa wananchi wazawa.

## 10.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**Mheshimiwa Spika**, napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Kilimo, Mhe. Japhet Hasunga (Mb), Manaibu Waziri Mhe. Omary Mgumba (Mb) na Mhe. Hussein Bashe (Mb), Makatibu Wakuu wa Wizara ya Kilimo, Mhandisi Mathew Mtigumwe na Prof. Siza Tumbo pamoja na Wataalamu wote wa Wizara ya Kilimo kwa ushirikiano waliotoa wakati Kamati ilipokuwa ikichambua Azimio hili.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee nawashukuru wadau wote waliotoa michango yao kwa maandishi na kwa kufika mbele ya Kamati. Michango yao ilisaidia kujengea uwezo Kamati na kuwawezesha Wajumbe kuwa na uelewa mpana kuhusiana na Azimio hili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao waliyoitoa wakati wa kuchambua na kujadili Azimio hili. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Christine G. Ishengoma, Mb M/Mwenyekiti
3. Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb Mjumbe
4. Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb "
5. Mhe. Eng. Edwin A. Ngonyani, Mb "
6. Mhe. Katani Ahmad Katani Mb "
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb "
8. Mhe. Haroon Mulla Pirmohamed, Mb "
9. Mhe. Ritta Enespher Kabati, Mb "
10. Mhe. Mattar Ali Salum, Mb "
11. Mhe. Lucy Simon Magereli, "
12. Mhe. Justin Joseph Monko "
13. Mhe. Omar Abdallah Kigoda, Mb "
14. Mhe. Anna Richard Lupembe, Mb "
15. Mhe. Pascal Yohana Haonga "
16. Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb "
17. Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb "
18. Mhe. Devotha Methew Minja, Mb "
19. Mhe. Haji Ameir Haji, Mb "
20. Mhe. Haji Khatib Kai, Mb "
21. Mhe. Sikudhani Yasini Chikambo, Mb "
22. Mhe. Juma Ali Juma, Mb "
23. Mhe. Emmanuel Papian John, Mb "
24. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb "
25. Mhe. Anthony Calist Komu, Mb "
26. Mhe. Jitu Vrajjal Soni, Mb "

**Mheshimiwa Spika**, mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa weledi mkubwa. Kwa namna ya kipekee naishukuru Sekreterietu ya Kamati ambao ni Ndg. Virgil Mtui na Ndg. Rachel Nyega pamoja na msaidizi wa Kamati Ndg. Mwimbe John kwa

kuihudumia Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na liridhie Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika kuhusu Kulinda Hakilimiki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Dkt. Christine G. Ishengoma, (Mb)  
**M/MWENYEKITI,**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO,**  
**MIFUGO NA MAJI**  
11 Septemba, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante, sasa namuita Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Vizara ya Viwanda na Biashara, atatoa maoni ya upinzani kuhusu azimio hilo. Dakika kumi! (*Makofi*)

**MHE. CECIL D. MWAMBE - K.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, nimekuja mbele yako kutoa Azimio la Bunge kuridhia Itifaki ya *Marrakesh* inayoweza upatikanaji wa kazi zilizochapishwa kwa watu wasioona, wenye uoni hafifu au ulemavu unafanya mtu kushindwa kusoma wa mwaka 2013 (*The Marrakesh Treaty to Facilitate Access to Publish Works for Persons who are Blind, Visually Impaired or Otherwise Print Disabled*). "Yanatolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 53(6) (c) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kuwa watu wenye matatizo ya uono ni wengi sana katika jamii. Bado katika jamii zetu ni wachache sana wenye tabia ya kuangalia afya zao mara kwa mara jambo linalopelekea matatizo haya ya

macho kukomaa na hata kusambaa katika jamii. Kundi hili kubwa linakumbana na changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na kukosa haki ya kupata taarifa au maarifa ambayo hutolewa kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wenye matatizo ya uono ambao hawaoni kabisa au wale wenye uono hafifu hupata ugumu sana katika kutambua dhana mbalimbali za kujifunzia. Hii ikiwa ni pamoja na kupata machapisho ya nyaraka mbalimbali kwa kuwa wenye taaluma ya maandishi ya nukta katika jamii zetu ni kundi dogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuja kwa Mkataba huu ambao unatambua haki ya kupata elimu na maarifa kwa kupitia machapisho kwa kundi hili la watu wenye matatizo ya uono bila vikwazo ni jambo kubwa na la kuungwa mkono na kila mmoja kati yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua kuwa katika nchi yetu bado kundi hili kubwa halijapewa kipaumbele. Mpaka sasa kuna shule chache sana au taasisi ambazo ni maalum kwa watu wenye matatizo ya uono. Katika mazingira ya shule, vyo au hata mahali pa kazi kuchanganya kundi hili hukumbana na changamoto nyingi kwa kuwa upatikaji wa nyaraka katika maktaba au hata zile za kiserikali hazijaweza kupatikana kulingana na mahitaji ya kundi hili maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya kibajeti, ukosefu wa wataalam au uduni wa teknolojia ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazosababisha kundi hili kuachwa nyuma. Katika hii Itifaki itazilazimu nchi wanachama kuongeza bajeti zao hasa katika wizara zinazohusika na walemavu ili azimio hili liweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba *Marrakesh* kuhusu upatikanaji wa kazi zilizchapishwa kwa watu wasioona, wenye uoni hafifu au ulemavu unaomfanya mtu kushindwa kusoma wa mwaka 2013, ni ukombozi kwa watu hao kuweza kuwa sambamba na wenzao wasio na tatizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa muungano wa watu wasioona Duniani (*The World Blind Union*) inakadiriwa kuwa asilimia 90 ya nyaraka zote zilizochapishwa duniani kote, hazipatikani au haziwafikii kwa urahisi watu wenye uoni hafifu au wale wasioona kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa *Marrakeshi* kutokana na umuhimu wake kwa mataifa mengi Duniani, katika siku ya mwisho Mkutano wa Mabalazi uliofanyika katika Jiji la *Marrakesh*, Nchini Morocco Juni 2013 na kukubaliana kupitisha mkataba huo na hadi kufikia Julai 2016 zaidi ya mataifa 75 yalikuwa yamesaini tayari hiyo ikiwa ni ishara nzuri kwa kuunga mkono Mkataba huo. Aidha baada ya miezi mitatu yaani Septemba 30, 2016 mataifa 20 yalikuwa tayari yameridhia mkataba huo, hili ni jambo kubwa sana kwa mikataba ya kimataifa kukubalika kwa haraka sana na nchi nyingi ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya mkataba, Ibara ya 4 ya Mkataba, inatoa kazi maalum kwa nchi mwanachama, nchi ambazo zitaridhia makataba huu, kuhakikisha zinarekebisha sheria za ndani zinazohusu haki miliki. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha sheria ya *COSOTA* inafanyiwa marejeo haraka ili Mkataba wa *Marrakesh* uweze kuwa na maana inayokusudiwa kwa jamii nzima ya watu wasioona na wale wenye uwezo wa uoni wa hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jema sana katika Mkataba huu ni pale unapotoa ruhusa kwa nyaraka zinazoweza kutumiwa na wasioona kutoka mataifa mengine kuingia katika nchi ambayo tayari imeridhia mkataba, rejea Ibara ya 5 ya Mkataba (*Cross-Border Exchange of Accessible Format Copies*). Jambo hili litaongeza mawanda ya nyaraka kwa ajili ya kufanyia rejea kwa wasioona au watu wenye uwezo hafifu wa kuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 5 kifungu cha 2 (a) na (b) kama zinavyosema;

(a) *Authorized entities shall be permitted, without the authorization of the right holder, to distribute or make available for the exclusive use of beneficiary persons accessible format copies to an authorized entity in another Contracting Party; and*

(b) *Authorized entities shall be permitted, without the authorization of the right holder and pursuant to Article 2(c), to distribute or make available accessible format copies to a beneficiary person in another Contracting Party;"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nukuu ya aya hizo mbili zilizo kwenye Mkataba, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona itakuwa ni jambo zuri kutambua, haki za msingi za mmiliki wa nyaraka au kazi ambayo zimewekwa kwenye muundo ambao unawawezesha wasioona au wenye uoni hafifu kuweza kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kutumia au kubadilisha kazi ya mtu bila kutambua mmiliki halali wa kazi hiyo ni kosa. Pia tukumbuke kuwa kazi hiyo ikishawekwa katika muundo wa mandishi ya nukta nundu, mmiliki hawezi tena kuelewa kama kazi hiyo ndiyo yenyewe au maudhui yamebadilishwa kwa sababu labda yeye siyo mtaalam wa masuala ya nukta nundu. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi kuhusu Ibara hiyo ya 5 kwa ujumla wake ili kuondoa sintofahamu ambayo inaweza kutokea hapo baadaye wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya 21 ya Itifaki hii, inayozungumzia lugha 21 (*Languages of the Treaty*), inasema:-

1. *"This Treaty is signed in a single original in English, Arabic, Chinese, French, Russian and Spanish languages, the versions in all these languages being equally authentic.*

2. *An official text in any language other than those referred to in Article 21(1) shall be established by the Director*

*General of WIPO on the request of an interested party, after consultation with all the interested parties. For the purposes of this paragraph, "interested party" means any Member State of WIPO whose official language, or one of whose official languages, is involved and the European Union, and any other intergovernmental organization that may become party to this Treaty, if one of its official languages is involved".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa Mkataba huu, ni vyema sana kama Mkataba huu ukawa kwa lugha ya Kiswahili. Naomba kurudia, kutokana na umuhimu wa Mkataba huu, ni vyema sana kama Mkataba huu ukawa kwa lugha ya Kiswahili kwa manufaa mapana ya wananchi wetu. Hii itasaidia hata kuondoa migogoro pale endapo mwenye haki miliki atakapona kazi yake imefanyiwa tafsiri kwa mujibu wa masharti ya Mkataba huu bila kutambua lugha ya Kiswahili kwenye Mkataba huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho. Kama ilivyo kwa mikataba mingine ni vyema sana kama nchi tukajiandaa ipasavyo ili kuweza kutekeleza yale yanayokubaliwa ndani ya mikataba ya Kimataifa kwa manufaa mapana ya nchi na wananchi wetu kwa ujumla. Kwa kufanya hivyo, Serikali inapaswa kutathmini utoaji mzima wa fedha za miradi ya maendeleo katika sekta zote, uboreshaji wa miundombinu mbinu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili la Mkataba huu maalum kwa watu wenye uono hafifu, ni lazima Serikali ijikite katika kuboresha utoaji wa elimu kwa kundi hili ikiwa ni pamoja na kupata zana za kutosha kwa ajili ya kufundishia, uboreshaji wa maktaba zetu ili kundi hili nalo liweze kupata nyaraka, kutoa ruzuku au kodi kwa mashine za kisasa ambazo zitasaidia kundi hili kupata elimu na maarifa kama makundi mengine yoyote yaliyoko nchini kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*



**MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU  
AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA ITIFAKI YA MARRAKESH  
INAYOWEZESHA UPATIKANAJI WA KAZI ZILIZOCHAPISHWA  
KWA WATU WASIOONA, WENYE UONI HAFIFU AU ULEMAVU  
UNAFANYA MTU KUSHINDWA KUSOMA WA MWAKA 2013  
(The Marrakesh Treaty to Facilitate Access to Publish Works  
for Persons who are Blind, Visually Impaired or Otherwise  
Print Disabled (MVT) 2013) - KAMA  
YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

*"Yanatolewa kwa Mujibu wa Kanuni ya 53(6) (c) ya Kanuni  
za Bunge, Toleo la mwaka 2016*

a. Utangulizi

1. **Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kuwa watu wenye matatizo ya uono ni wengi sana katika jamii. Bado katika jamii zetu ni wachache sana wenye tabia ya kuangalia afya zao mara kwa mara jambo linalopelekea matatizo haya ya macho kukomaa na hata kusambaa katika jamii. Kundi hili kubwa linakumbana na Changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na kukosa haki ya kupata taarifa au maarifa ambayo hutolewa kwa njia ya maandishi.

2. **Mheshimiwa Spika**, watu wenye matatizo ya uono ambao hawaoni kabisa au wale wenye uono hafifu hupata ugumu sana katika kutambua dhana mbalimbali anazojifunzia. Hii ikiwa ni pamoja na kupata machapisho ya nyaraka mbalimbali kwa kuwa wenye taaluma ya maandishi ya nukta katika jamii zetu ni kundi dogo sana.

3. **Mheshimiwa Spika**, kuja kwa Mkataba huu ambao unatambua haki ya kupata elimu na maarifa kwa kupitia machapisho kwa kundi hili la watu wenye matatizo ya uono bila vikwazo ni jambo kubwa na la kuungwa mkono na kila mmoja wetu.

4. **Mheshimiwa Spika**, tunatambua kuwa katika nchi yetu bado kundi hili kubwa halijapewa kipaumbele. Mpaka sasa kuna shule chache sana au taasisi ambazo ni maalum

kwa watu wenye matatizo ya uono. Katika mazingira ya shule, vyuo au hata mahali pa kazi kuchanganya kundi hili hukumbana na changamoto nyingi kwa kuwa upatikaji wa nyaraka katika maktaba au hata zile za kiserikali hazijaweza kupatikana kulingana na mahitaji ya kundi hili maalum.

5. **Mheshimiwa Spika**, matatizo ya kibajeti , ukosefu wa wataalamu na uduni wa teknolojia ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazosababisha kundi hili kuachwa nyuma. Katika hii Itifaki itazilazimu nchi wanachama kuongeza bajeti zao hasa katika wizara zinazohusika na walemavu ili azimio hili liweze kutekelezeka.

6. **Mheshimiwa Spika**, mkataba Marrakesh kuhusu upatikanaji wa kazi zilizchapishwa kwa watu wasioona, wenye uoni hafifu au ulemavu unaomfanya mtu kushindwa kusoma wa mwaka 2013, ni ukombozi kwa watu hao kuweza kuwa sambamba na wenzao wasio na tatizo hilo.

7. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa muungano wa watu wasioona Duniani (The World Blind Union) inakadiriwa kuwa asilimia tisini ( 90%) ya nyaraka zote zilizochapishwa duniani kote, hazipatikani au hazifikiki kwa urahisi na watu wenye uoni hafifu au wale wasioona kabisa.

8. **Mheshimiwa Spika**, Mkataba wa Marrakeshi kutokana na umuhimu wake kwa mataifa mengi Duniani, katika siku ya mwisho Mkutano wa Mabalazi uliofanyika katika Jiji la Marrakesh, Nchini Morocco Juni 2013na kukubaliana kupitisha mkataba huo, na hadi kufikia Julai 2016 zaidi ya mataifa 75 yalikuwa yamesaini tayari hiyo ikiwa ni ishala nzuri kwa kuunga mkono Mkataba huo. Aidha baada ya mieze mitatu yaani Septemba 30,2016 mataifa 20 yalikuwa tayari yameridhia mkataba huo. Hili ni jambo kubwa sana kwa mikataba yakimataifa kukubalika kwa haraka sana na nchi nyingi.

b. **Mapitio ya Mkataba**

9. **Mheshimiwa Spika**, Ibara ya 4 ya Mkataba, inatoa kazi maalum kwa nchi mwanachama (nchi ambazo zitaridhia

makataba huu) kuhakikisha zinarekebisha sheria za ndani zinazohusu haki miliki, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha sheria ya COSOTA inafanyiwa marejeo haraka ili Mkataba wa Marrakesh uweze kuwa na maana inayokusudiwa kwa jamii nzima ya watu wasioona na wale wenye uwezo hafifu wa kuona.

**10. Mheshimiwa Spika**, jambo jema sana katika Mkataba huu ni pale unapotoa ruhusa kwa nyaraka zinazoweza kutumiwa wasioona kutoka mataifa mengine kuingia katika nchi ambayo tayari imeridhia mkataba, rejea Ibara ya 5 ya Mkataba (*Cross-Border Exchange of Accessible Format Copies*). Jambo hili litaongeza mawanda ya nyaraka kwa ajili ya kufanyia rejea kwa wasioona au watu wenye uwezo hafifu wa kuona.

**11. Mheshimiwa Spika**, katika ibara hiyo ya 5 kifungu cha 2 (a) na (b) kama zinavyosema;  
*“(a) authorized entities shall be permitted, without the authorization of the right holder, to distribute or make available for the exclusive use of beneficiary persons accessible format copies to an authorized entity in another Contracting Party; and  
(b) authorized entities shall be permitted, without the authorization of the right holder and pursuant to Article 2(c), to distribute or make available accessible format copies to a beneficiary person in another Contracting Party;”*

Kwa nukuu ya aya hizo mbili zilizo kwenye Mkataba, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona likatakuwa ni jambo zuri kutambua, haki za msingi za mmiliki wa nyaraka au kazi ambayo imewekwa kwenye muundo ambao unawawezesha wasioona au wenye uoni hafifu kuweza kutumia.

**12. Mheshimiwa Spika**, Kitendo cha kutumia au kubadilisha kazi ya mtu bila kutambua mmiliki halali wa kazi hiyo ni kosa, pia tukumbuke kuwa kazi hiyo ikishawekwa katika muundo wa mandishi ya nukta nundu, mmiliki hawezi tena kuelewa kama kazi hiyo ndiyo yenyewe au maudhui yamebadilishwa.

13. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Wazir atoe ufafanuzi kuhusu Ibara hiyo ya 5 kwa ujumla wake ili kuondoa sintofahamu ambayo inaweza kutokea hapo baadae wakati wa utekelezaji wa Mkataba huu.

14. **Mheshimiwa Spika**, katika Ibara ya 21 ya Itifaki hii, inayozungumzia lugha 21. **'Languages of the Treaty'**

*1. "This Treaty is signed in a single original in English, Arabic, Chinese, French, Russian and Spanish languages, the versions in all these languages being equally authentic.*

*2. An official text in any language other than those referred to in Article 21(1) shall be established by the Director General of WIPO on the request of an interested party, after consultation with all the interested parties. For the purposes of this paragraph, "interested party" means any Member State of WIPO whose official language, or one of whose official languages, is involved and the European Union, and any other intergovernmental organization that may become party to this Treaty, if one of its official languages is involved".*

15. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa Mkataba huu ni vyema sana kama Mkataba huu ukawa kwa lugha ya Kiswahili pia kwa manufaa mapana ya wananchi wetu. Hii itasaidia hata kuondoa migogoro pale endapo mwenye haki miliki atakapona kazi yake imefanyiwa tafsiri kwa mujibu wa masharti ya Mkataba huu.

**c. Hitimisho**

16. **Mheshimiwa Spika**, kama ilivyo kwa mikataba mingine ni vyema sana kama nchi tukajiandaa ipasavyo ili kuweza kutekeleza yale yanayokubaliwa ndani ya mikataba ya Kimataifa kwa manufaa mapana ya nchi na wananchi wetu. Kwa kufanya hivyo, serikali inapaswa kutathimini utoaji mzima wa fedha za miradi ya maendeleo katika sekta zote, uboreshaji wa miundombinu mbinu n.k

**17. Mheshimiwa Spika**, katika hili la Mkataba huu maalum kwa watu wenye uono hafifu ni lazima serikali ijikite katika kuboresha utoaji wa elimu kwa kundi hili ikiwa ni pamoja na kupata zana za kutosha kwa ajili ya kufundishia, uboreshaji wa maktaba zetu ili kundi hili nalo liweze kupata nyaraka, kutoa ruzuku au kodi kwa mashine za kisasa ambazo zitasaidia kundi hili kupata alimu na maarifa kama makundi mengine yoyote.

**18. Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....  
Cecil David Mwambe (Mb)

**Kny: MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI-  
WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

11.09.2019

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, kwa taarifa yenu na *Hansard* kwenye ukurasa wa 8 wa taarifa ya Kamati ya Viwanda na Biashara, kwenye *six paragraph* ya pili kuna marekebisho. Imeandikwa hapa Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mheshimiwa George Boniphace Simbachawene na inaendelea. Hii ni taarifa ya Waziri inatakiwa isomeke, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Innocent Bashungwa na Naibu wake Mheshimiwa Stella Manyanya na wataalam wote. Kwa hiyo, naomba kwa taarifa yenu na *Hansard* mfanye marekebisho hayo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaanza kuchangia na tunaanza na Mheshimiwa Ally Saleh, Mheshimiwa Haonga, Mheshimiwa Mwambe, Mheshimiwa Amina Mollel, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma na Mheshimiwa Eng. Chiza. Dakika tano, tano.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jana tulipokuwa katika mafunzo ya watu wanaoshiriki katika Mabunge mbalimbali ya Afrika, tuliambiwa kwamba nchi yetu inachelewa kuridhia mikataba. Kwa mujibu wa viwango vya mikataba hii ambayo imeletwa leo hapa lakini *specifically* huu wa Marrakesh haujachelewa kabisa kulinganisha na mikataba mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba huu ni muhimu sana kwa sababu unakwenda kusaidia kundi kubwa la watu wetu. Maelezo yanasema kwamba watu wasioona, wenye uoni hafifu na ulemavu wa kusoma (*print disabled*) na hawa baadhi ni wale ambao kwa lugha ya kiingereza wanaitwa *Dyslexia* ambao wanaona sawasawa, wana *intelligence* sawasawa lakini ni *slow learners*. Wale ambao kwenye shule tunasema mbona huyu haelewi, mbona huyu anachelewa kuelewa, nao wamekuwa *considered* katika mkataba huu. Kwa hivyo, mkataba huu unakwenda ku-cover kundi kubwa katika jamii ambalo hivi sasa linakosa fursa ambazo wangeweza kuzipata kwa kuwa mkataba huu umechelewa kuja kidunia lakini sasa hivi tayari upo na ndani ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo mengi ya kufanya kama nchi. Mojawapo ni kama ilivyosema hotuba ya Kambi ya Upinzani na hotuba ya Kamati kwamba kuna haja sasa kutengeneza sheria kwa haraka kuhusu *copyright*. Hilo liende sambamba na kuwaambia watu wetu wa ndani kwa mafunzo, maelezo na semina juu ya umuhimu wa kutengeneza kazi hizi na wao wajue kwamba kazi zao zinaweza kukuzwa ili watu kama hao waweze kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine ni namna ambavyo tunaweza kuwa na kanzi data ya uhakika ili wale ambao wanafaa kupewa hizo kazi ambazo zimekuzwa na siyo kutafsiriwa, kutafsiriwa haimo katika hili, ni kukuza maandishi ili waweze kuona basi kuwe na uhakika kwamba wanaopewa ni watu sahihi. Tunaomba pia taasisi ambayo itahusika na labda wengi wetu tunafikiri ni kama Chama cha Watu Wasiiona au Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) ambao wao ni *authorized* kwa mujibu wa

mkataba huu ili na wao waweze kutumia vizuri nafasi hiyo na wasiitumie vibaya kiasi kuweza kuathiri vibaya mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nafikiri kuna haja, kwa sababu tumechelewa kuingia katika mkataba huu ingawa siyo sana kama watu walivyosema kwamba zaidi ya nchi 70 zilishajunga, ya kwenda kujifunza kwenye nchi nyingine wamefanya nini hadi hivi sasa. Moja ya nchi hiyo ni Australia ambayo iko mbele sana katika mkataba huu. Naishauri Serikali ikafanya utaratibu, sidhani kama Afrika tumekwenda mbele sana lakini kama ziko nchi zimekwenda mbele sana basi pia tujifunze kwenye nchi za Kiafrika nini wao wamefanya japokuwa tumechelewa kujunga lakini tusifanye makosa yale tukafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni haja sasa ambapo tunasema mara kwa mara kutengeneza kanzi data. Kila siku tunaambiwa kuna kanzi data lakini jambo kama hili sasa unakuja umuhimu sana kuonesha kwamba ili tuweze kufanya makisio, ili hiyo kazi ichapishwe kwa haki ya kukuza vya kutosha ni muhimu kuwa na kanzi data juu ya watu wasioona, wenye uoni hafifu na wale ambao wana *print disabled*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ingawa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri halikuwemo kuhusu suala la Marrakesh, ametuambia hapa kwamba Zanzibar imeshirikishwa lakini ingependeza katika Waraka huu rasmi wa Bunge na *record* zikaonesha kwamba Zanzibar ilishirikishwa. Hata hivyo, ukisoma Waraka huu hamna maandishi hayo kwamba Zanzibar ilishirikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Haonga. Wale ambao wana nia ya kuchangia ambao hawatapata nafasi walete michango yao kwa maandishi. Jiandae Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba kuchangia na nitajikita zaidi

kwenye hii Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za SADC kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za Mbegu za Mimea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni kuhusu asilimia moja ya pato ghafi la Taifa kutopelekwa kwenye utafiti. Ni kwa muda mrefu sana Serikali yetu haipeleki asilimia moja ya pato ghafi la Taifa kwenye mambo ya utafiti na leo tunaenda kuridhia Itifaki hii, kama fedha hazitapelekwa tafsiri yake ni kwamba tunaenda kuwanufaisha wale ambao watakuwa tayari kupeleka fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba nchi kama Afrika Kusini imeendelea sana na iko *serious* sana kwenye mambo ya utafiti, leo tunaenda kushindana nao hao kwenye suala hili lakini kwa sababu wao wako *serious* na sisi hatujawahi kupelekea fedha huko, Serikali ituambie baada ya kupitisha Itifaki hii watakuwa tayari sasa kuanza kupeleka fedha za utafiti ili tutakachopitisha leo hapa au tutaporidhia Itifaki hii isije mwisho wa siku tukashindwa kuwasaidia watafiti wetu. Kwa hiyo, nadhani hili ni jambo muhimu sana isije kuwa tunasindika wenzetu ambao tuko nao lakini wao wamejiandaa kuliko sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu fedha za maendeleo ambazo mara nyingi hapa Bungeni tumekuwa tukizipitisha au kuidhinisha lakini fedha hizi hazitolewi. Kwa mfano, leo tunapozungumzia suala hili la Hakimiliki za Wagunduzi wa aina mpya za mbegu maana yake hizi ni fedha za maendeleo na tunajua kwenye fedha za maendeleo Serikali hii ya Awamu ya Tano naona haijajipanga kabisa kwa sababu mara nyingi sana imekuwa ikisuasua kupeleka fedha kama Bunge linavyoidhinisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwaka 2016/2017, zile fedha za maendeleo zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge hili shilingi bilioni 100.527 zilipelekwa shilingi bilioni 2.2. Sasa kama zilipelekwa fedha hizo na hapa tunapitisha Itifaki hii, je, utekelezaji wa haya mambo inakuwaje? (*Makofi*)



Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2017/2018 tulipeleka asilimia 11 tu ya fedha za maendeleo ambazo ziliidhinishwa na Bunge hili. Sasa leo tunapitisha Itifaki hii na kwenye Itifaki hapa tunaambiwa bajeti lazima itatumika, sasa inakuwaje kama hatutatenga fedha za maendeleo kwa ajili ya kwenda kutekeleza mambo haya ambayo tunaenda kuyapanga leo? Kwa hiyo, niseme tu kwamba kama Serikali haijajipanga kwenye mambo kama haya ni bora tukawa na subira ili mwisho wa siku tujipange vizuri na baadaye tuangalie namna ya kuweza kufanya lakini kama watatuhakikishia na Mheshimiwa Waziri yuko hapa kwamba fedha za maendeleo zitatolewa vizuri basi hii Itifaki itatekelezwa lakini kama hazitolewa kama ambavyo miaka ya nyuma zimekuwa hazitolewi, nadhani tutaenda kugonga mwamba na hatutafanikiwa kwenye suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni suala la mbegu za asili. Serikali ituambie wamepanga utaratibu gani kuweza kulinda mbegu za asili. Nafahamu kwamba nchi yetu tumekuwa na mbegu za asili nyingi sana na nyingine zimeanza kupotea polepole. Tulikuwa na mchele mzuri kule Kyela na zamani mnakumbuka ulikuwa unanukia, ule wa Kamsamba leo Serikali imejipangaje kutunza mbegu hizi maana zinaingia mbegu hizo mpya na za kwetu za asili zinapotea.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia. Leo nimeamua tu nichangie niweze kuongea na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa maana ya kukumbushana majukumu yetu. Ukiangalia *trend* ya michango yetu sisi wote humu ndani kama Wabunge kuanzia jana pamoja na leo na hotuba zetu sisi za Kambi jana pamoja na leo tumeamua kuunga mkono moja kwa moja Maazimio haya yaliyoletwa mbele hapa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo makusudi ili kuweza kuwakumbusha wenzetu kwamba jukumu letu la Kibunge la kwanza kabisa ni pamoja na kutunga sheria. Suala la pili ambalo ni majukumu yetu pia ni kusimamia na kuishauri Serikali katika kutekeleza mipango mbalimbali. Tukifika kwenye hiyo *junction* wote tukajua majukumu yetu kimsingi hatuwezi kuvutana kwenye haya mambo yanayojitokeza humu ndani na kuharibu *atmosphere* ya Bunge wakati fulani kwa sababu tunakaa na kusikilizana. Kwa hiyo, hali ya hewa inakuwa nzuri kabisa kama ambavyo mmeona imetokea jana na leo pia ilivyotokea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachotaka nikiseme ni kwamba haya Maazimio ambayo yamekuja mbele ya Bunge lako Tukufu, wote tunaungana mkono kusema kwamba yameletwa ndani ya Bunge hili kwa kuchelewa. Yangukuja mapema sana shida tunazozipata huko Majimboni kwetu, kwa mfano, mimi natokea Wilaya ya Masasi ambapo tuna Shule ya Msingi ya Masasi ambapo mimi nilisoma pale darasa la pili mpaka darasa la tano. Pale ndani tuna walemavu wa macho na vijana wenye uoni hafifu, wanavaa miwani lakini bado hawawezi kuona, wanatumia haya maandishi ya nukta nundu. Kipindi cha nyuma walikuwa wanatumia *Braille* ambazo ziko kama rula, wanachoma kwa vidoti wanaendelea, baadaye waka- *improve* wakaweka pale mashine, mashine zile kule ndani zimechakaa kabisa na haziwezi kuwasaidia, vijana wapya wanaoingia pale wanashindwa kupata hizi mashine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Ikupa alinisaidia na Mwalimu Kamtande alisema nikushukuru kwa sababu niliweza kupata kwa kufuatilia Serikalini mashine ya kuchapa kwa kutumia nukta nundu. Suala linalokuja na matatizo tunayoyapata, tumempelekea pale mwalimu ambaye ni mwajiriwa kabisa wa Serikali anafundisha shule ya Msingi Chibugu, bahati mbaya sana lakini kutokana na pesa anazozipata hawezi tena kutumia mshahara wake kwa ajili ya kwenda kununua karatasi maalum kwa ajili ya kwenda kuchapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapoingiza hii teknolojia mpya tunataka sasa nukta nundu zianze kutumika maalum kabisa na Serikali imeiridhia tuone na namna ya kuongeza bajeti. Bahati mbaya sana jambo limekuja baada ya bajeti kuu kupitishwa. Sina uhakika kama Wizara kuna fungu ambalo wamelitenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo limenipa mshangao, mimi ni Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara na jambo hili limewasilishwa pale na Waziri wangu wa Viwanda na Biashara, hivi kuna mahusiano gani kati ya nukta nundu na Waziri wa Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hili jambo lingekwenda kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya kulisimamia vizuri upande unaoshughulika na masuala ya walemavu na wengine, kwa mfano Wizara anayosimamia Mheshimiwa Ikupa hapa lingekuwa na maana zaidi labda na bajeti yake pale ingekwenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumesema tunaunga mkono Azimio hili, hatuna pingamizi lolote. Hata mawazo mazuri yatakayoletwa na Serikali hapa kwa kusikilizana yakianza kwenye Kamati zetu za mtambuka na baadaye yakaja ndani ya Bunge, wote tukaona tuna nia moja ya kujenga nchi yetu, Taifa letu liweze kuongea kwa lugha moja tunaweza tukafika sehemu nzuri kushauriana kwa kusikilizana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi ya kusema, nilitaka niseme tu hayo machache niwaambie kuna haja ya kuridhiana na kuweza kwenda pamoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namuita Mheshimiwa Amina Mollel ajiandae Mheshimiwa Dkt. Ishengoma na Mheshimiwa *Engineer* Chiza.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kuhusiana na Azimio hili la Mkataba wa Marrakesh.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 14 Novemba, 2017, niliuliza swali ambalo lilihusu Mkataba huu wa Marrakesh. Katika majibu yao, Serikali waliahidi kulifanyia kazi na kullileta hapa ili mkataba huu uweze kuwasaidia watu wenye ulemavu wa kutoona. Kipekee kabisa naishukuru Serikali imeonesha wa vitendo kwamba kile walichokiahidi wamekifanyia kazi. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jitihada hizi ambazo kwa kweli zinaleta faraja kubwa sana kwa watu wenye ulemavu pamoja na Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Marrakesh? Marrakesh ni kwa sababu mkutano huu ulifanyika nchini Morocco katika Mji wa Marrakesh na nchi 20 zikaridhia Azimio hili ambapo katika mkataba huo waliridhia kuhusiana na kuweza kuruhusu vitabu mbalimbali viweze kutafsiriwa kwa kuchapishwa katika maandishi ambayo yatawasaidia wenzetu wenye uono hafifu na wale wasioona. Kwa kweli kama ambavyo wengine wamesema, Serikali imefanyia kazi jambo hili haraka sana na tunawashukuru kwa hilo kwa sababu wanafunzi wengi waliokuwa wakisoma katika vyuo vikuu walikuwa wakilazimika kutafsiriwa na wakati mwingine kutafsiriwa huwezi jua nini ambacho wakati mwingine kimekosekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mkataba huu watu wasioona utaweza kuwasaidia kwa mapana zaidi ili basi maandishi mbalimbali iwe kwenye michoro, vitabu au kwa lugha nyingine zozote zile uweze kutafsiriwa na kuwasaidia kupata elimu. Elimu ndiyo kila kitu na hasa kwa watu wenye ulemavu elimu ndiyo mtaji wake. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kuleta Mkataba huu wa Marrakesh ili basi watu hawa waweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu tunafahamu kabisa kwamba hapa nchini kwetu haki ya kupata taarifa hasa kwa watu wenye ulemavu wa kutoona ilikuwa ni shida hapo awali. Kwa hivi sasa, kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano tunaona kabisa Mheshimiwa Rais amekuwa na jitihada kubwa. Kwa hiyo, Baraza la Mawaziri pia na kwa kuwa tayari

katika Baraza hilo la Mawaziri tunaye pia mtu ambaye anatuwakilisha, tunaona sasa haya yote yakifanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli Awamu hii ya Tano imekuwa na jicho la ziada katika kuhakikisha kwamba hakuna anayeachwa nyuma wakiwemo watu wenye ulamavu. Ni pongezi za pekee kwa kweli nazitoa kwa Mheshimiwa Rais pamoja na Baraza la Mawaziri na Serikali yote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika kutafsiri huku wakati mwingine wako wengine ambao watataka kujinufaisha. Naomba Serikali iwe makini kuhakikisha kwamba kile ambacho kimekubaliwa basi watu wenye ulemavu wa kutoona waweze kusaidiwa kwa haki na vile vingine ambavyo havitokuwa na manufaa basi sheria iweze kufuata mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Sheria ya Hakimiliki ambayo iko chini ya *COSOTA* tuone sasa kwamba sasa ni kwa jinsi gani iendane na mkataba huu wa Marrakesh; na yenyewe pia tuna haja na kila sababu ya kuweza kubadilisha vile ambavyo vinahitaji viingie huko na kusiwepo na kipingamizi chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwakweli kutokana na hili lililofanyika, langu kubwa ni pongezi lakini pia kuona kwamba sasa wakati huu tunapokwenda tuone na mikataba mingine ambayo kwa namna moja au nyingine bado imeachwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa mamlaka ya Kiti naongeza nusu saa. Namwita Mheshimiwa Dkt. Ishengoma na Mheshimiwa Chiza ujiandae. Wale wengine mnaweza mkachangia kwa maandishi.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Nami

najikita kwenye Azimio la Kuridhia Itifaki ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Afrika (SADC) kuhusu kulinda hatimiliki ya Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu Pamoja na Mimea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa, wagunduzi, ambao wamefanya utafiti wao wa muda mrefu, kama hii ikiridhiwa itakuwa nzuri sana kwa sababu ya kupata motisha. Watakuwa wanamotisha sana na wataona kuwa wametambuliwa na watazidi kufanya utafiti wao kusudi waweze kupata huo ugunduzi na waweze kugundua aina mpya za mbegu pamoja na mimea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili likiridhiwa, nchi yetu nayo itaweza kufaidika kwa njia mbalimbali kupitia mapato kwa sababu aina mpya hii ya mbegu za mimea tunaweza kubadilishana pamoja na nchi nyingine za SADC kwa njia ya uhalali. Hapo mwanzoni ilikuwa haibadilishwi kwa njia ya halali kwa sababu tulikuwa tumejifunga kwenye nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, vijana wetu na wenyewe watapata motisha kuweza kuchukua haya masomo ya *Plant Breeding* ambayo yatawawezesha kufanya utafiti na kugundua aina hizi mpya za mbegu za mimea kusudi waweze kutambulika na waweze kuendelea vizuri pamoja na nchi yetu kuweza kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyosema kwenye Kamati, nchi yetu itaweza kufaidika pamoja na wagunduzi kwenye mrabaha ambao pia unaweza kutumika mrabaha mwingine kuendeleza ugunduzi mpya kwenye mambo haya ya aina mbegu za mimea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe na watu wengine walikuwa wanafahamu kuwa tatizo la mbegu hasa hapa nchini ni kubwa sana, lakini kwa kuridhia huu mkataba, hawa watafiti baadaye wakigundua na kuwa wagunduzi, wataweza kujikita sana kwenye tafiti zao na kugundua aina mpya za mbegu za mimea ambazo zitaweza kuzalisha

mbegu nyingi hapa Tanzania na tutaweza kupata mbegu hizi kwa urahisi bila matatizo yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema wagunduzi, simaanishi wale ambao wamesoma tu, kuna wagunduzi wakulima ambao na wenyewe wanagundua na hawa wakulima na wenyewe itawalinda kusudi waweze kugundua aina mpya za mimea pamoja na mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira itazidi kuwepo kwa sababu vijana wengi na wakulima watajikita kwenye ugunduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo naweza kuongelea hapa ambalo nchi yetu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Dakika tano zako zimekwisha. Mheshimiwa Eng. Chiza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa hilo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami naomba niipongeze Serikali kwa kuleta maazimio haya. Kwanza hata mimi naona tumechelewa, tungeanza jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba moja kwa moja niipongeze Serikali kwa kufanya mabadiliko katika kanuni zile za matumizi salama ya bioteknolojia. Kwa wale ambao walikuwa wanafuatilia kwa jambo hili, jambo hili la *Strict liability*, hiki kipengele kwa muda mrefu kimekuwa kikwazo kikubwa sana kwa watafiti wetu katika nchi hii. Maana mtatiti anapona kwamba yeye akifanya utafiti halafu yeye mwenyewe tena anakamatwa, anashikiliwa, anaadhibiwa kwa utatiti ambao ameufanya, basi amekuwa anakosa nguvu ya kuendelea na utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Ibara hii ya 12 ambayo Mheshimiwa Waziri wa Mazingira ameileta, kwa kweli naona imeleta ahueni na motisha kwa watafiti wetu kuendelea sasa kujikita kwenye utafiti. *(Makofi)*

Mwenyekiti Mwenyekiti, mbegu bora, mbegu zenye ukinzani na magonjwa, mbegu ambazo zinazalisha, zinaleta tija katika uzalishaji ndizo tunazozitaka. Tukijifanya sisi hatutaki kufanya utafiti, tutaendelea kutumia tafiti ambazo wenzetu wamefanya uko nje ambazo haziendani na ekolojia ya nchi yetu. Kwa hiyo, tusiogope kufanya utafiti katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, nashauri tuache kabisa tabia ya kutotenga fedha za utafiti. Nakumbuka kabisa mwaka 2003 nchi yetu tulikubaliana, tuliridhia pamoja na ile nchi za SADC katika Azimio la Maputo, pamoja na nchi za AU kwamba nchi zetu zitenge kila moja asilimia kumi ya bajeti zake kwenda kwenye kilimo. Nasi tukajiongeza kwamba katika hiyo, asilimia moja iende kwenye utafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina uhakika jambo hili tumelifanya kwa wakati gani, lakini kama tumechelewa, basi huu ndiyo wakati sasa tuanze kutenga fedha hizi, watafiti wetu wafanye kazi vizuri kwa uhuru, wapate motisha ili angalau waweze kutupeleka mbele sasa katika kutafiti mbegu za mimea ili tuweze kuongeza tija katika uzalishaji hasa wakati huu ambao tutahitaji zaidi kuzalisha malighafi za kilimo kwa ajili ya viwanda vyetu vya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri, tunapokwenda kwenye utafiti huu, tunazungumza pia hakimiliki za kulinda wagunduzi. Amesema vizuri Mheshimiwa Dkt. Ishengoma, watafiti hawa hawafanyi kazi peke yao, wanafanya kazi na wakulima. Baadhi ya watu watakaoathirika na matokeo ya utafiti yakiwa ni hasi au chanya, ni wakulima.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza tuweke utaratibu, tukitenga fedha za utafiti, tutenge fedha za kutosha za kutoa elimu kwa wagunduzi, wafanyabiashara wa mbegu pamoja na wakulima wetu ikiwa ni pamoja na kuwafundisha wakulima wetu wajue haki zao ni zipi nao wanalindwaje wakati wanapopata matatizo yanayotokana na matokeo hasi yanayotokana na utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono maazimio haya kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, (Muungano na Mazingira), dakika tano.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kujumuisha au kusema kwa kifupi kwa yale ambayo yamechangiwa. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Bishara na Mazingira, Mheshimiwa Saddiq Murad na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Col. Mstaafu Masoud Ally pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Aidha, nawashukuru pia Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Eng. Joseph Mwalongo pamoja na Naibu Katibu Mkuu Balozi Joseph Sokoine na wataalam wote wa Wizara Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushiriki na kuandaa azimio hili hadi hatua hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi wachangiaji wengi kwa pande zote mbili za Kamati ikiwepo upande wa Upinzani ni kama vile wameunga mkono Nyongeza la Azimio hili la kuhusiana na masuala ya Bioteknolojia. Kusema kweli, ingawa ilielezwa hapa kwamba tumechelewa, lakini upande wa Upinzani wamesema kwamba tulipaswa kuacha kuridhia kwa sababu tumefanya hivyo kwa haraka na pengine wadau hawakushirikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Azimio hili ni nyongeza tu la Azimio la Cartagena ambalo Tanzania iliridhia mwaka 2003. Nyongeza hii ilitokana na namna ambavyo hatua za uwajibikaji na ulipaji wa fidia kwa wale watakaothirika na matumizi ya bioteknolojia ambapo kulikuwa na mvutano na kikawekwa kifungu cha 27 ili nchi ziweze kwenda kutafakari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nyongeza hii kutoka mwaka 2003 mpaka 2019 ni miaka takribani 16. Kwa hiyo, tathmini na tafakari zimefanyika sana na ndiyo maana sasa limekuja kuwekwa humu kuwa eneo au sehemu ya Azimio lile la Cartagena ambalo ilipitishwa mwaka 2000 na Tanzania tuliridhia mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwatoe mashaka kwamba ushirikiswaji haukufanyika. Siyo kweli, ushirikiswaji ulifanyika kwa kiasi kikubwa sana na kwamba hatua hii ni muhimu sana kwa sababu hatuna namna yoyote ya kuzuia madhara yanayotokana na bioteknolojia. Sisi Tanzania *basically*, hatujaanza kutumia bioteknolojia, lakini hatuna namna ya kuzuia kwa sababu bioteknolojia inaweza kukuathiri kwa namna nyingi; inaweza kuwa *direct or indirect*. Bidhaa zake tunazitumia na wapo watu inawezekana wameathirika. Kwa hiyo, kusema tusiridhie au tusite ni kuendelea kujiweka katika mazingira ambayo watu wetu wakipata madhara, hatuwezi kupata fidia au hawawezi kufidiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwanza tumechelewa, lakini sasa tumeamua na Bunge lako limeamua kukaa na kujadili na kwa kiasi kikubwa wameunga mkono. Kwa hiyo, nawashukuru sana, akiwepo mchangiaji mmoja Mheshimiwa Eng. Chiza ambaye amezungumzia kuhusiana na suala la utafiti kwamba tafiti zimeondolewa. Kwenye ule utafiti umeweka msamaha kwa hatua za kisheria kwa utafiti katika matumizi ya bioteknolojia au shughuli za kitafiti kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tu, pande zote; kwa upande wa Upinzani, Kamati na Waheshimiwa

Wabunge wote wametoa maoni mazuri. Sisi kama Serikali tumejipanga na maoni yale yaliyotolewa tutayazingatia kwamba lazima tujenge uwezo wa wataalam kubaini madhara lakini pia jamii kupata elimu ya faida na madhara ya bioteknolojia. Maoni haya yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge tumeyachukua na tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa lamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya pamoja ya ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur kuhusu Uwajibikaji Kisheria na Fidia kwa Madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya Bioteknolojia ya Kisasa katika 14 kutekeleza Itifaki ya Cartagena (Nagoya – Kuala Lumpur Supplementary Protocol on Liability and Redress on Cartagena Protocol on Biosafety, lilitidhiwa na Bunge)*)

**MWENYEKITI:** Wote wameafiki. Mheshimiwa Waziri, sasa hili ni Azimio Rasmi la Bunge na linaingia kwenye *record*. Hongera sana Mheshimiwa Waziri na Wabunge wote ambao kwa pamoja mmeunga mkono Azimio hili.

Waziri wa Kilimo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru wewe mwenye binafsi kwa kutupa nafasi. Pia nashukuru Kamati ya Kilimo Maji na Mifugo kwa michango mizuri ambayo wametoa kwa namna ambavyo wameishauri Serikali na sisi tunasema kwamba ushauri wao wote tumeupokea, tutaufanyia kazi ili tuweze kutekeleza vizuri itifaki hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa *SADC*. Kwa kweli tunampongeza sana sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuridhia itifaki hii ya maendeleo za nchi za Kusini mwa Afrika, inatupa heshima kubwa kwamba Mwenyekiti wetu sasa atakuwa na nafasi nzuri ya kuweza kutekeleza majukumu yale yote ambapo amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Nchi za *SADC*. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tuunge mkono itifaki hii kwa sababu ina manufaa makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imetoa maoni mengi kuhusu uwekezaji kwenye utafiti na wengi wameshauri kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kuwekeza asilimia moja kwenye mapato ghafi ya Taifa. Ni kweli wazo ni zuri na wengi wameshauri hivyo, tunapokea, lakini nataka niseme tu kwamba uwekezaji kwenye utafiti tunaouzungumzia ni utafiti kwa ujumla, siyo kwenye kilimo peke yake. One percent kutoka kwenye *GDP* ni kwenye utafiti wote katika Wizara nzima, iwe kwenye elimu iwe kwenye kilimo na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo, maana yake ukichukuwa kwa mfano sasa hivi pato la Taifa ambalo ni takribani zaidi ya Dola za Marekani bilioni 54, maana yake tunahitaji karibu *almost* trilioni moja kwa ajili ya uwekezaji. Ni wazo zuri, nasi Serikali tunalipokea, lakini wakati wa kupanga vipaumbele, tunaangalia kwa sababu ya mapato kidogo yanayokuwepo, vipaumbele ni nini? Tuwekeze kiasi gani? Kwa hiyo, hili tunalichukuwa, tunaendelea kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya utafiti, inatoka kwenye vyazo vya ndani, inaweza ikatoka kwa Washirika wa Maendeleo, inaweza ikatoka kwa watu binafsi. Sisi kama Serikali kwa mfano upande wa kilimo, mwaka huu tumetenga zaidi ya shilingi bilioni nane kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunafanya utafiti wa mbegu; na hizi hela tutahakikisha kwa kweli *TARI* wanafanya vizuri katika kufanikisha utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi Wagunduzi wetu wa mbegu wamefanya vizuri sana. Kwa mfano, katika Afrika sina uhakika kama kuna taasisi kama *TARI* kule Naliendele, kazi ambayo wameifanya na ugunduzi ambao wameufanya na mbegu ambazo zimegundulika, sina uhakika kwenye zao la korosho kama kuna taasisi hapa Afrika ambayo imefanya kama vile; na mbegu zetu sasa hivi zinatumika katika nchi nyingi hapa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuridhia itifaki hii, maana yake manufaa ya mbegu zetu ambazo zinatumika sasa hivi Zambia na nchi nyingine, tutakuwa na uwezo sasa wa kupata angalau mrahaba unaotokana na ugunduzi huu. Kwa hiyo, nataka kusema kwamba mambo ni mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunayo kazi ya kufanya mapitio. Sasa hivi tunapitia Sera yetu ya Kilimo ya Mwaka 2013, pia tutakuja na sheria mpya ambayo itakuwa ni jumuiifu, ambayo itarekebisha vikwazo vyote ambavyo vitafanya itifaki hii ishindwe kutekelezeka. Kwa hiyo, tutarekebisha kama tulivyoshauriwa na Waheshimiwa Wabunge na Kamati, haya yote tutayazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, pamoja na Mheshimiwa Haonga wamechangia sana namna ya kuboresha mbegu, nami nakubaliana na suala la kubadilishwa mbegu za asili. Mbegu za asili ndiyo zimetufikisha hapa, nasi tutakuja sasa hivi na sheria nyingine kwa ajili ya kulinda hizi mbege za asili. Kwa sababu ili uje na mbegu nyingine za kisasa, ni lazima hata mbegu ya asili uitambue; na utakapokuwa una-*cross*, unaunganisha, basi zote hizi tunataka tuwatambue na tuhakikishe tunalinda kwa maslahi mapana ya Taifa letu. Nina uhakika kama haya tutayatekeleza, mambo yatakwenda vizuri sana. Kwa hiyo, nilihakikishie Bunge hili kwamba itifaki hii itakuwa na manufaa makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ni nyingi tumeshazisema, kwa sababu ya muda hatutaweza kusema mengi, lakini nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote kwa

pamoja, turidhie Itifaki hii ya Ugunduzi wa Mbegu Mpya za Mimea ili ziwe na manufaa na wagunduzi wetu wapate kuwa na motisha ya kuendelea na ugunduzi na kufanya utafiti wa kila namna; nami nina uhakika mkisharidhia, wagunduzi wengi au watafiti wengi wataenda kuwekeza kule kwa sababu wana uhakika sasa wakiwekeza watapata faida na watapata mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Itifaki ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (The Protocol for Protection of New Varieties of Plant [Plant Breeder's Rights] in the Southern African Development Community – SADC) liliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Walioafiki wameshinda na Bunge zima limekubali. Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge, hongereni sana. Sasa hili linaingia kwenye *record* ni Azimio la Bunge.

Waziri wa Viwanda na Biashara, dakika tano.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja ya Mkataba wa Marrakesh. Pia naishukuru sana Kamati ya Viwanda na Mazingira kwa ushirikiano walioipa Wizara yangu katika mchakato mzima wa kuandaa azimio hili mpaka kufikia Bungeni leo hii. Nawashukuru sana Mheshimiwa Suleiman Saddiq Murad, Col. Masoud pamoja na Wajumbe wote wa Kamati ya Viwanda Biashara na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru sana Naibu Waziri Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa *COSOTA* na wataalam wote kwa kazi nzuri walioifanya katika maandalizi ya azimio hili la Mkataba wa Marrakesh.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru sana Chama cha Wasioona wakiongozwa na Mwenyekiti Lucy Benito pamoja na Emmanue Simon, Katibu; nawashukuru sana kwa kufika kwenye Bunge letu Tukufu kushuhudia azimio letu hili muhimu sana kwa walengwa wetu, ndugu zetu, watu wenye ulemavu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru sana Naibu Waziri, dada yangu Mheshimiwa Stella Ikupa, Mheshimiwa Balozi Venance Mwamoto, Mheshimiwa Dada Amina Mollel na Mheshimiwa Kaka Ally Saleh, wametoa mchango mkubwa sana katika kusukuma azimio hili liweze kufikia hatua muhimu ya leo. Nawashukuru sana Waheshimiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia, waliotoa ushauri na wale ambao hamjachangia, wote najua mnaunga mkono hoja hii. Tunawashukuru sana kwa niaba ya ndugu zetu watu wenye ulemavu, nawashukuru sana kwa kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi nimekuja kushukuru kwa sababu hoja hii haijapingwa na Mbunge hata mmoja zaidi ya kutoa maoni ushauri na tumeelekezwa na Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira pamoja na michango ya Waheshimiwa Wabunge kwamba mara tu baada ya kuridhia Itifaki, basi tujitahidi sana marekebisho ya Sheria ya *COSOTA* yafanyike haraka iwezekanavyo ili ndugu zetu walengwa waweze kunufaika na itifaki hii, nasi kama Serikali, ushauri huu tumeuchukuwa tutasukuma kwa nguvu ili mapitio ya sheria hizi yaweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na *concern* ya *copyright* kwa mwandishi wa awali, pale ambapo maandishi

yake yanahamishwa kwenye muundo wa nukta nundu, kwamba *copyright* yake, *intellectual propaties*, atapoteza ile haki, lakini napenda kuwaondoa wasiwasi Waheshimiwa Wabunge, kuhama kwa machapisho kunahama pia kwa *copyright* ya *author*. Kwa hiyo, jambo hili nilitaka kuwaondoa wasiwasi, *copyright* inahama pamoja na muundo wa machapisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Ally Saleh kama alivyopendekeza, tuna fursa ya kujifunza kutoka kwenye nchi ambazo tayari zimesharidhia. Kwa hiyo, tutaangalia *best practice* kwenye hili pamoja na mengine ili kuhakikisha mapitio na ya sera na sheria yanakidhi kiu na nia ya kuhakikisha mkataba huu unawasaidia ndugu zetu wasioona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulitolea maelezo ni suala la ushirikishwaji wa wadau. Mchakato mzima umeshirikisha wadau kikamilifu; na kwa mara nyingine niwashukuru sana ndugu zetu upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wadau wote kupitia *COSOZA* wametupa maoni mazuri sana ambayo yamepelekea kukamilika kwa mchakato wa kushirikisha wadau na kuleta azimio hili hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tutahakikisha maudhui ya itifaki yanatafsiriwa katika Kiswahili ili yaweze kupatikana kote nchini kwa walengwa wetu pamoja na suala zima la kanzidata kama ilivyoshauriwa. Kuwa na kanzidata ni muhimu sana kwa sababu itatusaidia kuwahudumia walengwa wetu vizuri. Kwa hiyo, jambo hili nalo tumelichukuwa tatalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nashukuru kwa kunipa nafasi hii tena na ninaomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.



*(Hoja ilitolewa lamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Itifaki ya Marrakesh inayowezesha  
Upatikanaji wa Kazi zilizochapishwa kwa Watu Wasioona,  
Wenye Uoni Hafifu au Ulemavu Unaofanya Mtu Kushindwa  
Kusoma wa Mwaka 2013 (The Marrakesh Treaty to Facilitate  
Access to Published Works for Persons who are Blind,  
Visually Impaired or Otherwise Print Disabled (MVT) 2013)  
Liliridhiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Wabunge wote wameafiki. Kwa pamoja nawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri kwa Maazimio haya yote matatu ambayo yamepita leo kwa muda muafaka, sasa napenda kuwaambia tu, kazi za Bunge zote za leo zilizopangwa zimekwisha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa wepesi wa kufanya kazi yetu kwa haraka na kwa uadilifu na kwa uaminifu mkubwa sana wa Taifa letu.

Naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.23 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 12 Septemba, 2019, Saa Tatu Asubuhi)*